**3 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 3 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali Waheshimiwa Wabunge; tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, sasa nimwite Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, aulize swali lake.

Na. 212

### Kuligawa Jimbo la Kilindi

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali italigawa Jimbo la Kilindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ipo katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Hivyo, kwa kuzingatia taratibu na vigezo, muda wa kugawa majimbo utakapofika tume itatoa tangazo rasmi kwa wadau wote wa uchaguzi juu ya kuanza kwa mchakato wa ugawaji wa majimbo ili wadau wawasilishe maoni na maombi yao na hivyo kushughulikiwa kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa Kikatiba, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri tu. Lakini pia nitumie nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti, hakika uko vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali madogo mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba maeneo madogo ya utawala ni tofauti na maeneo makubwa ya utawala. Sasa je, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba maeneo madogo hayapewi rasilimali nyingi na watumishi wengi kuliko maeneo makubwa ya utawala? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; nini mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba maeneo yote makubwa ambayo yako sawa na Kilindi ambayo yanahitaji kugawanywa yanafanyiwa mkakati wa haraka ili yaweze kugawanywa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Omari Kigua kwa kazi nzuri anazofanya jimboni, lakini pia niendelee kumhakikishia kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan,

tunatambua uwepo wa maeneo haya makubwa na madogo ya kiutawala. Na kama nilivyojibu katika swali la msingi alilouliza, tutaendelea kufanya kazi kuona namna ambavyo tunaendelea kufikisha huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa ufafanuzi zaidi, vigezo tunavyovizingatia katika nchi za *SADC* ikiwemo na Tanzania tutaangalia pia ukubwa wa jimbo husika, mipaka ya kiutawala, hali ya kiuchumi na hali ya kijiografia pamoja na suala la idadi ya watu katika eneo husika, pamoja na uwezo pia wa Ukumbi wetu wa Bunge na idadi ya Wabunge wa Viti Maalum; yote hayo tutayaangalia katika mchakato huu alioulizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema pia maeneo makubwa; tunatambua na tunafahamu na nimelijibu swali hili hii ni mara ya pili ndani ya Bunge lako Tukufu. Maeneo haya ambayo ni makubwa tume kama ilivyopewa majukumu na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutafanyia kazi maeneo hayo na tutaomba tuendelee kupata ushirikiano wa kutosha kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja na wadau wote wa masuala ya uchaguzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Jimbo la Mbeya Mjini ni kubwa sana na lina kata zaidi ya 36 na wapigakura wengi; ni lini Serikali mtaamua kuligawa jimbo jilo ili liweze kumpa urahisi Mbunge husika waweze kugawa namna ya kulitumikia jimbo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, nimesema Serikali tunatambua lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye ni Mheshimiwa Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia, ameshawasilisha suala hili na lipo Mezani. Kwa hiyo, muda utakapofika Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatazama pia Jimbo la Mbeya Mjini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jimbo la Kishapu lina jumla ya kata 29, lina *square kilometers* 48,000; lina vijiji 117. Eneo hili kiutawala ni kubwa sana; ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba jimbo hili linagawanywa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan inatambua uwepo wa maeneo makubwa, kama alivyosema huku Kishapu kata 26 na vijiji 117. Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao, muda

utakapofika tutaangalia vigezo na masharti ili kuona kama jimbo hili linafaa kugawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Serikali niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge wote, kwenye eneo hili yapo majimbo mengi, kwa hiyo tutayafanyia kazi Waheshimiwa Wabunge. Karibu tuungane pamoja na wadau wengine wa Uchaguzi tutoe maoni na nina imani tutafanya vizuri tu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Tabora Mjini lenye kata 29 na wakazi sasa katika sensa hii nadhani hawatapungua 500,000 kwenye jimbo moja, na tulishawasilisha maombi ya kuligawa jimbo hilo kwa muda mrefu: -

Lini Serikali itaweza kuligawa jimbo hilo ili liweze kuwa na majimbo angalau mawili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, tunatambua ukubwa pia wa Jimbo la Tabora Mjini. Lakini vilevile niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote na Mheshimiwa Mwakasaka

kwamba muda utakapofika, tume tayari tumeanza maandalizi ya uchaguzi wa mwaka 2025, tutashirikiana kwa ukaribu kuona namna ambavyo tunaweza tukagawa majimbo hayo kwa mujibu wa vigezo na masharti. Na niwaambie kwamba tutazingatia pia suala la idadi ya watu, hususan iliyotokana na Sensa yetu ya Watu na Makazi, itaendelea pia kutuongoza kwenye kipengele hicho namna ambavyo tunaweza kufanya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge; tunakushukuru sana.

Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nimuite Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 213

**Ujenzi wa Soko Kuu Lindi**

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaipatia fedha Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ili iweze kutekeleza mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Soko Kuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ni miongoni mwa miji 45 ambayo imepewa kipaumbele cha kupata ufadhili wa Mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Miji, Manispaa na Majiji ambapo ujenzi wa soko ni miongoni mwa miundombinu itakayotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha upimaji eneo la ujenzi wa soko na kupata hati yenye ukubwa wa mita za mraba 5,845 pamoja na cheti cha Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(EIA)* kutoka *NEMC* kama sehemu ya lazima katika kuanza kwa mradi huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niishukuru Serikali kwa majibu hayo yenye kuleta matumaini. Pamoja na kwamba wamechukua hatua mbalimbali za upimaji wa eneo na kuchukua tathmini ya hati ya mazingira, ninaomba niulize swali moja la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Lindi Manispaa limejengwa mwaka 1950, kwa hiyo ni soko ambalo tumerithi kutoka kwa wakoloni, ni la muda mrefu tangu Lindi ikiwa eneo dogo na sasa hivi Lindi Manispaa ina kata 31 na makusanyo ya manispaa ni shilingi bilioni tatu kwa mwaka. Makusanyo ni madogo lakini tunatoa huduma katika kata 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Serikali itaona umuhimu mkubwa wa kutupatia fedha katika kuhakikisha kwamba

tunakwenda kutekeleza mradi huu wa kimkakati wa ujenzi wa soko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua shauku ya Mheshimiwa Mbunge juu ya soko hili, na amekuwa akilipambania tangu akiwa Mbunge wa Viti Maalum na mpaka sasa ni Mbunge wa Jimbo. Na ukweli ni kwamba Manispaa ya Lindi ipo katika *Tier II* katika miradi ambayo inaanza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24, kwa hiyo nimuondoe shaka tu na wananchi wake kwamba utekelezaji wao utafanyika kama ambavyo watu wa *Tier I* sasa hivi wako katika hatua za mwisho, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale kwenye bajeti ya 2018-2020 tulitengewa fedha kwa ajili ya kujenga stendi ya kisasa kama mradi wa kimkakati, lakini fedha zile zilirudishwa kutokana na sababu zisizojulikana. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha hizo tena ili mradi ule wa kimkakati uweze kukamilika kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Bunge lako lilipitisha hapa sheria ya kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo zimeelekezwa katika miradi na kuvuka mwaka wa fedha ziendelee kubaki ili zitekeleze miradi ambayo imekusudiwa. Na jambo hili alilozungumza Mheshimiwa Mbunge maana yake sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI italifanyia kazi kulipitia ili ione namna bora ya kuhakikisha fedha zile zinarudi na kufanya kazi ambayo imekusudiwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Soko Kuu la Bukoba Mjini ni chakavu na dogo kwa matumizi ya sasa, je, lini Mradi wa *TACTIC* utaanza ili soko hilo lijengwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Manispaa ya Bukoba iko katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC (Tier II)*. Kwa hiyo nimwondoe hofu, kama ambavyo Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Stephen Byabato analifuatilia na jambo hili linakwenda kutekelezeka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye Jimbo la Ukonga tarehe 23, Februari, alitoa maelekezo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuanza mchakato wa ujenzi wa soko kwenye Kata ya Gongo la Mboto, soko ambalo litatumiwa na wafanyabiashara ambao kwa sasa wanafanya biashara barabarani na kutumiwa na zaidi ya kata tano. Je, Serikali imefikia wapi kwenye utekelezaji wa agizo hilo la Mheshimiwa Waziri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo aliyatoa ni maelekezo ambayo Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala alishaelekezwa kuyatekeleza. Kwa hiyo, ninarudia tu kumwelekeza mkurugenzi wa manispaa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa kwa muda mrefu nimekuwa nikifwatilia juu ya ujenzi wa soko la mazao pale Vwawa; je,

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba lile soko linajengwa kama ambavyo imekuwa ikiahidi kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Hasunga tunatokea katika mkoa mmoja na anatambua kabisa Soko la Vwawa liko katika Mradi wa *TACTIC Tier III* kwa hiyo, utekelezaji wa mradi utakapoanza ambapo mimi na yeye tuko katika kundi moja, maana yake na yeye atapatiwa hiyo huduma. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata, Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 214

**Shule za Sekondari Lyamahoro na Rubale kuwa za kidato cha tano na sita**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza: -

Je, lini Shule za Sekondari za Lyamahoro na Rubale zitaanza kutoa elimu ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza shule za kidato cha tano na sita katika halmashauri zote nchini kwa kuongeza miundombinu ya mabweni, madarasa na bwalo. Kupitia jitihada hizo, Shule ya Sekondari Lyamahoro imepata sifa ya kuwa Shule ya Kidato cha Tano na Sita na inatarajia kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha tano kwa Mchepuo wa *CBG* Julai, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Rubale bado haina miundombinu ya kutosha kuiwezesha kuwa ya kidato cha tano na sita. Nitumie nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na wananchi kuanza kujenga miundombinu mingine na Serikali itatekeleza kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu hayo ingawaje kuhusu *Lyamahoro Secondary School* limejibiwa hivi zaidi ya miaka miwili, kwamba inaanza mwezi ujao, lakini haijaanza. Sasa swali: -

Je, Serikali inafahamu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba nzima haina shule ya ngazi ya kidato cha tano na sita? Inafahamu hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali inafahamu kwamba tukipata shilingi milioni 80 kila shule, kwa Lyamahoro 80 na Rubale 80, shule hizi zinakamilika kuwa na kidato cha tano na sita, zinaweza zikaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua shauku ya Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha katika Halmashauri yake ya Bukoba wanapata shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita. Na ndiyo maana katika jibu la msingi Shule ya Sekondari ya Lyamahoro imeshapata sifa. Kwa hiyo, nimhaikishie tu kwamba Julai inapokuwa inaanza maana yake na shule hii itatekelezeka; kwa hiyo tunatambua kwamba hakuna na ndiyo maana utekelezaji wake unakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu kupeleka hizo shilingi milioni 80 katika hizo shule mbili ni sehemu ya fedha ambayo nafikiri itatosha tu kukamilisha baadhi ya miundombinu kwa sababu ili shule iwe na kidato cha tano na sita inahitaji bweni, bwalo, jengo la utawala pamoja na madarasa ya ziada na vyoo. Kwa hiyo kuna bajeti kidogo ambayo inahitajika kwa hiyo nimhakikishie tu kwamba Serikali itatafuta fedha ikishirikiana na halmashauri pamoja na yeye Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahasante sana. Shule ya sekondari Ifaru iko katika jimbo la Chemba mwanzoni ilikuwa na kidato cha tano na sita baadaye wakasitisha kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu. Sasa uchakavu ule tayari Serikali imefanya ukarabati. Ni lini sasa itarejesha kusajili wanafunzi wa kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mohamed Monni Mbunge wa Chemba kwamba Ofisi ya Rais *TAMISEMI* imelipokea jambo hilo na italifanyia kazi; kwa sababu moja ya malengo ya Ofisi ya Rais *TAMISEMI* ni kuhakikisha halmashauri zote nchini zinakuwa na shule za kidato cha tano na cha sita kwa sababu ya ongezeko kubwa la wanafunzi ambao wanawekwa sasa, kwa hiyo lipo katika mchakato na linafanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimuulize Naibu Waziri swali dogo; Halmashauri ya Mji wa Bunda wananchi wamehamasika na wameanza ujenzi wa Sekondari mpya katika kata ya Nyamakokoto. Ni lini sasa mtamalizia majengo manne ya shule ya sekondari Nyamakokoto ili watoto wetu wa Bunda nao wapate nafasi ya kusoma vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu pia Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ambaye amewazungumzia wananchi wa Bunda, kwamba moja ya malengo makubwa ya serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba shule zote ambazo zimeanza zinapata fedha na kumaliziwa. Kwa hiyo na hilo lipo katika mpango itapelekwa fedha kwa ajili ya kuhakikisha shule hiyo inakamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Halmashauri ya Wilaya ya Hai tayari imeshapeleka maombi ya kupandisha hadhi shule nne kutoka kidato cha nne kwenda cha tano na sita, ambazo ni shule ya Lemila, Masikia, Longoi na Mkwasa. Je, ni lini Serikali itasajili shule hizi ili ziweze kutoa elimu ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mafuwe Mbunge wa Jimbo la Hai kwamba Ofisi ya Rais *TAMISEMI* baada ya kuona shule zote zinakuwa zimeshakamilisha na kufikisha vigezo maombi ya usajili wa shule kuwa kidato cha tano na sita yanapelekwa Ofisi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo jambo hilo nafikiri lipo huko. Ofisi ya Rais *TAMISEMI* itashirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuhakikisha jambo hilo linakamilika kwa zile shule ambazo zimekidhi vigezo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Joseph Kasheki Musukuma Mbunge wa Geita Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 215

**Hitaji la Hostel Sekondari ya Rubanga – Geita**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa hosteli katika Shule ya Sekondari ya Rubanga ili iwe ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuwezesha shule za sekondari kuwa za kidato cha tano na sita ikiwemo upelekaji wa walimu wenye sifa na taaluma stahiki, ujenzi wa miundombinu ya mabweni na madarasa pamoja na upelekaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kuanzisha shule ya kidato cha tano na sita kunategemea pia eneo, pamoja na uhitaji kulingana na wingi wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na itatekeleza kulingana na uhitaji na upatikanaji wa fedha. Aidha, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita tayari ina shule tatu za kidato cha tano na sita za Kamena, Butundwe na Bugando, naomba kuchukua fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge tuimarishe shule za kidato cha tano na sita zilizopo ili kuendelea kupokea wanafunzi kulingana na uhitaji kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali hili nimeliuliza mwaka 2020, 2021 na nikajibiwa majibu haya haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametaja kwamba halmashauri ya Geita ina shule za sekondari tatu sisi halmashuri ya Geita tuna majimbo mawili, jimbo la Busanda na Jimbo la Geita. Shule mbili ziko jimbo la Busanda. Jimbo la Geita lina *population* ya zaidi ya watu laki saba na nusu, kwangu, tuna shule moja. Watoto wanalazimika kutembea kilometa 80. Sasa, bado nahitaji majibu sahihi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Nkome ina wanafunzi 9500 ina shule nne; na miundo mbinu yote ya madarasa tumejitosheleza, tunapungukiwa tu ujenzi wa bweni kwa ajili ya kufungua kidato cha tano na cha sita.

Je Serikali iko tayari kupeleka pesa kwenye kata ya Nkome ili tuweze kufungua pia kidato cha tano nasita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba majibu tuliyotoa kwa sasa ni sahihi kwa kuwa ni kweli Halmashauri ya Geita ina majimbo mawili, kwa maana ya Geita na Busanda ambao wana hizi shule za kidato cha tano na sita tatu. Ninajua mahitaji makubwa ambayo yako pale, ndiyo maana kwa sasa tumesema tunaendelea kuziimarisha ili kuongeza idadi ya wanafunzi wakati tunatafuta fedha kuhakikisha tunaongeza shule nyingine. Kwa hiyo nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inapopata fedha itafanya hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu hii Shule ya Sekondari Nkome ambayo ina idadi kubwa ya wanafunzi na wanahitaji Bweni tu. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais *TAMISEMI* niseme ombi hili tumelipokea na litafanyiwa kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kakonko inayo shule moja tu ya kidato cha tano na sita, ambayo ni Shule ya Sekondari Kakonko, lakini tunazo Shule za Sekondari Nyamtukuza, Mhange, Shuhudia, Kasanda na Gwanum ambazo zina sifa, kwa maana ya kwamba zina madarasa lakini hatuna hosteli.

Je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kujenga hosteli ili wanafunzi waanze kupokelewa kidato cha tano na cha sita? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Kakonko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba mahitaji ya shule za sekondari kidato cha tano na sita yanapewa kipaumbele kwenye takriban majimbo mengi kwa sasa; na ndio maana katika jitihada zake Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kutafuta fedha mliona, kwamba kwa kushirikiana na kampuni ya madini *African Barrick* walipewa dola milioni, takriban bilioni 70, ambazo ni kwa ajili ya ku-*support* elimu nchini. Fedha hizo zimeelekezwa katika ujenzi wa miundombinu ya kidato cha tano na sita. Kwa hiyo lengo la Serikali ni kuhakikisha hii adha inaondolewa. Kwa hiyo Mheshimiwa Kamamba nikuondoe hofu kwa sababu iko katika mipango ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina shule moja tu ya sekondari ya kidato cha tano; lakini inazo shule mbili ambazo zina sifa ya kuwa kidato cha tano, Shule ya sekondari ya Mpotola na Shule ya Sekondari Makukwe, lakini tuna shindwa kwa sababu hatuna mabweni au hosteli.

Je, ni lini Serikali itatuunga mkono kutujengea hosteli ili tuanze kidato cha tano na cha sita katika shule hizo mbili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda Mbunge wa Newala vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu na yeye, kwamba Serikali imesikia na imepokea hayo maombi na itayafanyia kazi kwa kadri ambavyo tunatafuta fedha ili kuhakikisha wananchi wake wanapatiwa hiyo huduma ya kidato cha tano na sita na Watanzania wote kwa ujumla, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusukuru kwa kunipa nafasi. Shule ya Sekondari ya Mkonoo iliyopo katika Jiji la Arusha ina madarasa kumi yaliyojengwa kwa fedha za uviko. Madarasa hayo yamekamilika na yana samani zote; lakini kwa sababu ya umbali madarasa haya hayajaanza kutumika hadi leo, takribani miezi sita sasa.

Je, Seikali haioni haja sasa kujenga hosteli kwenye shule hii ili madarasa haya yaanze kutumika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shule hiyo madarasa yameshakamilika na miongoni mwa halmashauri ambazo zina mapato makubwa ni pamoja na Jiji la Arusha. Kwa hiyo nimwelekeze tu Mkurugenzi wa Jiji kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni hilo ili shule hiyo iweze kupata usajili na kusajiliwa kama ambavyo maombi ya Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa tatizo hili la uhaba wa hosteli katika shule za Serikali nchini limekuwa kubwa sana;

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa una haja kubwa ya kupeleka timu katika halmashauri zote ili kuratibu na kuona upungufu ulivyo mkubwa na hatimaye kuja kuiweka kwenye mipango ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kwa maoni ambayo ameyatoa. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeyasikia na hivyo itayafanyia kazi kwa kuunda timu maalum ambayo itazunguka maeneo yote ili ipitie na kugundua ukubwa wa changamoto ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Shule ya Sekondari ya Busagara na Shule ya Sekondari Kumgogo zilizoko katika Jimbo la Muhambwe zina miundombinu ya madarasa kwa ajili ya kuanzisha kidato cha tano na cha sita.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga hosteli ili tuweze kuanza huduma ya kidato cha tano na sita katika shule hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi Mbunge wa Jimbo la Mhambwe. Kama ambavyo nimeeleza hapo awali katika majibu mbalimbali ambayo nimeyatoa kwa waheshimiwa Wabunge, nimwondoe hofu kwamba sehemu ya timu ambayo itatumwa nafikiri itatumwa kupokea maoni yote ambayo Wabunge wote wameeleza; mapungufu katika shule ambazo tunaweza kuongeza aidha hosteli, bweni ama jengo la utawala na zikatumika kama kidato cha tano na sita zikiwemo za jimbo lako. Kwa hiyo waondoe hofu wananchi wa Muhambwe kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo kazi na itafanya kazi hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyangeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga hosteli katika Shule za Sekondari za Meatu na Kimali ili kuwapunguzia wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu kwa kifupi Mheshimiwa Minza Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Simiyu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaeleza nia ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuongeza shule za kidato cha tano na cha sita nchi nzima ikiwemo katika Mkoa wa Simiyu. Kwa hiyo niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge wote kwenye dhana hii, kwa sababu fedha inatafutwa na sehemu ya fedha imeshapatikana ambayo itaelekezwa katika halmashauri zenu kwa ajili ya kuongeza mabweni sehemu zingine mabwalo ya chakula sehemu nyingine madarasa na vyoo ili tuweze kuzisajili na kuzifungua. Kwa hiyo hofu hiyo iondolewe kwa waheshimiwa wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq swali la nyongeza.

*(Hapa Mhe. Fatma H. Toufiq hakusimama kuuliza swali la nyongeza)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika inazo shule za Kalema, Kabungu pamoja na Bulamata, ambazo zina tatizo kubwa sana la ukosefu wa mabweni.

Je, ni lini Serikali watapeleka fedha ili waweze kujengewa mabweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Tanganyika na halmashauri ya Tanganyika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni kwamba Serikali bado inaendelea kutafuta fedha, na sehemu ya fedha ambayo imeshapatikana katika awali tayari kuna maeneo ambayo tayari imeshaelekeza kuhakikisha kwamba zinafunguliwa shule za kidato cha tano na sita na zianze kufanya kazi. Kwa hiyo hata haya maombi yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha hapa yatawekwa katika mpango ili Serikali iweze kuyatekeleza kwa kutafuta fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga hosteli katika Shule ya Sekondari ya Nasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la

nyongeza la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu kama ifiatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa shule ambazo ziko katika mpango wa Serikali kuongezewa hosteli ni pamoja na shule ya Sekondari Ngaza ambayo Mheshimiwa Mbunge ameianisha hapo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khalifa Mohamedi Issa Mbunge wa Mtambwe sasa aulize swali lake.

Na. 216

**Kero za Muungano zilizoibuliwa na kutatuliwa**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza:-

Je, ni kero zipi za Muungano zilizoibuliwa na kutatuliwa toka kuasisiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ?

**MWENYEKITI:** Mhehimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa Mbunge wa Mtambwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimejadili na kuzipatia ufumbuzi jumla ya changamoto 22, ambapo baadhi ya

changamoto hizo ni gharama za kushusha mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayotoka Zanzibar, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, utaratibu wa vikao vya kamati za pamoja za SJMT na SMZ vya kushughulikia masuala ya Muungano. Aidha, changamoto zote zilizopatiwa ufumbuzi zimefafanuliwa kwa kina na zinapatikana kupitia tovuti yetu ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizobakia kutatuliwa ni nne, ambazo ni Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Usajili wa Vyombo vya Moto, Uingizaji wa Sukari katika Soko la Tanzania Bara, na Mgawanyo wa Mapato Yatokanayo na Hisa za *SMZ* zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na Faida ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna msemo wa kisheria unasema, kwa tafsri yangu mimi, haki inayocheleweshwa ni haki inayonyimwa. Kwa kuwa mfuko wa pamoja wa fedha ni takwa la kisheria na ni muda mrefu sasa jambo hili linapigiwa makelele haujaundwa;

a) Je, ni nini *commitment* ya Serikali juu ya kuundwa kwa mfuko huu?

b) Je, ni lini Zanzibar itapata mgao wake wa hisa wa iliyokuwa *East African Currency Board* na faida katika Benki Kuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu masuala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa Mbunge wa Jimbo la Mtambwe. Kwanza nataka nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Khalifa amekuwa ni mfatiliaji mzuri wa masuala haya ya Muungano ambayo yanagusa mustakabali wa nchi zetu zote mbili. Mheshimiwa Khalifa hongera sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba moja miongoni mwa mambo ambayo hayajapatiwa ufumbuzi kama sehemu ya changamoto ni hili jambo la uundwaji wa hii kamati au Tume hii ya Pamoja ya Fedha. Tume hii ilikuwepo bahati nzuri imekwisha muda wake. Hata hivyo, sisi tayari tumeshapeleka mapendekezo kwa ajili ya kuteuliwa kwa tume hii. Nimwombe tu Mheshimiwa Khalifa awe na subra ili sasa tuzipe mamlaka zinazohusika zifanye uteuzi wa tume hii ili lengo na madhumuni sasa mambo haya ya muungano yaweze kwenda vizuri kama ambavo yanatakiwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu swali la msingi kwa upande wa swali la pili; ni kwamba changamoto hizi zilikuwa ziko nyingi, lakini kupitia Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Hassan tumefanya juhudi kubwa kupitia kamati zilizoundwa za pande zote mbili. Kwa hiyo nimwambie tu kwamba huu mgawanyo ambao ameuzungumza unakwenda kupatiwa ufumbuzi na tutahakikisha kwamba tunafanya moja miongoni mwa jambo muhimu la utatuzi wa hii changamoto kwenye changamoto ama miongoni mwa haya mambo ya muungano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa kero za Muungano, ingawa Mheshimiwa Waziri hapa amejibu, anasema kwamba kero ya bandari imetatuliwa; lakini hadi jana nimepokea simu kutoka kwa wananchi ambao wamesafiri kutoka Zanzibar wamekuja Dar es Salaam na wamezuiwa mizigo yao midogo midogo bandarini. Nataka kujua, Serikali ituambie hapa;

Je, ni lini watalikomesha jambo hili na kero hii kuisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu suala la nyongeza la Mheshimiwa Asia Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kikao chetu ambacho tulikaa tarehe 6 Disemba, 2022, miongoni mwa maazimio ambayo tuliazimia, kwa sababu kama nilivyosema kwamba suala la utatuzi wa changamoto za Muungano limeundiwa Kamati Maalum, kuna Kamati ya Wataalam, kuna Kamati ya Makatibu Wakuu lakini kuna Kamati ya Mawaziri. Kwa hiyo, mpaka tarehe hii tulipokaa tulikubaliana na tukatoa maelekezo kwa *TRA* na *ZRA* na Wizara zinazohusika kulifanyia kazi suala hili na kutoa mapendekezo ya ni kipi kinatakiwa kilipiwe na kipi ambacho hakitakiwi kilipiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira, hili jambo tunalifuatilia na tunahisi tunapokwenda kwenye kikao kijacho tutalipatia ufumbuzi. Nawaomba Watanzania waendelee kuwa

na subira, Serikali zote mbili zinazifanyia kazi hizi changamoto za Muungano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, sasa aulize swali lake.

Na. 217

**Ujenzi wa vituo vya abiria vya Bugorola Ukara na Kisorya – Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Vituo vya Abiria vya Bugorola, Ukara na Kisorya Ukerewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Godfrey, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* katika mwaka wa fedha 2022/2023, umetenga fedha kiasi cha shilingi 332,220,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Abiria vya Bugorola, Ukara na Kisorya katika Wilaya ya Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TEMESA* imeingia makubaliano na Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA* - Mwanza) kwa ajili ya kufanya usanifu wa miundombinu ya majengo na mchanganuo wa makadirio ya gharama husika. Taratibu za kumpata Mkandarasi atakayejenga miundombinu hiyo zitatekelezwa baada ya usanifu kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nishukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa kituo cha Bukimwi kinachopokea abiria kutoka Kayenze nacho vile vile hakina Banda kwa ajili ya abiria kusubiri usafiri. Je, ni sehemu ya vituo vitakavyofanyiwa ujenzi kama ilivyo Bugorola, Kisorya na Ukara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kivuko cha kutoka Kitale kwenda Ilugwa na kingine kutoka Kakukuru kwenda Ghana ni vivuko vilivyoko kwenye maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020 - 2025. Je, Serikali ina mpango gani kuanza ujenzi wa vivuko hivi kwa ajili ya kuokoa maisha ya wananchi kwenye eneo hilo? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwa awamu. Nikiri hivi vivuko alivyovisema viko kwenye ilani, lakini katika Ziwa Victoria tunajenga vivuko vipya vinne na katika Vituo vya

Bukimwi – Kayenze vituo hivi kwa sasa haviko kwenye mpango wa kuvijenga kwa mwaka huu wa fedha labda kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vituo alivyovitaja vya Kitale – Ilugwa, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu na tuna uhakika kadri idadi ya watu inavyoongezeka kuna haja kubwa sana ya kuongeza vituo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa visiwa hivi kwamba Serikali inafahamu na tunalifanyia kazi kutafuta fedha kuhakikisha kwamba tunakuwa na mawasiliano katika vile vivuko alivyovitaja vya Kitale, Ilugwa hadi Ghana, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. TEYA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Daraja la Kijazi ile *flyover* ukipita inavutia na imenyooka, sasa ukiendelea kule mbele ukapita kwenye ile *flyover* pale *VETA* yaani sisi tunaoangalia inaonekana pale juu ukingo ule umepinda. Mheshimiwa Waziri, anasemaje kuhusu ile? Inaleta picha mbaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Serikali tuchukue na tuliangalie kama limepinda ama ni *design,* halafu tutakuja kulitolea majawabu kama tatizo lilikuwa ni usanifu ama tatizo lilikuwa ni Mkandarasi kama anachosema Mheshimiwa Mbunge kitaonekana kwamba kina mapungufu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mbeya ni jiji lakini hatuna stendi kubwa ya kutosha, stendi ile ni ndogo lakini hata taa haina. Je, ni lini Serikali itajenga stendi kubwa ya kutosha kwenye Mkoa wetu wa Mbeya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu tulichukue kama Serikali na tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ambao hasa kwa kweli ndio wanaohusika na kujenga stendi hizi kwenye miji na majiji na kama *TANROADS* tutahitaji kusaidia, basi tutafanya hivyo ili Mkoa wa Mbeya hasa Jiji la Mbeya liweze kupata stendi kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu sasa aulize swali lake.

Na. 218

**Mwongozo wa taa bora za barabarani**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, Serikali imetoa mwongozo gani kuhusiana na kiwango cha ubora wa taa zinazowekwa barabarani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijatoa mwongozo rasmi kuhusiana na ubora wa taa zinazowekwa barabarani. Kwa sasa, Wizara imekasimisha shughuli za usimikaji wa mifumo ya umeme ikiwemo taa za kuongozea vyombo vya moto *(traffic lights)* na taa za usalama barabarani *(street lights) kwa* Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* ambapo hutoa msawazo *(specifications)* wa taa kwa Taasisi nunuzi unaoendana na mazingira na teknolojia ya wakati husika kwa viwango vya kimataifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kutoa masikitiko yangu kwa Serikali, majibu yaliyotolewa na Serikali kiukweli hayaridhishi. Kama Serikali yenye wajibu wa kutoa mwongozo kuhusu namna gani taa za barabarani ziwekwe haijatoa mwongozo mpaka sasa, hali hii inasababisha mamlaka zilizokasimiwa kufanya shughuli hii kuweka taa za barabarani kwa utaratibu wanaotaka wao. Kwa sasa hivi ukiangalia maeneo mengi taa zilizowekwa barabarani ni hafifu mno, hazina ubora, lakini bado taa hizo hizo zilizowekwa barabarani zimewekwa aidha upande mmoja hali ya kwamba ikitokea labda zimeungua eneo hilo linabaki giza. Hata hivyo, taa hizo hizo hazifanyiwi *maintenance* kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, Serikali iko tayari sasa kama yenye mamlaka kutoa waraka au mwongozo

ili mamlaka zilizokasimiwa ziweze kuleta maana halisi ya uwekaji wa taa barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Jimbo langu la Ulyankulu tangu kuundwa kwake halijawahi kuwa na barabara ya lami hata kilomita moja. Hata hivyo, kwa sasa kuna ujenzi wa kilomita moja na nusu ambao unatekelezwa kama ahadi ya Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Je, Serikali iko tayari kwanza kumalizia kilomita moja na nusu ya lami iliyobakia na kuweka taa za barabarani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rehema Juma Migila, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TEMESA* ndiyo ambao wamepewa kazi ya kuweka na kusimamia taa za barabarani. Pia *TEMESA* ndio wataalam wa kufanya kazi hizo kwa upande wa Serikali. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kwamba taa kulingana na teknolojia inavyobadilika unaweza ukasema utaweka taa hizi lakini kadri teknolojia inavyobadilika taa zimeendelea kubadilika. Zamani tulikuwa tunatumia umeme sasa hivi tunatumia *solar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama unaweza ukaweka Mwongozo unaweza pia ukawa unashindwa kwenda na teknolojia. Ndiyo maana katika jibu langu la Msingi nimesema wanakwenda kulingana na mabadiliko ya teknolojia na nini wenzetu duniani wanachofanya na wataalam ndicho wanachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwamba pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna aina mbili ya barabara na tuna taasisi mbili zinazosimamia barabara. Katika Mkoa wa Tabora ambao Mheshimiwa Mbunge anatoka, katika mtandao wa taa mkoa mzima tuna taa 1,568 mpaka leo ninavyoongea ni taa 50 tu ambazo haziko katika mtaa mmoja ambazo ni mbovu. Kwa hiyo, inawezekana barabara anayoisema inawezekana si barabara ambayo pengine inasimamiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. Hata hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama kuna changamoto ambayo mtaa mzima hauna taa nitaomba baada ya hapa tukutane naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ulyankulu tutakamilisha ujenzi na tutamwekea taa za barabarani 47 katika kituo chake hicho cha Ulyankulu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omary Ali Omary, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 219

**Hitaji la magari Jeshi la Polisi – Kaskazini Pemba**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuiliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka magari kwa jeshi la polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kulipatia Jeshi la Polisi magari kama nyenzo ya kutendea kazi. mwaka 2022, Mkoa wa Kaskazini Pemba ulipatiwa magari matatu (3) yaliyonunuliwa na Serikali ili kupunguza uhaba wa magari katika mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bajeti yake ya mwaka wa fedha 2022/2023, imetoa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 15 kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya kununulia magari na pikipiki. Pindi magari na pikipiki yatakapopokelewa yatagawiwa kwenye mikoa na wilaya zenye uhitaji mkubwa ikiwemo Mkoa wa Kaskazini Pemba, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa taarifa nilizokuwa nazo kwamba magari ya polisi yaliyoko Mkoa wa Kaskazini Pemba ni mawili tu. Je, hili gari moja limekwenda sehemu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Jeshi La Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba lina magari machakavu mengi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatengeneza magari haya au kuyapiga mnada?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa alizonazo yeye ni magari mawili, lakini taarifa nilizopewa na *IGP* ni magari matatu. Tutafuta hilo la tatu liko wapi, kama limepelekwa mahali fulani tutahakikisha linapelekwa Pemba ili magari matatu yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchakavu wa magari, tutafanya tathmini kama kawaida ilivyo kwa mali za Serikali, magari yaliyochoka yanafanyiwa tathmini, yanayoweza kufanyiwa ukarabati au matengenezo yakarejea barabarani yanafanyika, yale yanayoshindikana huuzwa kwa utaratibu unaosimamiwa na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, tutafanya tathmini ya haraka ili yale yaliyo machakavu kabisa tuyaondoe kwenye daftari kwa kuyauza na yale yanayoweza kutengenezeka yafanyiwe matengenezo, yasaidie usafiri wa vijana wetu, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Kahama ina mwingiliano mkubwa sana wa raia wa kigeni lakini Ofisi ya *Immigration* katika Wilaya ya Kahama haina gari kabisa na haina kabisa usafiri. Inafikia hatua mpaka viongozi wa uhamiaji wanakimbizana na raia wa kigeni kwa kutumia pikipiki ambayo ni hatari sana kwenye maisha yao. Je, Serikali itapeleka lini gari la Uhamiaji katika Wilaya ya Kahama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inaendelea kuimarisha kuviwezesha vyombo vyake vya usalama ili viweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Bahati mbaya katika swali la msingi huwa tunauliza polisi na hili limekuja kwa *Immigration*. Tutafuatilia Idara ya *Immigration* kuona uwezekano wa kuwapatia watu wa Kahama gari kulingana na changamoto ya wageni na shughuli za kibiashara nyingi zilizopo katika Mji wa Kahama. Kwa hiyo tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili kuona namna ya kutanzua tatizo hilo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka 2015 nilipata msaada wa gari la Polisi kutoka Japan, nikalipeleka kwenye Kituo cha Afya cha Gonja ambacho kiko Kata ya Maole. Mimi mwenyewe nilifuatilia, Serikali ilikuwa hailiangalii lile gari mpaka sasa hivi sijui lina hali gani. Je, Waziri ataniambia leo Serikali itakwenda kuliangalia lile gari lirudi barabarani kama nilivyolileta kutoka Japan?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuahidi Mheshimiwa Malecela Anne Kilango, kwamba binafsi nitalifuatilia kuona hilo gari liko wapi na ni changamoto gani inayosababisha lisiende kuwahudumia watu wa Gonja kama ilivyokusudiwa na Mheshimiwa Mbunge katika jitihada zake za kutafuta gari hilo. Namuahidi Mheshimiwa nitalifuatilia kwa kina baada ya kikao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika wilaya ya Kilwa Jeshi letu la Polisi lina gari chakavu sana. Je, ni lini Serikali itapeleka gari jipya kwa ajili ya matumizi ya Jeshi letu la Polisi, Wilayani Kilwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba katika mwaka huu wa bajeti tunaoendelea nao, Serikali imetutengea bilioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa magari na ahadi yetu ni kwamba ma-*OCD* wote watapata mgao wa magari haya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndulane kule Kilwa pia watapata mgawo wao, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Azan, swali la Nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, Serikali itapeleka lini magari katika Mkoa wa Kusini, Pemba ambao una uhaba wa magari hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurejea jibu langu la msingi kwamba, mara tutakapopokea magari yatakayonunuliwa kwa bilioni 15 tulizopewa na Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mkoa wa Kusini Pemba pia ni moja ya maeneo yatakayogawiwa magari hayo. Namwondoa mashaka Mheshimiwa Maida kwamba Mkoa wake pia utapata gari, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 220

**Kupunguza ajali Kaskazini B – Unguja**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza ajali zinazosababishwa na magari ya mchanga Wilaya ya Kaskazini B - Unguja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Kaskazini A na B – Unguja ajali zilizotokea kuanzia Januari, 2021 hadi Desemba, 2021 ni tatu ambazo zimesababisha vifo vya watu wanne na majeruhi mmoja. Ajali zilizotokea kuanzia Januari, 2022 hadi Machi, 2023 ni moja na imesababisha kifo cha mtu mmoja. Kwa jumla kesi zilizofikishwa mahakamani ni nne na zilizopata hukumu ni tatu na kesi moja inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali zinazosababishwa na magari ya kubeba mchanga zimeendelea kupungua kutokana na Serikali kuweka alama za matumizi ya barabara, kuweka Kituo cha Ukaguzi wa Magari, kukagua leseni za madereva, kuweka utaratibu wa kupima macho na kutoa elimu ya matumizi bora na sahihi ya barabara kwa watumiaji wote, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soud, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na kwamba takwimu haziko vema na ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri apate muda akajiridhishe na hizo *data* au takwimu zilivyochukuliwa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa magari ya mchanga yanasababisha sana ajali za daladala pamoja na ajali za bodaboda hasa katika maeneo ya Kaskazini A Kule Nungwi na maeneo ya Donge kwa ujumla wake. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana mpango gani wa kukaa na Wizara za Mawasiliano pamoja na Wizara husika kule Zanzibar ili kuweza kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa tatizo la magari ya mchanga kwenda mwendo wa kasi ni tatizo sugu hivi sasa. Je, Mheshimiwa Naibu Naibu Waziri haoni haja ya kukaa na taasisi inayoshughulikia masuala ya usafirishaji wa mchanga pamoja na maliasili isiyorejesheka ili kukaa na kuratibu utaratibu mzima wa leseni pamoja na utaratibu wa kusafirisha hizi rasilimali za mazao yasiyorejesheka? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza takwimu hizi nimeletewa na Kamisheni ya Polisi Zanzibar, kwa hiyo nina Imani zimetoka kwenye mamlaka sahihi. Hata hivyo, kwa vile amesema tujiridhishe, mimi na yeye tutashirikiana kuzifuatilia, kama ana

*source* nyingine yenye takwimu tofauti na hizi tutasaidiana kuona ni zipi ni sahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu magari haya kusababisha ajali kwa wingi kama alivyoeleza, kwa takwimu zetu kunaonekana kuna dalili ya kupungua. Hata hivyo, nieleze hata kama gari inabeba mzigo au ni mfanyabiashara na nini, anapoingia barabarani lazima azingatie Masharti ya matumizi ya barabara na kwa maana ya Sheria ya Usalama Barabarani inamhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari haya kusababisha ajali kwa wingi kama alivyoeleza, kwa takwimu zetu inaonekana kuna dalili ya kupungua, lakini nieleze hata kama gari inabeba mzigo ama ni mfanyabishara na kadhalika, anapoingia barabarani lazima azingatie masharti ya matumizi ya barabara na kwa maana Sheria ya barabarani inamhusu. Kwa hiyo, kwa hawa wanaobeba mchanga ninashauri nchi nzima siyo tu lile eneo la Mheshimiwa Soud alilolieleza kwamba, kwanza inatakiwa ule mchanga ufunikwe ili usitoe vumbi wanapokuwa wanaendesha yale magari. Pili wahakikishe magari yale ni mazima yanapoingia barabarani na madereva kwa kweli wawe *sober enough* wasiwe wamekula vilevi wakasababisha ajali kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu na kupitia Bunge lako Tukufu nimwelekeze *IGP* kupia Kamisheni ya Polisi Zanzibar waimarishe usimamizi wa eneo hili lililobainishwa na Mbunge, eneo la Nungwi na maeneo ya jirani ili kukomesha kabisa ajari za namna hiyo. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nashukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa

Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima aulize swali lake

Na. 221

**Mahakama za Ardhi chini ya mhimili wa Mahakama**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mahakama ya Ardhi chini ya Muhimili wa Mahakama ?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi unaanzia katika ngazi ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata ambayo yote yana mamlaka ya kufanya usuluhishi. Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ndiyo yenye jukumu la kutatua migogoro ya ardhi nchini ambapo ikiwa mtu hakuridhika na uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba ya Wilaya atakata rufaa kwenda Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa Mahakama ya Ardhi napenda kumfahmisha Mheshimiwa Mbunge kuwa katika Mahakama Kuu kuna Divisheni maalum ya Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufanya

maboresho katika Marabaza ya Ardhi ili kuangalia namna bora ya kuyawezesha ikibidi ihamishiwe katika Muhimili wa Mahakama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Songe swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ahsante kwa majibu ya Serikali.

Kwa kuwa, ufanisi wa Mabaraza umekuwa mdogo sana kwa sababu hayapo kila Wilaya, ukilinganisha kwa mfano Itilima wanapata huduma Maswa, Meatu wanapata huduma Maswa na tumefanya wanachi kuingia gharama kubwa bila sababu za msingi. Ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 74(1) ukurasa wa 179, imeeleza kwamba Mabaraza haya sasa yahamishiwe kwenye Muhimili wa Mahakama.

Je, ni lini Serikali itaanza mchakato huo na kuukamilisha mapema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na naomba nijbu swali moja la Mheshimiwa Simon Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Simon kwa kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Wizara yetu ya Katiba na Sheria pamoja na Wizara ya Ardhi pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama na mfumo mzima wa Mahakama wako kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mjadala huu wa kuhamishia Mabaraza haya kwenye Muhimili wa Mahakama kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeeleza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 222

**Bei ya pembejeo za kilimo**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kushusha bei ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo ili kuongeza uzalishaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kupunguza gharama za upatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya kilimo. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu bora kwa mazao ya alizeti, miche ya chikichi, parachichi, chai na kahawa pamoja na viuatilifu vya mazao ya korosho, pamba na viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea ikiwemo viwavijeshi, inzi, panya, kweleakwelea na nzige.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya tani 349,922 za mbolea zimenunuliwa na wakulima 799,937 kwa bei ya ruzuku. Vilevile, Serikali imetoa jumla ya lita 48,033 za viuatilifu vya kudhibiti viwavijeshi, *ekapaki* 1,823,688 za viuatilifu vya pamba, tani 15,015.03 na lita 2,684,470.5 za viuatilifu vya zao la korosho, tani 1,004 za mbegu bora za alizeti na miche bora 61,486,981 ya mazao mbalimbali kwa utaratibu wa ruzuku. Aidha, utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima utaendelea kufanyika kulingana na bajeti ya Serikali.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa, mawakala ambao walitakiwa kutoa mbegu katika Jimbo la Arumeru Magharibi wamekataa kutoa mbegu kwa madai kwamba Serikali haijawalipa fedha zao na kusababishia wakulima kutopata mbolea katika maeneo husika. Je, nini kauli ya Serikali kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hawa kwa haraka ili waweze kupata mbolea hasa katika msimu huu wa kilimo?

Swali la pili, kwa kuwa Mawakala hawa wanateuliwa na Wizara moja kwa moja kwenda kwenye Majimbo au Halmashauri.

Je, Serikali haioni sasa ifanye jambo la haraka kuwateua mawakala wa uhakika watakaokwenda kutoa huduma hiyo kwa wananchi hawa ili waendelee kupata huduma?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba Mawakala hawajalipwa fedha zao na ndiyo sababu ya kutokupeleka mbolea ya ruzuku kwa wananchi jambo hilo sidhani kama lina ukweli wowote, isipokuwa ni kwamba Serikali inafanya taratibu za kumalizia malipo kwenye baadhi ya Mawakala ambao watalipwa na kazi yao itafanyika, lakini kigezo cha kutokulipwa kwa sababu hiyo ni kigezo ambacho Serikali kupitia Wizara ya Kilimo haioni kama ni njia muafaka wa kuwasaidia wakulima na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawataka Mawakala wote kutekeleza yale maelekezo ya mikataba ambayo walisaini kati ya Mawakala na Wizara ya Kilimo. Pia kuteua Mawakala wa uhakika jambo hilo tumelipokea na ndiyo maana katika awamu hii iliyofanyika, maana yake imetoa somo kwa Wizara ya Kilimo ambalo katika mwaka unaokuja maana yake itazingatia yale mapungufu yaliyojitokeza mwaka huu ili yasiweze kujitokeza katika msimu ujao wa kilimo. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa niombe radhi uliniita lakini sikuwa nimeuliza swali. Naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, kuna baadhi ya viwanda vinazalisha mbolea hapa nchini kikiwemo kiwanda cha *Intracom* pale Nara, kiwanda cha Minjingu na viwanda vinginevyo. Je, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba viwanda hivi na vinginevyo

vinazalisha mbolea ya kutosha ili kuweza kukabiliana na upungufu wa mbolea nchini?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuleta wawekezaji wengi nchini ili waweze kuzalisha mbolea ya kutosha kwa ajili ya kusaidia usambazaji wa mbolea kwa wakulima wote nchini, ndiyo maana ukiangalia moja ya mwekezaji wetu ni hawa *Intracom* kutoka Burundi ambao wao watazilisha karibu tani 60,000 na moja ya mkakati mwingine wa Serikali ni kuhakikisha Minjingu inaongeza uzalishaji kutoka tani 30,000 mpaka tani 100,000 kwa mwaka. Lengo ni kuahakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea zote kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu huo ni mkakati wa Serikali na Serikali iko kazini kuhakikisha tunaongeza wawekezaji vilevile tunaongeza wigo wa viwanda vilivyopo kuongeza uzalishaji nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali kwa Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka, sasa aulize swali lake.

Na. 223

**Malipo kwa waathirika wa Benki ya *FBME* iliyofilisiwa**

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fedha zao waathirika wa Benki ya *FBME* iliyofilisiwa tangu Mei, 2017?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande, majibu

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2023, Serikali kupitia Bodi ya Bima ya Amana - *DIB* imelipa jumla ya shilingi bilioni 2.43 kama malipo ya awali ya fidia ya Bima ya Amana kwa wateja 3,446 waliojitokeza wa Benki ya *FBME* iliyofilisiwa mnamo mwezi Mei, 2017. Malipo ya fedha za ufilisi *(liquidation proceeds)* kwa wateja wenye amana zaidi ya shilingi 1,500,000 yanayotokana na uuzaji wa mali, makusanyo ya madeni na fedha nyingine za Benki ya *FBME* yatafanyika baada ya Mahakama ya Cyprus kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa na Benki Kuu ya Cyprus la kuitambua *DIB* kama Mfilisi wa benki yote ikijumuisha Makao Makuu pamoja na tawi la Cyprus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uamuzi wa Mahakama unatarajiwa kutolewa ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji, swali la nyongeza.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mbali na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa benki hii haikufilisika bali ilifilisiwa na inasemekana walikuwa na fedha za kulipa waathirika wa benki hii. Je, Serikali inajua maumivu wanayoyapata waathirika wa benki hii?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali ndiyo dhamana wa mabenki yote Tanzania na Watanzania wengi wameathirika na benki hii. Je, haioni haja hivi sasa Serikali ikachukua jukumu la kuwalipa Watanzania wlioathirika katika benki hii na wao wakasubiri jibu la Mahakama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Haji Mlenge kwa namna anavyofuatilia kwa karibu sana suala hili la benki ya *FBME*. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inajua kadhia hii na ndiyo maana Serikali inafuatilia kwa karibu sana siku hadi siku, mpaka kutoa wataalam wetu hapa kwenda kusimamia kesi hiyo kule Cyprus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, naomba Mheshimiwa Mlenge uwe na subira mara tu maamuzi ya Mahakama yatakapotolewa na taratibu kukamilika nakuhakikishia kwamba Serikali itawalipa wateja hao bila pingamizi yoyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 224

**Madereva na kondakta wa jinsia zote kwenye mabasi ya watoto wa shule**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isiagize kuwe na madereva na kondakta wa jinsia zote kwenye mabasi ya shule ili kudhibiti vitendo vya ubakaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Waraka wa Elimu Na. 1 wa Mwaka 2023 imetoa maelekezo kwa wamiliki wote wa shule zinazotoa huduma ya usafiri kwa wanafunzi kuhakikisha kuwa wanakuwa na mhudumu wa kike na wa kiume katika kila basi au gari linalosafirisha wanafunzi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waraka huo, Wizara ilikutana na wadau wa elimu kujadiliana namna bora ya kutekeleza Waraka tajwa na tulikubaliana kwamba *deadline* ya kutekelezwa imefutwa. Hivyo, wadau wote wanatakiwa

kujitahidi kutekeleza Waraka huo na kabla ya kupanga *deadline* nyingine tutapanga kikao na wadau wote kujadiliana namna ya utekelezaji. Kwa sasa tunahimiza kwamba, mabasi yote ya wanafunzi yawe na watumishi au wahudumu wa jinsia zote. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Najma, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niwapongeze Serikali kwa kuchukua mikakati hii maalum kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali langu la kwanza, Je, ni hatua gani watachukuliwa ambao hawatatekeleza agizo hilo ama maelekezo hayo ya Serikali?

Swali langu la pili, kutokana na hali ilivyo sasa hivi hapa nchini kwetu na harakati ambazo wazazi na walezi tunazo, kuna umuhimu wa wale wasaidizi wetu ambao wanaishi na watoto wetu majumbani, kuwa na elimu ya ulezi wa Watoto. Mambo haya tayari yanafanyika duniani, ukienda Bara la Amerika yapo, ukienda Bara la Asia yapo, ukienda Bara la Ulaya pia yapo pia na Bara la Afrika kwa mfano, nchi za ya South Africa tayari wana *training* za *child care* kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu waweze kupata malezi bora.

Je, ni lini Serikali itaanzisha vitengo hivi maalum, hata kama ikiwa ni *VETA* kuwafundisha wale Dada zetu wanaotoka maeneo mbalimbali ya Tanzania wanaokuja kufanya kazi majumbani ili waweze kupata hiyo *training* kwa ajili ya kuwalea watoto wetu kwa malezi yanayostahiki?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Najma Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza anataka kufahamu mkakati na hatua za Serikali itakazochukua kwa wale ambao watapinga utekelezaji wa waraka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, Serikali inaendesha taratibu zake kwa mujibu wa kanuni, sheria, taratibu na miongozo, kwa yule atakayekaidi au kupinga au kwa namna yoyote ile akakataa kutekeleza, basi sheria, kanuni na taratibu ndizo ambazo tutakazotumia kuhakikisha kwamba waraka huu unatekelezwa ili mambo yote yakae sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, anataka kufahamu mkakati wa Serikali juu ya namna gani tunafanya kwa wale wahudumu wa majumbani. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu Wizara ya Elimu kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - *VETA* tumeanzisha kozi mbalimbali, sasa hivi tumeanza na hizi kozi za *housekeeping* ambazo zinafundisha hawa wahudumu wa majumbani au *house girl* na ma-*house bo*y.

Naomba tuchukue ushauri huu wa Mheshimiwa Mbunge ni ushauri mzuri tuende tukaufanyie kazi tuweze kuangalia namna bora ya kuweza vilevile kuingiza kozi hii *ya child care training* kwa wale wahudumu wa majumbani. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 225

**Mradi wa Maji – Bukoba Manispaa**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata za Maruku, Karabagaine, Nyakato, Kunazi, Katoma, Kemondo na Bujugo Jirani na Bukoba Manispaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji Kata ya Katoma na wananchi wanapata huduma ya maji. Vilevile, utekelezaji wa miradi ya maji unaendelea kwenye Kata za karabagaine na Nyakato ambapo miradi imekamilika katika vijiji vya Itahwa, Kabale na Burugo. Maeneo ya Kemondo na Kunazi utekelezaji wa mradi unaendelea na umefikia asilimia 88. Kwa Kata za Maruku na Bujugo, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kumuajiri Mkandarasi na ujenzi utaanza mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi kwenye vijiji vilivyobaki katika Kata za Karabagaine na Nyakato.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, napenda kujua sasa kwa miradi ambayo inaendelea itakamilikalini?

Swali langu la pili, Bukoba Manispaa mradi wake una chanzo cha uhakika ambacho ni Ziwa Victoria. Je, Serikali haioni kwamba kwa kushirikiana na *BUWASA* wanaweza kutazama uwezekano wa kutumia mradi huu ambao una maji mengi, ambao unaweza kupeleka maji katika Kata za Bujugo na Maruku? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo imeanza kama ambavyo tumeainisha hapa, mingine ipo asilimia 88 maana yake iko katika hatua za mwisho za utekelezaji wake, kwa hiyo kikubwa tu nimhakikishie kwa niaba ya Waziri wa Maji kwamba Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu ili miradi yote itekelezeka kama ambavyo tumesainiana katika mikataba kati ya Wizara na Mkandarasi

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chanzo cha uhakika cha Ziwa Victoria na maoni ambayo umeyatoa Wizara imeyapokea na itayafanyia kazi ili kuhakikisha tutumie hicho chanzo kuwaletea huduma wananchi wa Bukoba Manispaa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu asubuhi hii. Ninayo matangazo machache hapa.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii kwanza kabisa ni wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Naysan Sahba ambaye ni *UNICEF Global Director of Communication and Advocacy*. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Shalini Buhuguna ambaye ni *UNICEF Representative in Tanzania*; tunaye Ndugu Angela Travis ambaye ni *UNICEF Regional Communication Adviser for Eastern and Southern Africa*; tunaye Ndugu Manisha Mishra ambaye ni *UNICEF Tanzania Chief of Communication, Advocacy and Partnership*; tunaye Ndugu Usia Nkhoma Ledama ambaye *Communication Specialist and Focal Person for* Bunge *and UNICEF partnership in Tanzania* na tunaye Ndugu John George ambaye ni *Liaison Officer UNICEF office in* Dodoma; ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Mbunge Mstaafu Ndugu Idd Azzan, Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Usalama Barabarani, karibu sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Dkt. Bonaventure Baya, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni 12 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambao ni Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati ya Usalama Barabarani kutoka Tanzania Bara. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 13 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambao ni Viongozi na Wafugaji kutoka Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhan ambaye ni mpiga kura wake kutoka Singida Kaskazini, Ndugu Frank Akonaay. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ambaye ni Mwalimu James Tarimo kutoka Muleba Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambao ni wajasiliamali kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Wapo pia wageni sita wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed ambao ni Viongozi wa UVCCM kutoka Jimbo la Shaurimoyo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wapiga kura wake kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo, ambaye ni Diwani wa Kata ya Buhare, Musoma Mkoa wa Mara, Mheshimiwa Jumbura Lugola. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Suma Fyandomo ambao ni familia yake kutoka Mbeya Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini cha Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

Katibu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 76 na Kanuni ya 53. Wakati nilipouliza swali la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwa namna ambayo tafsiri yake inakuja kwamba, Mbunge anaweza akawa hajatoa taarifa sahihi katika Bunge lako, akisema kwamba jambo hilo siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza kwamba, kwa kuwa mawakala walioko kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi wamekataa kutoa mbolea kwa madai kwamba Serikali haikuwalipa, lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba hilo jambo siyo kweli. Sasa angetoa ufafanuzi zaidi kwamba je taarifa niliyoitoa ndiyo siyo kweli, au siyo kweli kwamba hawakuwalipa mawakala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri hiyo katika Bunge lako inaweza ikaenda nje kwamba Mbunge kasema uongo kwenye Bunge lako. Naomba ufafanuzi, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Noah Lemburis kwa Kanuni yetu ya 76 akiomba Mwongozo wa Kiti kama jambo lililotokea mapema Bungeni linaruhusiwa ama haliruhusiwi, na lilihusu swali ambalo aliuliza, na majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri.

Mwongozo wangu ni kwamba nitapitia Kumbukumbu Rasmi zile za Bunge tuone alivyojibu, baadaye nitatoa Mwongozo. Ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja iliyoko mbele yetu, Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na ninayo majina ya wachangiaji hapa. Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa hii fursa ya kuchangia. Kipekee sana, niungane na Waheshimiwa

Wabunge wote waliompongeza sana Mheshimiwa Waziri Ulega kwa hotuba yake ambayo imejaa mikakati mingi na mizuri ambayo imekusudia kuikomboa Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi. Vile vile namshukuru na kumpongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde na Katibu Mkuu, Mheshimiwa Profesa Shemdoe kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wanautoa kwa wadau wa sekta hii na kwa maandalizi ya taarifa makini na yenye mikakati mizuri na mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, moja katika mipango au mikakati iliyopo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kuzalisha au kutengeneza ajira milioni nane, kuanzia mwanzo wa Bunge hili mpaka mwisho wa Bunge hili. Mwanzo wa uhai wa Bunge hili mpaka mwisho wa uhai wa Bunge hili, tunatakiwa tuwe tumeisaidia Serikali kutengeneza ajira milioni nane kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo sekta mama mbili ambazo zinaweza kutengeneza ajira hizo milioni nane au zaidi iwapo Serikali itatusikiliza Wabunge, na iwapo Serikali itapeleka kipaumbele kwa mujibu wa ushauri wa Wabunge. Wabunge humu ndani wameeleza mara nyingi, moja katika sekta muhimu ambazo zitapunguza mlundikano wa watu waliokosa ajira, sekta ambazo zitatuwezesha kupata ajira milioni nane, ni Sekta ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mikakati kwenye kilimo, mikakati mizuri ambayo inawapeleka vijana kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo. Kwa upande wa Mheshimiwa Ulega tumeona mikakati yake ya kutupeleka na kuwapeleka vijana wa Kitanzania wakawekeze kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Umewasikiliza Waheshimiwa Wabunge humu, wameeleza mahitaji ya nyama na mazao mengine ya mifugo ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Wabunge ambao wametembelea nchi mbalimbali zikiwemo Ulaya, nchi za Magharibi, waliotembelea nchi za Uarabuni, kote huko wamekiri ndani ya Bunge lako Tukufu Sekta ya Nyama ingeweza kulikomboa Taifa hili. Mahitaji ya nyama nchi za Uarabuni ni kubwa kuliko ambavyo sisi tunaweza kupelea. Nchi yetu imekaa kijiografia, imekaa eneo la kimkakati sana. Kusafirisha ng'ombe walio hai au nyama zenye sifa kupeleka nchi za Uarabuni, kupeleka Comoro ni rahisi kuliko nchi yoyote Afrika ambayo ingeweza kufanya jukumu hilo. Leo tuna maelfu ya Watanzania hawana ajira kwa sababu hatujaamua kuwekeza kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi nyingi ambazo zimejenga uchumi wao kwa kutumia Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Nenda Marekani mkaangalie ni asilimia ngapi ya uwekezaji unapelekwa kwenye ufugaji? Leo sisi tulishwe na nchi za Amerika ya Kusini nyama. Fikiria kusafirisha nyama toka Brazil kupeleka Uarabuni na kusafirisha nyama kutoka Tanzania kupeleka Uarabuni, nani anatengeneza faida kubwa zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe, na niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuongeze nguvu kwenye hii sekta. Nasikitika simwoni Waziri wa Fedha hapa. Waziri wa Fedha apeleke fedha Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tuahirishe mambo mengine ambayo hayana tija, tupeleke fedha kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nimeitazama mikakati ya Mheshimiwa Waziri hapa, moja katika mikakati mahususi ni uzalishaji wa malisho na ambari kwa maana ya mbegu bora za mifugo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangia hoja na Bunge lako kwamba kuna kikao cha Baraza la Mawaziri kinachoendelea sasa, ndiyo maana Mawaziri *almost* karibu wote hawaonekani Bungeni hapa, lakini pia yupo Naibu Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, anaposema jambo Wizara ya Fedha, maana yake Naibu Waziri yupo, atalichukua na tutakwenda kulifanyia kazi kama Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mhagama, unaipokea taarifa?

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninaipokea taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na ninatambua kwamba Serikali ipo humu ndani na inasikia na ninaomba inisikilize kwamba hakuna mapinduzi ya uchumi tutayapata Tanzania kama hatupeleki fedha kwenye mifugo na uvuvi. Mikakati ya Mheshimiwa Waziri ni bayana, ipo *very clear*, kwamba anahitaji kufanya *transformation* kwenye Sekta ya Mifugo. Kuna eneo la malisho, kuna eneo la mbegu bora. Ukiangalia takwimu alizozileta Mheshimiwa Waziri, haziendi kujibu tatizo. Mheshimiwa Waziri amependekeza kuzalisha malisho hekta 11,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hekta 11,000 ni sawa sawa na tani 55,000 za malisho kwa maana ya *hay*. Hizi unalisha ng'ombe 25,000 tu kwa mwaka. Tanzania tuna ng'ombe milioni 36,000. Unaona kwamba Waziri ana hamu ya kusonga mbele lakini sisi Serikali tunamkamata miguu. Kwenye hili nimshauri Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tunaanza, aachane na biashara ya kwenda kuzalisha *hay* yeye mwenyewe, isipokuwa fedha hii akaiwekeze kwenye kuzalisha mbegu za malisho. Akazalishe mbegu za malisho hekta 11,000 tupate mbegu za kutosha. Hizi mbegu tuwawezeshe sekta binafsi kuzalisha malisho wao wenyewe. Kwa sababu hizo hekta 11,000 utaenda kutatua tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu, tuanzie hapo. Peleka hii fedha ambayo utapata kwenye hekta 11,000, peleka kwenye mbegu za malisho. Tumefanya kwenye mahindi, tumefanya kwenye maharage, tumefanya kwenye mazao ya kilimo; tumewekeza kwenye uzalishaji wa mbegu, Serikali ihakikishe tunapata mbegu, lakini sekta binafsi ndiyo izalishe, ifanye *multiplication* ya hizo mbegu. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri, hii fedha atakayoipata aipeleke kwenye kuzalisha mbegu. Tuna mahitaji makubwa sana ya mbegu ya *brachiaria,* haipo nchini, lakini katika mbegu nzuri sana, *hay* nzuri sana utaipata kwenye *brachiaria*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida ya *setaria*, nimeenda mpaka hapo Iringa, hakuna. Kwa miaka mitatu unasubiri kupata kilo 200 za mbegu. *Imagine,* nchi hii tupo nyuma sana. Miaka mitatu, minne bado unasubiri upate *supply* ya mbegu toka kwenye mashamba ya Serikali. Hatuwezi kufanya mapinduzi ya mifugo kama hatutathubutu kuwekeza vizuri kwenye uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *cenchrus* ni mbengu ambayo inafanya vizuri sana hapa Dodoma, lakini nchi hii kuna maeneo

mengi yanakuwa makame kama ilivyo Dodoma. Hakuna utafiti uliofanyika Mkoa wa Ruvuma na mikoa mingine kuhakikisha kwamba hii *cenchrus* ambayo ni *resistance* kwa mazingira, inaweza ikafanya vizuri kwa maeneo hayo. Mheshimiwa ilete ukaiwekeze huko…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhagama, muda wako umeisha, naomba umalizie.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa na mchango kwenye maeneo mengine ya miundombinu na masuala ya chanjo, lakini nitapeleka kwa Mheshimiwa Waziri kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Nitajikita zaidi kwenye mambo yanayohusu jimboni kwangu kwa sababu kuna mambo ambayo hayajakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa kutuandikia *speech* nzuri sana. Pamoja na hayo, Wananjombe bado tuna masikitiko kwa sababu sekta hii ya mifugo, kama wengi wanavyosema, tunaiona ina *potential* kubwa, lakini bado ina matatizo makubwa sana na yanaji-*reflect* katika namna bajeti ilivyogawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kwamba, ukiangalia *importation* ya maziwa kama moja ya *main product* ya sekta hii, ni kubwa mno kuliko *export*. Tuna-*export* karibu lita 280,000, hazifiki hata milioni moja, lakini tuna-*import* lita milioni 11.6 kwa gharama ya Shilingi bilioni 22. Ni wazi kwamba hapa kuna tatizo, aidha tija ni ndogo au hakuna uwekezaji. Kwa kesi yetu hapa, ni wazi kwamba vyote viwili vina-*apply;* kwamba hakuna tija kwenye uzalishaji, na hakuna uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji aliyepita amejaribu kuliongea vizuri sana, nami nisingependa kurudia yale aliyoyasema, lakini niseme wazi, iko haja ya Serikali kuongeza uwekezaji katika sekta hii na katika Wizara hii ya Mifugo. Twende mbali zaidi, tuangalie kwamba mwekezaji mkubwa ni Serikali kwa kutengeneza mazingira, lakini tuangalie kwamba mwekezaji anayeweza akawa *game changer* ni *private sector* kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimefarijika kuona Waziri anaongelea kwamba wanakwenda kupitia taratibu, kanuni na sheria za sekta hii. Nina matumaini kwamba zinapitiwa kwa nia ya kuondoa maeneo ambayo yana-*frustrate* hii sekta. Wizara inatakiwa i-*facilitate,* siyo i-*frustrate* hii sekta. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba hilo litafanyika na likifanyika nina uhakika sekta inaweza ikatoa mchango mkubwa na tukaacha kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mambo ambayo yananitatiza. Jimbo la Njombe Mjini ni Jimbo la wakulima na wafugaji. Tumeanza kufuga kule Njombe toka miaka ya 1930 na ufugaji umekua na kumekuwa na taasisi nyingi zimesaidia ufugaji. Miaka ya karibuni kumekuwa na mdororo mkubwa sana wa eneo la ufugaji. Mwaka 2018 tulikuwa na kaya 2,190, karibu kaya 3,000; kila kaya ilikuwa na angalau ng'ombe watatu; mwaka 2022 tumeporomoka mpaka kaya 1,000. Kaya moja ina ng'ombe mmoja mpaka mmoja na nusu au wawili. Sababu kubwa kwa wakati wa miaka hii ya karibuni ni kutokana na kutokuwa na kiwanda au soko la uhakika la maziwa kwa mkoa wetu, wilaya yetu na Halmashauri yetu ya Njombe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Njombe tuna kiwanda cha maziwa. Kiwanda kile ni moja ya viwanda ambavyo ni *model* nzuri sana, kwa maana ya kwamba kinamilikiwa na wafugaji, Halmashauri zetu na taasisi binafsi kama makanisa. Kiwanda hiki kimeingia katika mgogoro wa deni. Tunawashukuru *TADB* kwa kutaka kukikwamua kiwanda hiki na kuleta deni kubwa la karibu shilingi bilioni 1.2. Deni hilo lingeisha mwaka 2025, lakini kutokana na *trend* mbaya *TADB* waliamua kwamba ingekuwa ni vizuri pengine kufanyike *re-organization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, napenda kusema, *TADB* hawajaweza kutusaidia sana kwenye ku-*reorganize* na ku-*restructure* kiwanda hiki. Napenda kusema, kumekuwa na jitihada nyingi za makusudi za kukikomboa kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki bado kina *potential,* ukiandika *business plan* inaonyesha kabisa kiwanda hiki kinaweza kikalipa deni la *TADB* bila matatizo yoyote. Kiwanda hiki kina *asset value* ya *2.6 billion* lakini deni la *TADB* ni kama *1.6 billion*. Kama kiwanda hiki *TADB* watachukua

*approach* ya kusaidia kama ambavyo nia ya *TADB* ni kusaidia na ku-*promote* wakulima na wafugaji, nina uhakika tunaweza tukafikia mahali pazuri kwa sababu wazalishaji, wazaaji wakubwa wa *products* za kiwanda hiki ni mahoteli ambayo mengi yako Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki kwa *cheese* pekeyake kinaweza kikazalisha kwa mwaka karibu shilingi bilioni tatu. Kwa hiyo, naona kina *potential* kubwa. Hakuna sababu kwa nini tusiweke *focus* kwenye hiki kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha wenzetu wa *TADB* badala ya kuliangalia jambo hili kwa upana na kwa kuangalia nia kubwa ya Serikali ya kuchakata mazao ya kilimo na biashara hapa hapa nchini wameamua kuweka dalali auze hiki kiwanda. Sasa hatuna tatizo na *TADB* kutafuta njia za ku-*recover* lakini tatizo ni njia gani wanazitumia za ku-*recover?* Njia wanazotumia za kuweka dalali zinaenda kinyume kabisa na matakwa na dhima nzima ya kwa nini *TADB* iliundwa ili isaidie wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na kiwanda ambacho kina matatizo unachotakiwa kufanya ni ku-*reorganize* na ku-*restructure*. Ukiweka dalali kazi yake ni moja tu. Yeye anafanya kitu kinaitwa *asset stripping*, anaua. Kwa hiyo, nipende kuiomba sana Serikali kwa kweli ifanye utaratibu na nimelisema hili hapa Bungeni siyo mara moja. Nimeongea na Waziri aliyepita, nimeongea na Waziri aliyepo lakini vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu naye nimeongea naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Waziri na ninashukuru Waziri ametoa *commitment* kwamba atakwenda kulishughulikia. Naomba jambo hili lishughulikiwe mwanzo mpaka mwisho lifikie mwisho ieleweke kwamba tunawakomboa

wakulima ambao wao wenyewe wamejikomboa kwa kuanzisha kiwanda wakishirikiana na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *modal* ni *modal* nzuri, tuiendeleze badala ya kuiua kwa kutumia benki yetu ambayo kazi yake ni kuendeleza wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mambo mawili matatu ambayo nayo yamejitokeza katika bajeti hii ambayo kwa watu wa Njombe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo muda wako umeisha malizia.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; ni mawili tu. Sisi watu wa Njombe tumesahaulika kwenye uhimilishaji. Sisi tunasemekana kwamba kuna tatizo kubwa sana la udumavu na tungetegemea Serikali ingeipa *focus* Njombe kwenye masuala yote yanayosaidia maziwa kuzalishwa kwa wingi ili kutatua tatizo hilo. Kwenye majosho tuna shukuru Serikali kwa kutupa fedha ya kutosha lakini tungeomba tuongezewe angalau majosho mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwenye ufugaji wa samaki nipende kuomba sana vile vile tumesahaulika tuna ufugaji wa samaki karibu wafugaji 200 mabwawa karibu 300 lakini kwa vile tunaonekana ni Njombe mjini inadhaniwa kwamba hatuhitaji na hatufugi samaki. Tuombe na sisi tupate majosho na madarasa ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kupata nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa uteuzi wao katika nafasi hiyo nyeti sana katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Mawaziri nawaamini na hii nafasi waliyopewa ni nafasi yao kubwa sana katika *icon* ya nchi hii lakini nawapa pole pia kwa nafasi hii kwa sababu wengi wamepita sana katika Wizara hii baada ya kutokuitendea haki. Naamini safari hii Mheshimiwa Ulega kwa sababu alikuwa ni mchezaji wa akiba yaani Naibu Waziri kwa Mawaziri wawili waliopita sasa leo amepewa zigo hili yeye mwenyewe. Ninaimani atalitendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya wavuvi, matatizo ya wafugaji, Mheshimiwa Ulega anayajua lakini ni watoto wa wavuvi na mmoja yule ni mtoto wa mfugaji; Mheshimiwa Silinde. Kwa hiyo ninaamini watatenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja katika suala la hereni, suala la hereni hili limekuwa ni tatizo katika nchi hii. Wajikite sana katika kuleta sera ya namna gani tutaweza kuboresha mifugo yetu wakaacha kupambana na wafugaji kuhusiana na suala la hereni. Huu ni ulaji tu wa watu wametengeneza wajamaa wakaleta hapa wanataka kuja kusumbua nchi na hili litaleta hatari kubwa sana.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru mchangiaji anachangia vizuri lakini napenda nimpe taarifa kwamba katika nchi hii inasemekana kwenye mapori yetu kuna mifugo mingi sana ambayo siyo ya kwetu. Hereni ina nia nzuri kabisa ya kutaka kutambua mifugo tuliyonayo nchi hii kwamba ni mingapi na ni ya nani? Hakuna upigaji hapo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Tabasam taarifa unaipokea?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haina nafasi ya kukubaliwa. Huyo ni mchana mbao hawezi kujua habari ya ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamuona anaondoka na kuondoka kwa sababu ni mchana mbao. Naomba uendelee kunipa nafasi ni kwamba kama ni nchi huru ambayo tayari inalindwa na mipaka yake na Mheshimiwa Rais kishaapa kwamba atalinda wananchi, atalinda nchi na mipaka yake, hao ng'ombe wamepitia wapi? Haya ni maneno ya watu wapigaji baba. Njaa inasumbua sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuja kuharibu heshima ya nchi yetu sisi kama ng'ombe wanajulikana, wananchi wanajulikana wafugaji wa ng'ombe, Tabasam ana ng'ombe kadhaa, kule chini tuna mabalozi, tuna Wenyeviti wa Serikali za

Vijiji, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Wajumbe. Hakuna mtu ambaye hajui ng'ombe wa fulani wako kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata buchani ukienda huwezi ukakuta ng'ombe yaani katika *label* ya ng'ombe pale buchani mguu unawekwa ulionona. Hatujawahi kuona kichwa kimewekwa kina hereni kuonesha kwamba ng'ombe unayenunua nyama hii ina hereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mpango wa kuzalisha majani. Huu mpango wa kuzalisha majani Mheshimiwa Waziri usiupeleke tu kwenye mashamba yenu. Huu iwe ni Sera ya Serikali kila mfugaji awe na shamba la ekari moja au mbili na tuleteeni mbegu. Kama Serikali imeweza kwenda kupeleka ruzuku katika mbolea, haiwezi Serikali kushindwa kuleta ruzuku ya majani. Kwa sababu majani yale watu wakishaona faida yake, tayari watu wataendelea kulisha mifugo yao bila hata wasi wasi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litapunguza habari ya kusafirisha ng'ombe kuwatoa Sengerema kuwapeleka Mtwara, kuwatoa Sengerema kuwapeleka Mbeya. Sisi tutabaki na ng'ombe wetu kwa sababu tayari tumeshafundishwa namna ya kufuga kisasa. Haya masuala mbona yanawezekana? Unao wataalamu, wataalamu tunao mpaka ngazi za wilaya. Tutengenezeeni sera nzuri, wafugaji tuwe huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kutuletea habari ya muda wote tukifikiria hereni, kesho chanjo, kesho chanjo ya miguu, chanjo ya midomo na bado tena mtatuletea zigo jingine la hereni, hili haliwezi kukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu nina malambo. Mimi nina malambo ambayo yamepasuka na haya malambo

umekuja kuyaona wewe mwenyewe ukiwa Naibu Waziri na leo wewe ni Waziri. Sasa Mheshimiwa hivi tunavyozungumza hili jambo la Mheshimiwa Waziri la malambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Lambo mimi la Nyanchenche unajua lina kata tatu. Nina Lambo la Bitoto, hili Lambo la Bitoto Mheshimiwa Ngeleja lilimuondoa kwa sababu ndiyo nyumbani kwao. Sasa siwezi kukubali niondolewe na Wananchi wa Bitoto. Malambo yako tisa, haya malambo sisi kwetu ni kitu adimu, kitu cha thamani sana. Nakuomba Lambo la Nyanchenche umekwenda umeona, Lambo la Kishinda, Bitoto, Nyampande, Kasungamile, Buzirasoga, Sima. Haya malambo yote yamepasuka. Lambo liko Nyamizeze, ndugu yangu nisaidie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni kwamba miradi yenu yote ya uvuvi na mifugo hebu ileteni wilayani. Ninyi mko watumishi wachache. Nimekuja ofisini kwenu kaofisi kako hapo *NBC* wamebanana mle wataalamu hata hewa hawana bado mnang'ang'ania miradi ya nchi nzima mkae nayo mtaweza wapi? Tuleteeni hizi fedha wale wataalamu mlionao ninyi muwaweke huku lakini pia zile ofisi zako siyo nzuri sana kwenye suala mtu akija pale ofisini anashangaa kwamba humu ndiyo kuna wataalamu ambao wanasimamia Sekta ya Uvuvi? Sekta ya Mifugo kuna watu wengi sana ambao wameajiriwa katika mifugo na uvuvi. Ndiyo sekta pekee katika nchi hii ambayo ina ajira ya moja kwa moja. Hebu ilindeni hii sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe, hawa ng'ombe mnaowaona ninyi tunawafuga sisi miaka minne ndiyo anakwenda kuuzwa mnadani. Nendeni mkaangalie Argentina. Ng'ombe wa miaka minne ana tani 1.5. Sisi ng'ombe wa miaka minne ana kilo 88, kilo 110, mnafeli wapi? Mbona wataalamu mko wengi, hicho Chuo cha *SUA* kimekuwa ni chuo cha nini? Maana yake sielewi. Hebu pelekeni hao wataalamu waende

*field* waende na Argentina. Hawezi kusoma *SUA* akaja field Sengerema kwenye ng'ombe wa kilo 80 wa miaka minne. Mpeleke akaone ng'ombe wa miaka minne Argentina na Brazil kule. Hata wewe angalia uwezekano wa kusafiri sasa kwenda kule, Mama ata toa kibali nchi imefunguka hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi. Mheshimiwa Ulega suala la uvuvi angalia sana hizi taa za *solar*. Hizi taa za *solar* zinapiga mpaka chini. Ziwa letu Victoria halina urefu mkubwa, kuna mita tisa, mita 20, mita 90. Sasa hizi taa zinapiga mpaka chini kwenye mazalia ya samaki. Litabakia ziwa la maji ya kunywa. Sisi tunakula samaki hawa kuanzia furu, nembe, gogogo, ngere yaani hatuna mahali chakula kingine sisi zaidi yetu hapo. Mmeona wenzenu sasa hivi wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Anayetaka kuendesha pikipiki anapata leseni. Sasa sisi wavuvi suala la leseni.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Tabasam malizia mchango wako.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Haya malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hawa wavuvi. Mtu anakuwa ana kambi ya watu 120 hana hata mtaalamu mmoja kwenye kambi yake. Kwa nini msifanye na wenyewe mtu anayepata leseni apeleke siku saba aende Chuo cha Uvuvi Nyegezi pale anakaa siku saba anafundishwa namna ya uvuvi anakwenda kuwafundisha watu kambini. Hakuna mtu anayeendesha chombo halafu akakosa kuwa na taaluma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana naunga mkono hoja lakini nakuomba hawa watu wetu wa Wizara ya Uvuvi waangalie Ziwa Victoria sasa linabakia kuwa la maji ya kunywa, samaki wanaisha kwa ajili ya uvuvi haramu, 75% ni wavuvi haramu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasamu muda wako umeisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi katika Ziwa Victoria. Ahsante sana Mheshimiwa Ulega nakutakia kazi njema. Mungu akujalie sana na watu wako wamekuja Sengerema nimeona nategemea Soko, kwenye soko la Samaki Nyapukalo na *cold room*, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Mariam Ditopile atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hezron Mwakagenda, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili ajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii kuweza kuchangia kwenye hoja iliyoko mezani ya Bajeti ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na wenzangu wote kwa pongezi walizotoa kuanzia kwa Mheshimiwa Rais wetu pamoja na viongozi wetu kwenye Wizara. Babu yangu Tabasam ametangulia kumpa angalizo Mheshimiwa Ulega kwamba yeye ni mzoefu kwenye Wizara hii na siyo mgeni na sasa ana mamlaka iliyokamilika kwa hiyo tunategemea makubwa sana na wewe ni kijana mnyenyekevu msikivu. Kwa hiyo, natumai hata Mheshimiwa Mhagama amekwambia ukitusikiliza Wabunge basi haya mambo uliyoyapanga yatafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwenye maeneo machache; la kwanza ni takwimu. Hivi tunavyoimba kwamba tuna ng'ombe milioni 32 tuna bata 10,000. Ni mfumo gani ambao umeutumia kutupa *data* hizi? Sitaki kuongea sana kwa undani lakini ushauri wangu sijui mfumo gani maana yako hayo mambo ya hereni na nini yanapigiwa kelele. Kama nia ni njema lakini huo utaratibu kidogo una ukakasi rudi nyuma kwa sababu huwezi kukamilisha mipango yako kama huna takwimu sahihi. Huwezi kwenda huko unakotaka kwenda kama hutokuwa na takwimu sahihi, una kaya ngapi zinazojihusisha kwenye mifugo na aina ya mifugo kwenye kaya hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kweli kwenye mipango yote anza na takwimu ndiyo itakuwa ufunguo mzuri wa wewe kwenda mbele kwenye mipango yako. Mheshimiwa Waziri kwa kweli hebu pitia upya sera zako pamoja na sheria mbalimbali kwenye mifugo na uvuvi. Leo hii kelele zote tunazopiga Waheshimiwa Wabunge kumshauri huyu anatumia Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, kweli Mheshimiwa Waziri? Tuko mwaka 2023 Sera ya Mifugo tunayotumia ni ya 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unatumia Ilani ya Uchaguzi ya 2020/2025, unatumia Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2021/2026. Kweli hii sera yako ya mifugo ya 2006 itakupeleka unakotaka kwenda? Kwa hiyo, ni vyema hebu tuweze kupitia hizi sera zetu. Pia kuna sera nyingine kati ya chache ambazo nataka kutolea mfano, kuna *policy* inaitwa *disease control policy* (Sera ya kupambana na kudhibiti magonjwa yatokanayo na mifugo na mazao ya mifugo). Kama hatutoweza kuipitia hii kitu kwa kweli ndoto ya sisi kuuza bidhaa zetu kwenye soko la kimataifa tulifute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano ambao uko hai. Kuna kampuni siitaji jina ilipata soko kubwa la nyama ambayo

imechakatwa kwenye thamani mbalimbali kule Afrika Kusini pamoja na Nchi ya Msumbiji. Walikwama kwenye soko hilo kwa sababu leo hii nyama yetu hairuhusiwi kuuzwa kwenye nchi za *SADC* kwa sababu tunao ugonjwa wa *foot and mouth disease*. Siyo kwamba huo ugonjwa hamuufanyii hatua za kuudhibiti lakini *policy* yetu ya *disease control* haiko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wafanyabiashara wengi hawasemi tu, hata hao wanaotafuta soko la maziwa, soko la nyama za kuku huko nje, mayai wanakutana na hichi kitu. Maswali wanayoulizwa hawana majibu sahihi. Kwa hiyo mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri hebu hizi sera zetu twende tukazipitie, sheria zetu lete hapa zifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaongelea *blue economy* lakini *nautical miles* zinazoruhusiwa kuvua samaki haziwezi kuleta tija siyo tu kwa wavuvi wadogo, hata kwa wawekezaji wakubwa wenye viwanda vya samaki haiwezi kutuletea tija Mheshimiwa Waziri. Naomba hizi sheria kaa uzipitie na wataalamu wako, tuletee hapa Bungeni tuweze kuzirekebisha na kuzipitisha ili hicho unachopanga kwenye mafanikio yako iweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri unataka kwenda kuongeza kipato kwenye sekta hii na wako Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wanashangaa Sekta ya Uvuvi siyo ya kuchangia 1%, hiyo ni aibu. Hebu jiulize leo nchi zinazotuzunguka tunawapelekea mahindi na bidhaa za kilimo kwa nini siyo bidhaa za uvuvi ama za ufugaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwennyekiti, tuna ng'ombe wengi kuliko nchi za jirani. Leo hii Tanzania tumezungukwa na *land locked countries* ambazo hawana bahari lakini kwenye maziwa matatu tuliyokuwa nayo, Victoria, Tanganyika na Nyasa sisi ndiyo wenye *share* kubwa ya hayo maziwa kuliko nchi jirani. Kwa nini

sisi tunashindwa kutumia hii kama fursa ya kuweza kujiongezea kipato lakini kuna mambo ambayo yanakuwa kikwazo kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni biashara ya haya mazao yetu mengi yanafanyika kwenye mfumo usio rasmi. Mfano, soko la maziwa, 97% ya maziwa yetu yanauzwa kwenye mfumo usio rasmi, ni 3% tu sasa hapo utaonaje tija ya biashara ya maziwa kama haujaimarisha kwamba haya maziwa yanayozalishwa na wafugaji wetu yakauzwa kwenye mfumo ambao ni rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tabasam ametangulia kusema anasikitika Ziwa Victoria lile tunaenda kuwa nalo ambalo halina tena mantiki tena babu zangu Mwanza kule bahati nzuri zamani walikuwa na dhahabu, sasa hivi dhahabu imehamia Geita. Sasa Mwanza hii miaka kumi na kitu iliyopita tulikuwa tuna viwanda zaidi ya 10. Leo Mwanza vimebaki viwanda vitatu tu vya kuchakata samaki.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Amar.

## TAARIFA

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hatuwezi kuwa na tija kwa wafugaji wetu kupata maziwa yaliyo mengi kwa sababu tuna maafisa ugani wachache. Mfano Nyang'hwale tuna maafisa ugani wako wanne na tuna kata 15 na kuna wafugaji unamkuta ana ng'ombe 100 lakini hata lita tano za maziwa hazipati. Hatuwezi kufanikiwa kwa mtindo huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mariam taarifa unaipokea?

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea na pia niunge mkono hoja ya Waziri ya kutaka kuanzisha hizi mamlaka maalum ili zitamuongezea rasilimali watu lakini na rasilimali fedha. Kwa hiyo rai yangu kwa Serikali hii mipango ya Waziri basi wakaipokee na waweze kumpa fedha ili aweze kuikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii niwaambie hatuwezi kuona tija na thamani ya sangara kama hatutopeleka sangara kwenye Soko la Dunia. Sangara akiuzwa kwa mama ntilie hapa ndani ya nchi hana tija na Waziri unajua. Sangara ana vitu viwili; ana mnofu, ana kitu kinaitwa mabondo *(fish morse)* lakini nisikitike leo viwanda vimeenda kufa ajira zimepungua kwa sababu tu hii biashara ya mabondo inafanywa kiholela. Unapoteza mapato Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie hebu kunja moyo fanya maamuzi magumu. Hebu tuombe ndani ya miezi mitatu au miezi sita, rasimisha hii biashara, mtu hakatazwi kuuza mabondo yake lakini aende akauze kwenye sehemu ambazo zimeidhinishwa na wizara, kama viwandani na *center* zingine za kupokea kwanza utafanya udhibiti wa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hakatazwi kuuza mabondo yake lakini aende akauze kwenye sehemu ambazo zimeidhinishwa na Wizara, kama viwandani na *center* zingine za kupokea. Kwanza utafanya udhibiti wa thamani; leo hii hayo mabondo yenyewe siyo kwamba yana *grade* moja, mabondo yana *grade A, B,* na *C*. Leo hii wewe huna hiyo takwimu, mabondo unauza tu kama bondo, leo hii mimi najua…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo una mipango mikakati mizuri ya kuzalisha sato. Leo hii sangara ana bei ndogo kuliko sato. Hao sato unaowazalisha watakosa soko kwa sababu sangara yuko humu ndani, wakati sangara tukimtoa nje ataleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumalizia, ninao ujumbe kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Kondoa Mjini, wanakusifu sana Mheshimiwa Waziri unafanya kazi kubwa wana maombi mawili. Machinjio yetu kule…

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI: …** kwa kweli yamechoka na hayakidhi usalama wa ng'ombe wanaochinjwa pale pia ni wafugaji wakubwa wa kuku wa kienyeji. Faida za kuku wa kienyeji tunazijua, tunaomba utuletee wawekezaji ili…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI: …** ufugaji ule wa kuku wa kienyeji uweze kuwaletea manufaa wananchi wa Kondoa Mjini, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Mzamili, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana tumefanya sensa ya Taifa na wenzetu wa *NBS* wametoa takwimu nzuri kabisa juu ya mifugo

tuliyonanyo katika Taifa letu. Ng'ombe tunao zaidi ya milioni 35, mbuzi milioni 25.6 na wanasema kondoo tunao takribani milioni nane. Hii pee itakusaidia wewe kupanga mipango yako vizuri kama wizara na kuhakikisha tunasaidia Watanzania kuvuka kwa mahitaji ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya ng'ombe na wanyama yameliingizia Taifa hili dola takribani milioni tatu. Hii ni hela ambayo kimsingi ikiongezewa nguvu tutapata zaidi ya hiyo pesa, kuweza kusaidia uchumi wa Taifa letu. Tatizo kubwa lililopo katika Taifa hili ni mipango na utekelezaji. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi wameelezea suala hili. Huwezi kuwa na mipango ambayo unaingiza nyama na wakati huo huo una wafugaji wako, na hawa wafugaji hujawajengea uwezo wa kulisha. Wamesema hapa, ng'ombe miaka minne ana kilo 80 wakati wenzetu ana zaidi ya kilo 500. Ni lazima tufanye kazi ya kuwasaidia Watanzania waweze kutoa bidhaa bora kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa Tanzania ni nchi ya pili kati ya nchi zenye mifugo mingi. Kwa nini sisi tusizalishe zaidi ya wenzetu ambao wanafanya vizuri, kama vile Botswana na nchi zingine? Mimi ninafikiri Waziri wa Fedha anahusika zaidi kutoa fedha kwenye Wizara hii. Nilikuwa nikiongea na Naibu Waziri anasema tukipata fedha tuna uwezo wa kufanya maajabu katika wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakaa hapa kama Bunge tukipanga mipango mingi lakini kutoa fedha hatuwezi kuwasaidia. Wataalam tunawalaumu, kwamba wapo, wamesoma na wapo ofisini wanalipwa mishahara, lakini usipowapa fedha hawawezi kufanya yale ambayo tumewapa, mwisho wa siku bajeti inakuwa ndogo. Tunakubaliana hapa kama Wabunge mwisho wa mwaka wanafanya fedha asilimia mbili, asilimia tatu; hatujafahamu ni nini mnakifikiria ilhali mnajua

kabisa wizara hii ina wakulima na wafugaji wengi. Hao ndio wanaoweza kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukosefu wa miundombinu, lakini pia miundombinu si salama na si rafiki kwa ajili ya wafugaji. Tunazungumzia maziwa kwa mfano, jana tumepata maziwa hapa kama Wabunge, lakini bado mfugaji amekuwa mtumwa wa ng'ombe au wa mifugo yake. Kwa mfano kule kwetu Rungwe lita moja ya maziwa ni shilingi 600; leo hii maji yana thamani kubwa kuliko maziwa. Mfugaji analala na ng'ombe anaamkia ng'ombe, akifiwa anamuwaza ng'ombe kwanza kuliko ndugu yake aliyefariki lakini mwisho wa siku lita moja shilingi 600; hatuwatendei haki wakulima. Tunaomba bei ya maziwa iongezeke. Maziwa ni chakula, huwezi kuuza maziwa lita moja kwa 600, maji madogo ya chupa nusu lita shilingi 1,000, hii si sawa kabisa. Inabidi kujipanga viongozo ili tuhakikishe tunawatetea wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa masoko, tulikuwa na kombe la dunia, tulipatapata kidogo masoko ya nyama, lakini mwisho wa siku, wamesema Waheshimiwa Wabunge waliopita; thamani ya nyama yetu miundombinu inayotengenezewa inafanya sisi tusipate soko la dunia kwa vizuri zaidi. Amesema hapa Mheshimiwa Mhagama, kwamba anayetoa nyama kutoka Afrika kuipeleka Dubai ni karibu zaidi kuliko anayetoka Brazil kuileta pale Dubai. Inabidi tukae chini na tujitafakari ili tuone nanma gani tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mlipuko wa magonjwa wananchi wenyewe wanaamua kujitetea. Magonjwa ya mifugo yanapokuja wao wenyewe wanaamua kuona namna gani wanadhibiti. Tunaomba Serikali isimamie. Maafisa Ugani ni wachache mwisho wa siku wananchi wenyewe wanaamua kujisimamia badala ya ninyi kufanya kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji mdogo, nimesema kuna viwanda vya uwekezaji, tuna machinjio ambayo kiukweli mengi; unajua nchi za kiarabu ndio wananunua zaidi nyama. Kwa hiyo ni lazima tuwahakikishie wenzetu waarabu ambao wao wanapenda nyama halali, kwa hiyo tuwahakikishie kwamba nyama yetu ni salama ili wawe huru kuja kununua nyama kutoka kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna nguvu zaidi inabidi kuongezeka. Tuna tani zaidi ya laki saba za nyama ambazo zinavunwa, lakini kwa jinsi tulivyo tunahitaji kupata nyama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafugaji na ufugaji wa kuhamahama. Ninajua wenzangu ambao wanatoka maeneo ya wafugaji watalalamika, lakini tufike mwisho, tupande majani kwa ajili ya wanyama wetu waweze kula katika maeneo yetu kuhamahama kupungue ili tuweze kupata nyama iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia suala herein, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu jana ametolea maagizo kwa Mheshimiwa Waziri; tunaomba alifanyie kazi haraka, kwa sababu tunatoa matamko; leo anapigwa chapa kesho mnasema herein, lakini mwisho wa siku utekelezaji unachelewa. Ninaomba sana uyasimamie aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu jana ili yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo tunaomba Waziri wa Fedha pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ongezeni fedha kwenye wizara hii, ili Watanzania waweze kunufaika na Wizara yao. Baada ya kusema hayo nasema ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu idadi ya wachangiaji ni kubwa sana kwa hiyo tutachangia kwa dakika nane.

Nimemtaja Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo atafatiwa na Mheshimiwa Daktari Thea Ntara, Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda ajiandae.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja, nisije nikasahau maana ya Wizara hii kidogo ni mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi nashindwa nianzie wapi. Changamoto ya ajira ni kubwa sana, na wote tunashuhudia kila Mbunge sasa hivi ana kimemo cha kuombwa ajira na wananchi wake, lakini sasa matarajio yetu kuna baadhi ya Wizara ambazo zingeenda kutatua changamoto hii ya soko la ajira, ikiwemo Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Michezo pamoja na Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nasikitika sana sijui kama Wizara hii itaweza kutatua changamoto hii ya soko la ajira. Kwa sababu nikisoma hizi Taarifa za Waziri na Kamati, Wizara hii hata makusanyo yao tu yenyewe hawawezi kukusanya ambayo wenyewe wamekadiria ili wakusanye, hawawezi kukusanya na hawafiki lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka 2022/2023 Wizara hii ililenga kukusanya bilioni 80.1 ambayo mifugo ikusanye bilioni 40.1 na uvuvi bilioni 40 lakini mpaka wanafikia mwezi Februari *quarter* tatu zimepita Wizara ya Mifugo imekusanya bilioni 16.6 na Wizara ya Uvuvi bilioni 13.3 kati ya bilioni 40 sawa na asilimia 33. Tumebakiza robo moja ya mwaka; na kwa makusanyo yote jumla wamekusanya kwa asilimia 37.5.

Kwa muundo huu hawawezi kufikia lengo; na sijui kwa nini hawafikii lengo na makadirio haya wameweka wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko Kamati ya TAMISEMI, kule kuna halmashauri zinakusanya makusanyo yake zinavuka lengo, zinakwenda asilimia 104, 110, yaani wanakusanya mpaka wanavuka lengo. Hata wale ambao hawavuki lengo basi angalau wanakuwa juu ya asilimia 50, lakini kwa Wizara hii sidhani kama watafika hata asilimia 50 mpaka kufika mwezi wa saba; kwa hiyo napata wasiwasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini makadirio ya bajeti ya kipindi kinachokuja cha mwaka 2023/2024 wameongeza tena bilioni mbili wakisema wataongeza makusanyo. Sasa napata wasiwasi; kama huu mwaka uliopita hata sidhani kama watafika nusu ya makusanyo lakini mwaka huu unaokuja wanasema wataongeza kidogo watakusanya bilioni 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ulega lazima waje na mikakati Madhubuti ya kuhakikisha wanaongeza makusanyo, vingenevyo hata mama mwenyewe hataona haja ya kuongeza bajeti kwenye hii Wizara. Kwa sababu hata kile ambacho wanakikadiria, yaani wao wenyewe hawajiwezi, kwa hiyo hataona sababu ya kuwawekeza sehemu ya watu ambao hawajiwezi, anaona akiweka huko fedha itaendelea kupotea. Fedha itakwenda, miradi itatekelezwa lakini hawatakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ulega yeye ndiyo umeingia juzi, wao ni wachapakazi, Mheshimiwa Silinde tumefanya wote kazi akiwa TAMISEMI, lakini Mheshimiwa Ulega mtani wangu yeye mwenyewe anajua; tangu mimi nimeingia Bunge hili kati ya Wizara ambazo nazifatilia kwa karibu sana ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wewe mwenyewe ni shahidi. Kwa hiyo nimuombe, sina wasiwasi na uchapakazi wake, aenende akaweke mikakati pamoja na watendaji wake wa kuhakikisha

anaongea makusanyo. Atatupa nguvu sana hata sisi Waheshimwa Wabunge wampiganie ili waendelee kuongezewa bajeti ya Wizara yao. Lakini sasa kama hawawezi kukusanya tutashindwa kupiga kelele wao waongezewe bajeti, kwa sababu hata kile kiasi wanachopewa kitakwenda kupotea. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aje atueleze mikakati yake hasa ya kuhakikisha anakwenda kufikia lengo la makusanyo kwanza malengo ambayo wao wameyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya miradi hii ya maendeleo walipewa bilioni 182 ya miradi ya maendeleo, lakini sasa hizi fedha za maendeleo zinatengwa, ambazo kwa mifugo walipewa bilioni 46.7 na uvuvi bilioni 135; lakini hizi fedha hazipelekwi, yaani ni hela walizotengewa lakini hazipelekwi, kwa hiyo hawawezi kufanya kazi. Kwa mfano kwenye uvuvi kati ya bilioni 135.6 imepelekwa bilioni sita pekee kwa ajili ya miradi ya maendeleo, wakati sisi TAMISEMI mradi mmoja tu wa soko la Nyamagana ni bilioni 20. Kwa hiyo sasa unaweza ukaona hapo, Wizara nzima ni mradi mmoja wa soko kwenye halmashauri moja, ndio wanapewa kama fedha za maendeleo kwa Wizara nzima ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Ulega hawawezi kutoboa, mradi mmoja wa maendeleo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mzamili, muda wako umeisha, malizia.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha ahsante sana nashukuru. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri; Wizara hii ina migogoro mingi, na kati ya vitu vinavyosababisha migogoro pia ni malisho. Jana nilimsikia alikuja na mkakati wa malisho akasema atazalisha malisho ya

kwenda kuuza mpaka nchi za Asia. Nishauri aachane na hii habari ya kuuza nchi za Asia kwanza …

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO: …** tutosheleze malisho ya hapa Tanzania kila mwaka ng'ombe wanakufa na wewe mwenyewe ni shahidi hauwezi kuuza Asia ilhali sisi wenyewe bado hatujajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daktari Thea Medard Ntara atafatiwa na Kilumbe Shaban Ng'enda, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru, nitakwenda kwa haraka sana. Naomba Mheshimiwa Waziri awe makini wachukue hizi point, najua watazidadavua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Wizara kwa mipango yenye kuleta tija, tunatumaini italeta tija. Lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri, jana nilikuwepo pale jioni wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa yale maagizo. Yale maagizo maana yake ni kwamba, bado tunahitaji utambuzi na ufatiliaji wa mifugo, hapa hatuwezi kukwepa; na alitoa yale maagizo ili ukayafanyie kazi ubaki kwenye hicho kiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ufugaji katika nchi yetu ni kama adhabu. Ni kama adhabu kwa sababu kuna mambo bado tunahitaji tulete mabadiliko ndani ya sekta hii ya mifugo. Nchi imesema ina ng'ombe milioni 36 lakini bado wafugaji wale hawana *access* kwenye elimu ya mifugo, hawana *access*

kwenye afya za mifugo yao, hawana *access* kwenye kujua malisho, hawana *access* hata ya elimu inayotolewa kwenye ufugaji wenyewe. Sasa hayo ni mambo ambayo Mheshimiwa Waziri wanatakiwa wayafanyie kazi; na wanaweza tu kuyafanyia kazi ikiwa kuna ufatiliaji, na ndani ya ufatiliaji ndipo tunapata hizo *research,* ndiyo maana ya *research*. Kwa hiyo hapo ndio utapata tafiti za kujua kwamba wafugaji wangu wana elimu, wanafaidika kweli, hawa wafugaji wangu wanajua afya za mifugo yao, magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna haya mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yanaingia katika kila sekta. Kwa hiyo mfugaji asipokuwa na elimu ya mifugo, elimu ya aina ya maradhi yanayokuja au magonjwa hatufiki huko. Kwa hiyo suala la ufatiliaji, suala la kutambua mifugo ni muhimu, hilo ninamwambia Mheshimiwa Waziri asilipindishe na alifanye kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini tukifanye sasa hivi, tukishafanya huo utambuzi maeneo muhimu ya malisho hayo wanayoyasema ya chakula yatajulikana, upatikanaji wa masoko pia utajulikana. Lakini pia tutaweza kuzuia ulaghai wa kuingiza wanyama kutoka nje ya nchi pamoja na ulaghai wa kuuza nyama isiyokuwa na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda haraka, na sasa ninakwenda kwenye hiyo Wizara yenyewe ya Mifugo. Nimuombe, nilizungumza kipindi kilichopita, katika Wizara ambazo zinaweza kusaidia, kama alivyosema Mheshimiwa Mhagama, Wizara zinazoweza kusaidia kuleta ajira hii ya kwake ni mojawapo, wasikwepe. Ile *program* ya BBT ije kwake kama *BBT2* na ile ya kilimo ya Bashe iwe *one*. Yeye alete *BBT2* atafanikiwa. Ni lazima wafungue hiyo ili wahitumu hawa wapate maeneo ya kupata ajira. Kwa hiyo atakapokuja kwenye *speech* yake ya mwisho aweke mikakati yako tuone

kama hili ameliweka, litakuongezea; na hilo ndilo linaweza kusababisha kuongezwa kwa bajeti, wakaona kwamba huyu ana mpango wa *BBT2* kwa vijana. Kwa hiyo hapo anaweza akaongezewa hata bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la uvuvi. Wenzangu wamesema, tuna Bahari na maziwa lakini pato linalotokana na huo uvuvi ni 1.7%, hiyo ni ndogo sana. Sasa mimi nataka nitoe ushauri kwenye eneo la uzalishaji wa vifaranga vya Samaki, anzeni kufatilia pale *SUA*. Kile chuo ukienda pale na mitambo yao utafurahi; sijui kama amewahi kutembelea pale, waende wakaone, wanazalisha vifaranga vya Samaki. Sasa wao wakiwasaidia, wakaungana, kwa sababu chuo ni cha Wizara ya Elimu lakini wale Samaki na mifugo iliyopo *SUA* ni vya kwake yeye. Waende wakaungane na chuo waone ni namna gani wanaweza kujaribu kutengeneza vifaranga vingi vikasambaza si Morogoro tu vikaenda mpaka mikoa mingine kwa sababu hawa walisema wanazalisha wanasambaza pale Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ile ni *project* kubwa, kwa hiyo wao wawasaidie ili iwe *project* ambayo ni kubwa zaidi, maana nasikia nchi hii kuna sehemu mbili tu wanazalisha vifaranga vya Samaki. Sasa kile chuo pia kitawasaidia kuwainua wao. Kwamba wanatumia vyuo vyetu, lakini pia hata kile chuo chenyewe kinaweza kikasaidika na kufanya mradi wake ukue zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo niseme nampongeza, lakini ili bajeti yake iongezeke achukue hii ya *BBT2* atakuja kunikumbuka siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiWa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Aida Joseph ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii muhimu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nianze kwanza, maana nisije nikasahau kuunga mkono hoja na kuwatia shime sana ndugu zangu hawa wawili Mheshimiwa Waziri ambaye ni mpya kwenye Wizara hiyo kwa maana ya kwamba ameaminiwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hiyo na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba wakati bajeti yake inasomwa hapa huko Mkoani Kigoma na hasa kwa wadau wote wa Ziwa Tanganyika, kuna taharuki kubwa sana ya suala la taarifa ya ufungaji wa Ziwa Tanganyika, kwamba Serikali za Nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika zimekaa kukubaliana kufunga Ziwa kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe 15 ya mwezi huu ili kuruhusu samaki waendelee kukua na kuweza kuvunwa wakiwa katika hali ya ukubwa na ubora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba jambo hili ni jema na niliye simama hapa kama mwakilishi wa wananchi sikusudii kulipinga, isipokuwa nakusudia kuweka maneno ambayo nafikiri Serikali ikiyachukua yatakuwa ya faida zaidi katika mpango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nataka Serikali ielewe kwamba duniani zipo Serikali za aina nyingi, kuna Serikali za Kijeshi ambapo Baraza la Kijeshi ndiyo mmiliki wa Serikali hiyo.

Zipo Serikali za Kifalme ambapo Mfalme na ukoo wake hata akifa huyu anarithi mwingine, zipo Serikali za Kisiasa kama ya kwetu ambapo Vyama vya Siasa vinakwenda kwenye uchaguzi, wananchi wanapiga kura, wanaunda Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yangu ya kusema hivyo? Uendeshaji wa Serikali hizi hauwezi kuwa sawasawa, Serikali ya Kijeshi haina sababu ya kupata ridhaa ya wananchi, itafanya mambo yake yote kwa kuzingatia mitazamo yake. Hivyo hivyo Serikali ya Kifalme, lakini Serikali ya kisiasa inafanya mambo yake kuamua na kutekeleza kwa kuzingatia maoni ya wananchi na Serikali ya Kisiasa inakuwa na wamiliki wawili mmiliki wa kwanza ni chama kilichopewa ridhaa ya kuunda Serikali na mmiliki wa pili ni wananchi waliopiga kura za kuchagua Serikali ile. Kwa hiyo mipango yetu yote lazima iwe na ridhaa ya wananchi, tusikae Wizara na Wizara, Nchi na Nchi, Serikali na Serikali tukaamua mambo kwa niaba ya wananchi na kuwapelekea wananchi tu, wafuate hayo tuliyoamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufunga Ziwa ni suala jema, lakini halina ushirikishwaji wa wananchi na kama halina ushirikishwaji wa wananchi hapo linapata ubatili. Kwa maana hiyo ningependa kusema kama mwakilishi wa wananchi kwamba hebu turudi tushirikishe wananchi. Hata hivyo, dhana ya kufunga Ziwa ni ya kufikirika haina tafiti za kutosha, Mheshimiwa Waziri anakumbuka Ziwa Tanganyika kwa takribani miaka zaidi ya ishirini halijafanyiwa *stock assessment,* ni hivi karibuni wamefanya na hawajapata majibu ya *stock assessment* ya utafiti huo. Kwa hiyo dhana ya kufunga ni ya kufikirika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuliongea kwa maongezi ya kawaida kwamba hili ziwa lifungwe lazima kuwe na mambo

ya msingi ya kutangulia. Wananchi waandaliwe wawe na ufugaji wa samaki sasa linalonisikitisha ni jambo moja wanataka kufunga Ziwa Tanganyika, lakini vizimba vya ufugaji wa samaki wamepeleka *Lake* Victoria. Ziwa Tanganyika hawakupeleka kizimba hata kimoja, lakini Ziwa Victoria wamepeleka vizimba 290 kwa taarifa nilizonazo. Hivi vizimba vingekuwa Ziwa Tanganyika na vinafanya kazi, leo tungesema fungeni maana wananchi wana *alternative* nyingine ya kupata kitoweo cha samaki, badala yake wamepeleka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nataka niliseme, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na CCM iwe makini sana, tunaweza tukaja kutengeneza tabaka kwenye nchi yetu. Leo, hii Kigoma na Mikoa mingine *resources* zinazopelekwa za nchi ni kidogo sana. Hata hivyo, kuna maeneo vitu vinapelekwa vingi, nitatoa mfano sina nia mbaya. Nia yetu ni kujirekebisha ili twende pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unapozungumza unapeleka vizimba, unapeleka mikopo mikubwa ya wavuvi *Lake* Victoria, lakini *Lake* Tanganyika hupeleki, unavutia maendeleo upande mmoja. Hata hivyo, huo upande unaovutia maendeleo, ndiyo ambao umejengwa daraja la bilioni 700 ambazo hazijawahi kuingia mkoa wowote. Huo Mkoa ambao umepeleka hivyo, ndiyo kuna meli tisa, *Lake* Tanganyika kuna meli tatu na kati ya meli tatu na kati ya hizo hakuna meli hata moja ambayo inafanya kazi. Huo mkoa unaopeleka hivyo vizimba ndiyo mkoa ambao reli ya *SGR* inajengwa imepelekwa huko kabla ya huku ambako kuna *resources* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niseme kama tunataka kujenga umoja wa Taifa, ni lazima tuhakikishe hizi rasilimali za nchi tunagawana haka kakeki ka Taifa. Sasa huko kwenye maendeleo ndiyo wanakopeleka maendeleo zaidi, kule ambako kumelala wanaacha, watatengeneza utabaka

siku moja tutakulana nyama wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo ninachokusudia kusema kwenye Bunge hili, Mheshimiwa Waziri… *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpa taarifa kaka yangu, Katibu wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam Mstaafu kwamba Daraja la Busisi ambalo limejengwa Mkoani Mwanza halitumiwi na watu wa Mwanza peke yake. Kwa siku kuna magari tisa yanakwenda Kigoma kutokea Mwanza yanapita kwenye daraja lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, pokea taarifa na muda umekwisha, malizia.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisaidie kunilindia muda. Hii taarifa siipokei kwa sababu imeendana tofauti na mchango wangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naomba umalizie mchango wako muda wako umeisha, malizia muda wako.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka niliseme kwa ujumla kwamba, sisi na wananchi wetu wa Ziwa Tanganyika tunataka Serikali ifanye jambo hili kwa utulivu, hatulikatai maana tulifunga misitu ili miti iweze kukua na kufunga Ziwa tunakubaliana lakini tushirikishane vizuri zaidi katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Ng'enda, ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida na Mheshimiwa Nashon ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ulega kwa kuchaguliwa kuwa Waziri wa hii Wizara. Nina matumaini kwamba Mheshimiwa Ulega atakuwa msikivu kwa sababu kama ni mwanafunzi amesoma kama miaka minane hiyo elimu ya Uwaziri, sasa sitegemei kama atatuangusha. Mwanafunzi mzuri ni yule anayesikiliza walimu wake na baadaye anafaulu, tunamwombea sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kusema sisi tunatoa tu ushauri kwa Serikali, wanaweza wakakubali au wakakataa, lakini mkikataa mbeleni tutakuja kuulizana maswali. Mwaka 2017/2018 ndugu yangu Mpina akiwa Waziri yeya akiwa Naibu, tulizungumza hapa kuhusu usumbufu waliokuwa wanaufanya Ziwani kwamba madhara yake tutayaona baadaye hawakutusikiliza. Leo tunalia samaki wameisha, wavuvi wamefilisika haya yote Mheshimiwa Waziri ameyapitia sasa tunataka tumpe ushauri atoke hapo alipoikuta Wizara, aende sehemu ambayo Mungu atamsaidia aendelee kubaki kwenye hii Wizara kama Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita tu kwenye suala la herein. Inahitaji kuwa mjinga sana kwa kizungu mnasema *you need to be very ignorant* kizungu ndiyo mnasema hivyo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake unatakiwa kuwa mjinga wa mwisho, kutoutambua huu mtego. Hawa wafugaji ni watu maskini na Serikali lazima wasikilize, hii biashara wanayoiweka wanaolalamika ni wananchi, wanaotutuma ni sisi Wabunge. Mwaka 2025 watasimamisha kukitetea chama chetu na kuomba tena nafasi ya kurudi humu kama hatuwasikilizi hawa na kuyaleta malalamiko humu ndani wakayafanyia kazi, wakaanza porojo za kupandishana, kuwekeana maneno mdomoni, haitatusaidia huko mbele tunakoenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, herein, mimi nafuga ng'ombe, watafiti na wataalam, waliosomea mambo ya mifugo, walianza wakaja hapa na mihuri ya kugonga si wao? Wakashauri tukiweka hivi tunapata thamani ya ng'ombe, wakagonga ngozi, wakaja wakavalisha bangiri, sasa wamekuja na hereni nataka niwaulize swali halafu mbaya zaidi tunatafuta takwimu sahihi za mifugo. Unaenda kuchukua wakala akufanyie takwimu ndiyo akukabidhi, hivi hatuna wasomi waliosoma mambo ya TEHAMA, tunasomesha watoto wetu kwa kazi gani? Nataka waniambie tulihesabu binadamu sensa yetu ya mwaka jana, kwa nini hawakuweka wakala? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliingia gharama bilioni 400, wakanunua vishikwambi, watu wakafanya kazi. Watoto wetu wamesoma TEHAMA, hawana ajira, wanaenda kuchukua mabilioni ya hela wanamrundikia wakala yumo humu ndani, ana-*lobby lobby* eti tufunge herein. Nataka niwaulize swali, sipingani na maagizo ya Waziri Mkuu, tunaboresha wasini-*quote* vibaya, hiyo hereni wanayoenda kuifunga, sidhani kama wamefuga ng'ombe, hivi ng'ombe wakigombana kule porini ikadondoka herein, wataniambia aliyepigana naye ni nani? Haya ng'ombe waangu wakihibiwa, wakaenda Mtwara kutoka Geita watanipigia Musukuma usiende pPlisi fuata wako Mtwara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utapeli ambao wanataka kutuingiza kutuchonganisha na wananchi. Mheshimiwa Waziri asikubali huu mtego, Wizara yakw iombe hela Serikalini, aajiri vitengo, katika kila halmashauri na kila kata tuna bwana mifugo ana kazi gani? Kwa nini asimpe takwimu za ng'ombe? Nataka niwaambie tusikubali huu mtego na Bunge likawa wakala wa kupitisha dili za watu humu ndani, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfugaji ni maskini, ili apate laki tano lazima auze ng'ombe, hivi Serikali nataka niwaulize, huyu mfugaji ambaye Tanzania hii hathaminiki anaishi kama mbayuwayu tu yuko huku, yuko huku, unaenda kuhesabu ng'ombe ambao leo wako Geita kesho wako Mtwara, kesho Bagamoyo, yanakoota majani ndiyo mfugaji anaenda. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kama kuna sehemu sasa amewekwa *target* ni hapa. Najua hili jambo alikuwa ulipendi maana tulikuwa tunateta kantini, sasa nataka nimwone *term* hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu wakala anayezungumzwa humu alishatajwa na Mheshimiwa Shabiby, atusamehe sana, sisi wote ni Wabunge na kila mtu ana neema kwenye jimbo lake. Jimbo la Kibaha linafuga kuku, tuzifunge kuku hereni kwanza kabla ya ng'ombe. Haiwezekani, hata kuku ni nyama na zinaingiza pato la Taifa. nikuombe sana Mheshimiwa Waziri akae vizuri asikubali huu mtego na najua watu tukizungumza humu wanasema huyu kafanyiwa lobbying kapewa hela, hakuna cha kutupa hela mimi ni mfugaji na Jimbo langu lina wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anayepiga upatu jimbo lake linaongoza kwa mabanda ya kuku, tuanze na kuku, tuone mfano, lakini tukimaliza hapo Mheshimiwa Ulega, najua tena nafurahi jana kulikuwa na wageni mashehe leo hawapo. Mashehe kazi yao ni kuomba na najua na wewe kwako kuna

ng'ombe, tujaribie Wilaya ya Mheshimiwa Waziri kwanza hizo herein, zikifaulu ndiyo walete hawawezi kuwa wanafanya majaribio kwa watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana hatuna nia mbaya na mategemeo ya Mheshimiwa Waziri, lakini anatuweka kwenye *angle* ambayo kiukweli siyo nzuri na Serikali yetu imetulia tunaenda kwenye chaguzi, watu wana amani, tumemaliza purukushani za machinga unaingia tena machinga mfugaji, hii kitu haiwezekani. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na hata yule anayepiga dili tuangaliane kwa macho hivi, sijui kaenda wapi? Kahamia wapi? Tusikubali hili suala, najitoa muhanga, tusikubali hili suala likazungushwa humu ndani. Waziri aweke teknolojia, aombe Serikali impe kompyuta agawe kwa kila Bwana Mifugo, Afisa Ugani kule katika kila Kata wapo, leo Maafisa Ugani kule wamekuwa wanywa gongo tu, wanakaa maofisini, ukienda wamechoka hawana hata kazi. Ni watu wa operesheni tu midomo, sijui miguu, hawana kazi za kufanya, Mheshimiwa Waziri apeleke watu, alafu aone maisha yanavyoenda… *(Makofi)*

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hivyo anavyozungumza tayari Wasukuma, wafugaji wote wa Mtwara, Geita, Mwanza na Magu wote ng'ombe zao zina herein, je, watarudishiwa fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msukuma, taarifa unaipokea?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa mimi ni mfugaji, kwanza ukiacha alizoziona zina hereni, kuna zinazodai yaani hata uwekaji wa hereni unalipa kwanza, unaingiza kwa mtu hela, halafu ndiyo anaenda kutengeneza. Nchi hii jamani inahitaji kusoma kwa mtaa kabisa, tuache shule za darasani. Nakubaliana na yeye kwamba kuna hereni, kuna nini, lakini ni maumivu makubwa ambayo wafugaji wanayo kule kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wafugaji wamekuja kusikiliza hii Wizara, tokeni nje hapo muwaulize hii si kitu wala siyo hitaji. Kama hitaji ni la Serikali tengeni bajeti, mbona sisi binadamu wametuhesabu bila kutuomba hela. Hivi binadamu na ng'ombe nani ana thamani unaacha binadamu anayeingiza kipato kumhesabu hata kwa shilingi elfu mbili mbili anatuhesabu bure, halafu ng'ombe wanaomlisha mtu anapata madini mwilini, wanaichaji elfu mbili. Hawana soko, hawana machungio, hawana sehemu ya kunyweshea maji, *wagosha wajameni*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tubadilishe mwelekeo, Mheshimiwa Waziri…

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma kuna taarifa, kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Shangai.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, kwenye minada yetu Wizara inapata shilingi 2,500 kwa kila mfugo unaouzwa. Watumie hizo fedha kuwahesabu hao ng'ombe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana nayo. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, asikubali kuingia kwenye huu mtego na hili akusanye hela atoke kwenye asilimia moja ya pato la Taifa, Mheshimiwa Waziri ananisikiliza au anachati? Atoke kwenye hii nafasi aliyobananishwa na naamini Wizara yake ina wasomi, tunamwamini sana rafiki yangu, msomi mwenzangu Shemdoe, wakae watengeneze utaratibu mzuri, haya mambo ya dili dili waachane nayo, ili upate kipato kizuri tujifunze kwenye Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini ilikuwa inachangia asilimia moja kwa sababu wachimbaji wadogo walikuwa wanawaona kama wezi, kila wanapovumbua madini wanawapeleka polisi, wanapiga watu wanaweka wazungu wenye leseni. Tulishauriana nao humu ndani leo angalia tunavyochangia kwenye pato la Taifa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina tatizo na, Mheshimiwa Ulega, lakini wakati wa ku–*wind up* hapa akija na jibu la mawenge mawenge namdakia shilingi yake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia siku

ya leo kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza nimshukuru Waziri na Naibu wake wamekuwa wasikivu unapowaambia jambo, tunamshukuru kwa sababu ni sifa pia ya kiongozi kuwaheshimu wenziwe na kusikiliza mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitajikita kwenye Fungu 64 - Uvuvi. Amezungumza kaka yangu Mbunge wa Kigoma hapa, tunasimama leo hapa *tension* iliyopo kwenye Mkoa wa Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa tunatamani tusikie kauli ya Mheshimiwa Waziri leo, masikio na macho ya wavuvi wa mikoa mitatu toka jana wanasubiri neno kwa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Rukwa na Katavi tunategemea Ziwa Tanganyika, Ziwa Tanganyika tuna – *share* zaidi ya Nchi nne kwa maana ya Tanzania yenyewe, Kongo, Zambia pamoja na Burundi. Kongo inatumia kwa asilimia 45 ya Ziwa Tanganyika. Tanzania asilimia 41, hizo nchi nyingine hizo mbili asilimia inayobaki ndiyo wanatumia wao. Unapoingia makubaliano ya kufunga ziwa na hizo nchi ambazo zina asilimia ndogo lengo ni nini, tunakwenda kumnufaisha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wengine wanaweza wakazungumza korosho ndiyo uchumi wao, madini ndiyo uchumi wao. Uchumi wetu ni Ziwa Tanganyika, ndiyo duka letu. Wavuvi hawa kwa sababu shughuli wanayoifanya ni halali ndiyo maana wanakata leseni kwa Serikali. Leo wamekata leseni ya mwaka mzima, Serikali inasema inakwenda kufunga Ziwa kwa miezi mitatu, watuambie, waliwashirikisha hawa wavuvi kwamba wanakwenda kufunga Ziwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakapokuja atuambie tafiti zake zinasema ni samaki wa aina gani wamepungua? Kwa sababu hawezi kusema anakwenda kufunga ziwa wakati pale kuna dagaa, kuna aina nyingi za Samaki. Kama tafiti zake ni sahihi lazima waje watuambie wamegundua ni samaki gani? Hawa ndiyo wafungiwe, huwezi kufunga ziwa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujiulize kwa nini tumefika hapa, lazima Wizara yako ijue kwa nini tumefika hapa? Kama ni kwa sababu nyepesi mnazotupa kwamba ni kupungua kwa samaki, kwa nini samaki wamepungua? Je, miezi mitatu ndiyo mmeona ni suluhisho la kurudisha samaki kwenye Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa samaki hakujapungua Ziwa Tanganyika peke yake na Maziwa mengine yote kuna upungufu wa samaki. Sasa kama sababu ni kupungua kwa samaki Serikali isije na majibu mepesi kwenye mambo magumu, lazima tuje na mkakati wa kudumu wa kuhakikisha tunazuia uvuvi haramu ndiyo changamoto ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza lazima uanze na kanuni zenu. Kanuni za uvuvi ni kanuni za ajabu sana, ambazo leo kuna kanuni zinakwenda kuwakandamiza wavuvi na kuwapa umasikini. Leo unaposema unakwenda kufunga Ziwa hujamshirikisha huyo mvuvi ambae unakwenda kufunga Ziwa, na ukiamini ndiye mwenye duka na leseni amekata. Mheshimiwa Waziri tukuite jina gani? Kwa sababu kama umechukua fedha za leseni ya mwaka mzima halafu unamfungia shughuli ambayo amekatia leseni, tuseme ni nini, uporaji? Tutumie lugha gani ambayo itafaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama Serikali ina nia njema kuongeza Samaki, kufunga ziwa miezi mitatu siyo suluhisho. Tuchukue hizo fedha ambazo mmetenga kwa ajili ya kufanyia *patrol,* kuwapiga wananchi ambao wanafanya kazi halali, shughuli halali, tukajenge vizimba ambao itakuwa mbadala wakati ambao tunasema tunasimamisha kwa muda ili Ziwa lipate Samaki, wananchi wawe na sehemu mbadala ya kupata kitoweo lakini kuweza kuendesha familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, pamoja na ujengaji wa vizimba napenda nishauri Mheshimiwa Waziri, mkiwa na ushirikishwaji mtaleta uelewa wa pamoja, tukiwa na uelewa wa pamoja tutafanya uwajibikaji wa pamoja. Tukitoka kwenye uwajibikaji wa pamoja tutakwenda kufanikisha kwa pamoja malengo chanya tuliyojipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hatuwezi kufikia huko kwa sababu hatujawashirikisha hawa wananchi. Nchi hii ni ya kwetu sote na kama ni ya kwetu tusiwaone hawa watu, kwa sababu kama kwa mujibu wa Katiba inatambua kazi hii kwamba ni kazi halali. Tukienda kuamua bila kuwashirikisha ni suala ambalo halikubaliki nasi Wawakilishi kwa sababu hamjatuambia au hamjatushirikisha, hatutakubaliana na hilo jambo kwa sababu halina nia njema kwa wananchi wetu, halina nia njema kwa wavuvi wetu na kwa sababu tunajua Wilaya kama ya Nkasi inategemea uchumi kutoka Ziwa Tanganyika, kwa hiyo ukienda kufunga unategemea na ile Halmashauri itaishije? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka Waziri aje atueleze hapa, utafiti walioufanya na je, wamewashirikisha wananchi? Kama hawajawashirikisha wazo letu kwa pamoja Wabunge wa Mikoa Mitatu kwa sababu na sisi tunahitaji samaki wengi, turudi kwanza kuwashirikisha wananchi wetu ambao ni wavuvi. Tuwashirikishe wadau wote wa uvuvi na haya mambo hakuna sababu ya kugombana kama kweli nia ni njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena tunajua hili jambo Waziri ulisema lakini tunataka leo wavuvi wetu wapate kauli moja, lini utawashirikisha kabla ya kufanya hayo maamuzi mliyopanga Tarehe 15, ili na wao watoe mawazo yao kwa sababu lengo ni kujenga nchi yetu na kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kufikia huko Mheshimiwa Waziri unaposikiliza yafanyie kazi mawazo ya wavuvi. Wavuvi wameshakuja mara kadhaa kulalamikia baadhi ya kanuni ambazo hazifai. Hizo kanuni ambazo tunazitoa leo ni lazima tuwe na lugha moja, hivi leo ukifunga Ziwa unasema tumekubaliana na Congo, ninyi mtapata nguvu wapi ya kwenda kuangalia Congo kama wamefunga hawatavua? Lakini kwa hali ya kawaida hivi huyu Zambia mwenye asilimia ndogo sana umekubaliana naye, unakubaliana naye kwa ajili ya nani? Sisi tunakubaliana kwa ajili ya wananchi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida muda wako umeisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, ajiandae.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia na mimi nichukue nafasi hii nikushukuru kwanza wewe Mwenyekiti kwa nafasi hii ambayo umenipa, pia nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa hotuba nzuri aliyoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wewe ni rafiki yangu, umekuja Kigoma mara nyingi sana, Kigoma unaifahamu, hasa eneo la uvuvi. Kwenye eneo la Mifugo kwa kweli hujafanya vizuri. Wewe umekuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi lakini umekuja kwenye Jimbo langu hasa kushughulikia kwenye eneo la uvuvi. Kwenye hilo naomba nikushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba nizungumzie mambo mawili, kwanza kwenye eneo la mifugo. Eneo la mifugo Mheshimiwa Waziri ninakupongeza Waziri aliyekutangulia alikuja Wilaya ya Uvinza kutoa eneo kwenye Ranchi ya Taifa ili liweze kutumika kwa ajili ya wafugaji. Hilo ni jambo jema sana. Ni baada ya mimi kuja kuomba Bungeni hapa na Wizarani, Waziri aone namna ya kutenga eneo ambalo litasababisha wananchi wale ambao ng'ombe zao zinazagaa katika vijiji vyote 61 waweze kupeleka ng'ombe huko. Hili jambo nashukuru lakini Mheshimiwa Waziri utekelezaji kwa maana ya kuhamisha wale ng'ombe kwenye vijiji 61 haujafanyika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja Kigoma kwenye ziara, alipoandamana na Naibu Waziri wako huyo Mheshimiwa Silinde ambapo naye ndiyo aliteuliwa kuingia kwenye Wizara hiyo akiwa Kigoma, nilimwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba naomba Naibu Waziri aje aweze kutatua huu mgogoro ahamishe kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa na Wilaya waweze kuweka mikakati mizuri ya kuondoa hizo ng'ombe katika vijiji hivyo ili wananchi wabaki salama wale wanaojishughulisha na kilimo, kwa sababu kilimo ndiyo uti wa mgongo lakini kilimo ndiyo kinachosaidia wananchi wetu wadogowadogo kwa ajili ya kujikimu na maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale ng'ombe wanapoendelea kubakia kwenye vijiji, maana yake kwa kweli

habari ya kilimo haipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri unaona jinsi ambavyo unapingana na Wizara ya Kilimo. Sasa hili nakuomba, lakini ng'ombe wale wamezagaa kwenye misitu ya *TFS* kwa hiyo unapingana pia na Serikali kwa upande huo mwingine. Itakapohamishwa hiyo mifugo maana yake kule itabidi uweke miundombinu kwa ajili ya majosho ambapo kule vijijini hakuna josho hata moja. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hilo ni la kwanza, naomba sana kwenye eneo hilo nadhani baada ya Bunge hili la bajeti nakuomba ama wewe ama Naibu Waziri aje kule Jimboni ili tuweze kufanya mikakati ya namna ambavyo tunaweza tukahamisha hiyo mifugo kupeleka kwenye eneo lililo rasmi, naamini Serikali itapata mapato kulikoni ambavyo ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine Mheshimiwa Waziri ni kwenye eneo hili ambalo limezungumzwa na Wabunge wenzangu kwenye eneo la samaki. Mheshimiwa Kilumbe ameongea vizuri sana, Mheshimiwa Aida amezungumza vizuri sana. Kwa kweli kwenye eneo hili Wabunge wa Mikoa mitatu ya Kigoma, Katavi, Sumbawanga, ndio ambao tuko kwenye ukanda wa hilo Ziwa Tanganyika, Mheshimiwa Waziri nataka nikuambie kwamba ziwa Tanganyika ndiyo chanzo kikuu cha mapato katika Mikoa hii mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hata hizi Halmashauri zetu zipo kwa sababu ya uvuvi, hakuna namna nyingine. Nataka nikuambie, nimekwenda kufanya ziara kwenye Kata mbili, Sigunga na Mgambo nilichokiambulia ni hiki. Kata ya Sigunga waliniambia Mheshimiwa Mbunge tunaomba kama Ziwa linakwenda kufungwa tuandalie makaburi, hatuna kazi nyingine ya kufanya, kazi yetu ni hapo ziwani. Sasa hebu niambie hiyo kauli ni nzuri kwa wananchi ambao ni wapiga kura? Nikasema siwezi kuwaandalia makaburi lakini Serikali lazima iwe makini namna ya kutekeleza hili jambo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kule kwenye Kata waliniambia kama Ziwa linakwenda kufungwa niwatafutie kazi nyingine ya kufanya.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Askofu Gwajima.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa anayezungumza kwamba Ziwa Tanganyika linategemewa na nchi nne, sehemu kubwa ya Ziwa hili ipo Congo na mtaalam Waziri anafahamu kwamba samaki huwa wanahamahama katika kuzunguka zunguka. Ukifunga kwetu huku kule Congo wanaendelea kuvua. Utakuwa umefanya uamuzi wa kijinga wa kuisaidia nchi nyingine kile ambacho ungekipata wewe, kinatumiwa na nchi nyingne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine zote zitaendelea kuvua halafu wewe utaacha kuvua, wale watapata wewe utakuwa maskini. Kwa hiyo namjulisha mzungumzaji kwamba ni uamuzi usio wa kisayansi.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon taarifa unaipokea?

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo iko sahihi lakini nadhani haelewi ni kwamba hili Ziwa linafungwa kwa maana ya nchi zote hizo zinazozunguka eneo la Ziwa, lakini mimi nazungumzia upande wangu kwamba wananchi wa Kata ya Buhingu wanasema niwatafutie kazi

nyingne ya kufanya, maana yake ni kwamba kazi yao wao ni hiyo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kutokana na kwamba jambo hili halikuwa na ushirikishwaji, Wabunge wenyewe hatukuwa tumelijua, pamoja na kwamba wananchi wetu kule Majimboni walikuwa wanajua kwamba Wabunge tumeshazungumza hili huku Bungeni au tumekwisha zungumza na Waziri jambo hili, hatukuwa tumezungumza na Waziri jambo hili, nasi kama wananchi ambavyo walikuwa hawalijui nasi pia Wabunge tulikuwa hatulijui. Kwa hiyo, jambo ambalo linatakiwa hapa ni kuona namna ya kutushirikisha Wabunge, wadau wa uvuvi na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna haja ya kufanya siri ya jambo hili, Ziwa ni la wananchi na Ziwa ni la Serikali na wananchi lazima watii sheria za nchi Serikali ambazo zipo ni jambo la kawaida lakini lazima kuwe na ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza ipo timu kubwa ya wavuvi ambao wako hapa Dodoma, wamekuja kukutana na Waziri na leo baadhi yao wataingia humu Bungeni wakati Waziri atakuwa ana-*wind up* watakuwa wanamsikia. Kwa hiyo, naomba jambo hili….

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Serikali ilichukulie kwa umakini sana na Wabunge hoja yetu siyo kukataa Serikali isifunge Ziwa, lakini hoja yetu ni kushirikishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Ahsante, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama katika Bunge lako hili Tukufu, pia kwa namna ya pekee sana naomba nimpongeze na nimshukuru Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kututeulia watu makini wanaoijua Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na muda naomba nijielekeze moja kwa moja kuchangia Fungu Namba 64 linalohusu masuala ya uvuvi, kuanzia ukurasa wa 68. Tunafahamu kabisa uvuvi na ufugaji hii ni sekta ya uzalishaji nasi kama vijana tunaamini sana sekta hii ingewekezwa vizuri ingetatua changamoto nyingi za vijana ikiwemo ajira lakini ikiwemo kutufanya vijana tuweze kufanya biashara kutokana na mazao ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana nimekuwa nikisimama kwenye Bunge hili mara nyingi, nikielezea na nikiomba Serikali itupe ufafanuzi wa namna ambavyo wanawekeza kwenye Ziwa Tanganyika. Majibu yamekuwa ni utafiti, utafiti, utafiti, utafiti unaendelea! Sasa hili ni jambo la aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumebarikiwa Mungu ametujaalia tuna maziwa mengi, tuna Ziwa Tanganyika, tuna Ziwa Nyasa, tuna Ziwa Rukwa, tuna Ziwa Victoria pia tuna Bahari. Ni aibu kuona leo sekta hii ya mifugo na uvuvi

inachangia kwa asilimia ndogo sana kwenye Pato la Taifa, ni aibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu tunawalaumu viongozi, lakini Serikali kwa kiasi kikubwa imefanya mchango wa uvuvi usionekane. Leo tukienda huko kwa Maafisa Uvuvi hali zao ni mbaya sana. Ukiangalia Mkoa wa Kigoma, ukiangalia Mkoa wa Katavi, ukiangalia Mkoa wa Rukwa vitendeakazi, miundombinu bado ni hafifu sana. Bado tunategemea sekta hiyo ya uvuvi izalishe, inazalishaje? Labda kama tunataka miujiza, lakini hatuwezi kuzalisha, hatuwezi kuona tija ya sekta hii kama hatutafanya uwekezaji wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya kwa sababu leo hii ukiangalia Mkoa wa Kigoma, Wilaya zinazofanya uzalishaji, Wilaya zinazofanya uvuvi ukiwaambia hata vitendeakazi wanafikaje *site?* Hawana magari, hawana hata pikipiki za kuwafanya wafanye *movements* za kwenda kufuatilia. Sasa unataka kuniambia kwa mazingira hayo ni namna gani sekta hii italeta tija kwa Taifa letu? Kwa hiyo, kuna haja kubwa sana ya Serikali kuwekeza katika sekta hii ili tuone tija yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitamani kulizungumza kwenye sekta ya uvuvi, wamezungumza hapa Wabunge wengi vizuri sana na mimi naungana nao. Sisi watu wa Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi, uchumi wetu kwa asilimia 90 unategemea Ziwa Tanganyika. Tumekuwa tukiongea hapa tuna masikitiko kwa sababu tunaona Serikali ni kama haitambui umuhimu wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo hii bado siku Nane, Wawakilishi wa Wananchi hatuna taarifa rasmi kuhusu kufungwa kwa Ziwa! Bado siku Nane! Haiwezekani maamuzi

makubwa kama haya, maamuzi ya kuwakosesha ajira watu wetu, ndani ya Mikoa mitatu bila kuwashirikisha wananchi…

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kilumbe.

**TAARIFA**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, wakati Serikali yetu na Serikali hizo nyingine zimefanya makubaliano katika jambo hilo, ukiingia kwenye *internet* Bunge la Congo limekataa hoja ya kufunga Ziwa Tanganyika, kwa maana hiyo na leo tuko kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunazungumza nasi tunakataa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia taarifa unaipokea? Endelea na mchango wako.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa ninaipokea kwa mikono miwili. Sisi Wawakilishi wa Wananchi hasa tunaotoka Ukanda wa Ziwa Tanganyika jambo hili hatukubaliani nalo kwa asilimia zote. Tutakubaliana nalo tu endapo Waziri atakapokuja atatuambia njia mbadala ya watu wetu ndani ya miezi mitatu hii wanaishije? Kama kuna vizimba kwa ajili ya watu wetu tutakubaliana nalo. Tunamuomba Waziri uandae majibu mazuri, kwamba ndani ya miezi mitatu hii tunapofunga Ziwa, wavuvi wetu, wafanyabiashara wadogo ambao wanategemea mazao ya samaki na sisi wananchi ambao tunategemea tupate kitoweo, tunaishije ndani ya miezi hii mitatu? Tunaomba tupate *alternative* ndiyo hapo tutakapounga mkono jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza hii ni Serikali yetu na ni Serikali sikivu, kama jambo hili ni kwa manufaa wavuvi kwa nini tusiambiwe mapema? Kwa nini msisikilize ushauri wetu? Kwa nini msitake maoni yetu? Kwa hiyo mimi niseme tu, Mheshimiwa Waziri wewe ni Kaka yangu na ninakuheshimu sana na wewe unajua mimi nakuheshimu sana, lakini katika jambo hili la kufunga Ziwa bila kutushirikisha wananchi, hapana hatuko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana jioni tumesikia maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka jana Tarehe 03 Novemba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizuia suala la herein, ukisoma taarifa ya Wizara utaona Tanzania ni ya pili Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, lakini ukifuatilia kwenye suala la uuzaji wa mifugo yetu nje, Tanzania tunazidiwa na nchi ambazo hata haziko kwenye *top* 10. Hii yote inatokana na sababu mifugo yetu bado haina *quality* ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa kama tuko kisiwani, Waziri Mkuu kaongea vizuri na mimi ningependa niishauri Serikali kwamba changamoto ya hereni ilikuwa ni bei ya hereni, lakini kama Serikali itafanya utaratibu mzuri ambao hautakuwa na changamoto kwa wafugaji, jambo hili lina tija ili kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, ameongea hapa Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Kaskazini, watu wa Tanganyika, watu wa Ziwa Tanganyika, watu wa Mkoa wa Kigoma, Rukwa na Katavi tunaomba Serikali ichukulie jambo hili kwa uzito sana, tunaomba Serikali ije na majibu mazuri itueleze ni amna gani tunaenda kumaliza suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sylvia. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia katika bajeti ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 katika Wizara hii nilikamata Shilingi, na niliahidiwa ahadi nyingi tu na Mheshimiwa Waziri aliyetangulia, lakini mdogo wangu Mheshimiwa Ulega, yeye ndiye alikuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Katika yote niliyoahidiwa, ni moja tu ambalo nimelipata. Bahati mbaya sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha hayupo, lakini siku hiyo yeye ndio alikuwa amenipa ushawishi mkubwa sana katika kusema kwamba, shida kubwa ya wafugaji ni malisho, shida kubwa ya wafugaji ni maji. Serikali imenunua mitambo mikubwa, adha hiyo ambayo mwaka ule ilipatikana, kwa mwaka huu haitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliambie Bunge lako Tukufu, hadi tunapozungumza leo hii, wakulima na wafugaji bado wana migogoro mikubwa inayotokana na wafugaji katika kutafuta malisho na maji. Napata shaka, niliambiwa mwaka ule nisubiri mpaka mwaka huu. Naomba nitangaze tu, nina dhamira ya kushika shilingi ya Waziri wakati utakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliahidiwa majosho kumi, mpaka dakika hii nimepata majosho manne tu. Niliahidiwa mabwawa mawili, mpaka tunazungumza dakika hii, hakuna hata bwawa moja ambalo limechimbwa. Niliahidiwa visima, hakuna hata kisima kimoja. Vilevile tuliahidiwa kupata madume

bora ya nyama kwenye Halmashauri ya Morogoro Vijijini, hakuna kitu kama hicho. Ni kielelezo tosha kwamba Serikali haiwezi kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ushauri kwa Serikali. Cha kwanza, ninaamini na ninaomba, sisi Wabunge tupambane wote hapa, hasa kwenye sekta ya mifugo; wale Wabunge ambao mikoa yao wanatoka wafugaji, tuone ni jinsi gani tunaishauri na kuishawishi Serikali, katika kipindi ambacho ni cha siku zile tano, Serikali na Kamati ya Bajeti wanakaa, na bahati nzuri Mwenyekiti ambaye leo unaongoza kikao ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tuone jinsi gani tunasaidia sekta ya mifugo kuongezewa fedha ili iweze kukabiliana na changamoto za migogoro ya wakulima na wafugaji, na changamoto wanazozipata wafugaji wetu katika kuhamahama ambapo inawaletea hasara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, amekuja na hoja ya kusema kwamba anataka kuanzisha mamlaka maalum ambayo itashughulikia matatizo au changamoto za wafugaji na wavuvi. Kwa ushauri wangu, tulikuwa na changamoto kwenye barabara, maji, na umeme. Ushauri wangu Mheshimiwa Waziri, hebu tusiende kwenye mamlaka, twende kwenye wakala. *TARURA,* imeondoa changamoto za barabara katika nchi yetu, lakini *RUWASA* imeondoa changamoto za maji, ndiyo maana sasa hivi Waziri wa Maji anatamba. Kwa hiyo, nakuomba na wewe, badala ya kwenda kwenye mamlaka, twende kwenye wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na changamoto kubwa za upatikanaji wa umeme katika nchi hii, vijijini hata mijini, lakini kupitia *REA,* leo kila Mbunge anapata faraja na wananchi wanaona kazi ambayo inafanywa na *REA*. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Waziri, kwenye suala la mamlaka, tusiende kwenye mamlaka, twende kwenye wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuishauri Serikali yangu, hebu tuangalie, sasa hivi wafugaji wanapata wakati mgumu, na vilevile hata watumiaji wengine wa ardhi. Angalieni uwezekano wa kukutana na Wizara ya Maliasili na Utalii, na Wizara ya Ardhi, twende tukaweke mipaka kwenye maeneo ya hifadhi. Wafugaji na wakulima, hawana *GPS*. Utajikuta ghafla bin vup, wameingia ng'ombe kwenye hifadhi, wakulima wameingia kwenye hifadhi, wanapata *fine* kubwa ambazo zinawapa wakati mgumu wafugaji na wakulima wetu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu tuangalie katika mwaka huu wa fedha, jinsi gani Wizara tatu; Ardhi, Wizara yako ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maliasili na Utalii, mwende mkaondoe chagamoto ambazo wanapata wafugaji na wakulima wetu katika maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namwomba Mheshimiwa Waziri, sijajua katika mwaka huu wa fedha mmetenga kiasi gani cha fedha kwenda kuendelea kutafuta maeneo ya malisho. Nimeona katika bajeti yake amesema kuna maeneo 77 yamepatikana ambapo zimepatikana hekta 994,827, lakini kuna Wilaya 14, Wizara ya Ardhi imetenga maeneo ya ardhi, naomba tuendelee kutenga kuweka fedha, ili tuendelee kutenga maeneo makubwa tuondokane na matatizo ya malisho na maji kwa wafugaji wetu na vilevile watumiaji wengine wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania bado ni kubwa. Ninaamini kabisa kwamba, tunaweza kuwa na maeneo mengine kama tulivyofanya pale Handeni, kama Serikali itajipanga vizuri. Katika hili naomba tu, Mheshimiwa Waziri, wewe ndiye mwenye dhamana hii. Waziri wa Maliasili katika kuinusuru Ngorongoro, alishirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Ardhi na wewe Waziri wa Mifugo mkaweza kupeleka kule ng'ombe. Sasa nakuomba, bado tuna changamoto, migogoro mikubwa itaendelea kutokea, lakini pamoja na migogoro

tunaipeleka nchi kwenda kwenye jangwa. Lazima tuandae maeneo ambayo tutapeleka wafugaji wetu kwenda kufanya shughuli zao za mifugo bila migogoro yoyote kwa wananchi, na wao bila kupata hasara kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent. Muda wako umeisha. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi na Mheshimiwa Zubeir Mohamed Kuchauka, ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa fursa hii kuchangia hoja hii ambayo iko mbele yetu. Nami nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa na Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ridhaa yako nisome kwenye randama ambayo imewasilishwa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kulikuwepo hoja nyingi sana ambazo zimejibiwa kwenye randama. Hoja namba sita ilikuwa inahusu ugawaji wa vitalu katika eneo la *Ranch* ya *Mwisa II,* na Wizara katika hiyo hoja imejibu. Naomba nisome. Serikali inasema, na ninaomba watu wangu wa Muleba wasikie. "*Zoezi la ugawaji wa vitalu katika Ranch ya Mwisa II haliendelei.*" Hiyo ni kauli ya Wizara ambayo naamini ni kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendeleo kusoma. *"NARCO inasubiri maelekezo ya Serikali baada ya Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kumaliza kazi yake iliyokuwa ikiifanya katika eneo la Mwisa II."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na ninaomba atakapokuja kuhitimisha hotuba yake, haya maneno ayaseme na ayawekee msisitizo na mkazo ili watu wangu wa Muleba ambao wameteseka sana, wananyanyaswa, wanaambiwa waondoke kwenye hili eneo ambalo ni eneo la makazi yao, kuna babu zao walizikwa pale, kuna makaburi yao, lakini leo unapokuja kuwaambia waondoke, Mheshimiwa Waziri haikubaliki hiyo, na hatutakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru watu wa Kigoma kwa mshikamano wao kuhakikisha kwamba Ziwa Tanganyika halifungwi. Nawapongeza kwa mshikamano wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Mwisa ni eneo la wananchi wa Muleba. Nimesoma kwenye randama na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema, mmiliki wa Mwisa na Rutoro ni *NARCO*. Tangu lini? Kwa mamlaka ipi? Utakapokuja kuhitimisha hii hoja Mheshimiwa Waziri, naomba utuambie, kama eneo la Mwisa II na Rutoro ni mali ya *NARCO,* kwa nini tuna Hati za Vijiji ambavyo vimesajiliwa na tumepata hati za mwaka 2000? Inakuwaje Mheshimiwa Waziri? Mheshimiwa Waziri utakuwa mtu wa kwanza kuhamisha watu kutoka kwenye vijiji kuwapeleka mbugani na kuwaleta ng'ombe waishi kwenye vijiji, haikubaliki. Hii tutaiingiza kwenye vitabu vya *Guinness* sijui ya mwaka gani! Haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mwisa II limechukua muda wetu mwingi sana. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anaongelea migogoro ambayo imezaliwa mwaka

2022/2023 zaidi ya migogoro 55. Anasema wametatua migogoro 13 tu, ina maana *NARCO* kazi yake na Wizara ni kuingia na kutatua migogoro ambayo wanaisababisha wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30 Juni, 2022 tulikaa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, alituita kwa ajili ya kujadili suala la Mwisa na suala la Rutoro. Kati ya maazimio tuliyofikia, tulisema suala la Mwisa lisimame mpaka hapo tutakapopata suluhu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Nakushukuru umelitamka hilo Mheshimiwa Waziri. Nakuomba hayo uliyoyasema yawe ni maneno ya kweli na hao watu ambao wanapita huko Muleba kwenye hayo maeneo yenye mgogoro, wanawaambia wananchi wahame, sijui wawapishe wawekezaji; Mheshimiwa Waziri nakuomba, utakapokuja kuhitimisha utoe kauli yenye uhakika hapa ili watu waendelee na maisha yao. Naomba Serikali itamke, kama tunasubiri taarifa ya Waziri Mkuu, wananchi ambao waliishi kwenye hivi vijiji, waendelee na kazi zao za kuzalisha mali, na waendelee kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea hapa nadhani wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilisema lile eneo la Mwisa ni kubwa. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema ni hekta 66,000, lakini naweza kusema ni zaidi ya hapo. Ndiyo maana tunaomba hili eneo likapimwe upya, vile vitalu vikapimwe upya, tukafanye uhakiki wa lile eneo. Sisi wakazi wa eneo hilo, tunalijua, siyo hizi hekta 66,000 alizotuambia, hapana, ni zaidi ya hapo. Tukishalipima upya, tukapanga matumizi bora ya lile eneo, tunakubali ndio, kaleteni wafugaji, lakini lazima lile eneo tukishalipanga tuhakikishe kwamba, tunatunza na mazingira ya lile eneo. Tunataka tupate maeneo ya kulima, tupate maeneo ya ufugaji na tupate maeneo ya mifugo kwa kutunza ikolojia ya Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, lile eneo la Mwisa ndiyo eneo linalozalisha chakula kinacholisha Wilaya ya Muleba na Mkoa wa Kagera. Tunaposema tunakwenda kuweka wafugaji pale, tunautangazia njaa ambayo haitakuwa na ukomo Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili tuliangalie. Naomba nisisitize na nitaendelea kulisisitiza suala la Mwisa II na *NARCO* ni maeneo ya vijiji vya wananchi. Ni vijiji vilivyosajiliwa na Serikali hii ambayo inasema ni vitalu. Sasa kupanga ni kuchagua; kama tutasema ni vitalu, *then* tutangaze. Serikali itoe tangazo kwa wananchi wote kwamba vile siyo vijiji ni vitalu, *then* wananchi mkawapangie maeneo mengine ya kuishi, siyo kuwaachia wenyewe watafute mahali pa kwenda. Haiwezekani! Hii nchi yao, wamezaliwa kwenye vijiji vyao, lazima tuwaheshimu na tuwape heshima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uvuvi, Kata ya Mazinga wamenituma nimwombe Mheshimiwa Waziri ifuatavyo: Kata ya Mazinga tuna kikundi kimoja kinaitwa UWAMAKAMA, wanasema waliomba mkopo, kwenye mikopo iliyotolewa na Wizara, lakini bahati mbaya hawakupata mkopo, hawaku-*qualify,* lakini wametekeleza vigezo vyote. Wanaomba kwenye mgawo wa mkopo ujao wapatiwe mkopo kwa ajili ya kufuga samaki wa vizimba. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Muda wako umeisha.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la wageni waliopo Bungeni mchana huu. Wapo wageni 36 wa Mheshimiwa Mussa Sima, ambao ni Wachungaji na Wanakwaya kutoka Kanisa la Pentekoste, Singida Mjini. Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai ajiandae.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nampongeza sana Rais kwa jitihada kubwa anazozifanya za kutafuta fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii ya jitihada kubwa za Rais kutafuta fedha kwa nchi yetu kwa ajili ya maendeleo kwa ujumla, nimepata maswali mengi sana, kwa nini sekta ya mifugo inapata fedha kidogo? Nilipoendelea kusoma *document* yao hii ya bajeti nimeona kuna changamoto kadhaa. Moja, sioni sayansi. Sijaona sayansi kabisa katika *document* yao. Ukiangalia ni kiasi gani cha fedha kimeelekezwa katika *Research and Development,* huoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakutana na changamoto kule Ziwa Tanganyika kwamba ghafla tu ziwa lifungwe. Je, kama tulikuwa tumewekeza kiasi cha kutosha katika *R & D,* leo tusingekutana na changamoto hii. Kama tungekuwa tumewekeza kiasi cha kutosha katika *Research and Development* tungepata malisho ya kutosha kwa ajili ya mifugo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya wana ng'ombe milioni 14 peke yake, lakini *they are the second largest milk producer* katika Afrika kwa ng'ombe milioni 14 tu. Nini walifanya? waliwekeza sana katika *research and development*. India sasa hivi wanalisha ulimwengu katika maziwa. Asilimia 24 ya maziwa yote duniani yanazalishwa India. Nini India wamefanya? Wamewekeza sana katika *research and development*. Kwa hiyo, bajeti hii haitoshi kwa sababu hakuna fedha ya kutosha kwenye *research and development*. Vyuo vyetu vya mifugo pamoja na uvuvi, unaona pesa nyingi ni kwa ajili ya uendeshaji tu, huoni fedha ya kutosha kwenye *research*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni biashara katika bajeti hii. Ukiangalia katika ufanyaji wa biashara ya mifugo, Tanzania *is highly costly. It is very cost* kufanya biashara ya mifugo Tanzania. Nimeona kwa mfano biashara ya *exportation* ya *5 tons* za *mutton,* nyama ya mbuzi, Tanzania gharama ni kubwa sana, ni zaidi ya Shilingi milioni 10 uki-*compare* na nchi ya Kenya. Kwa hiyo, ile mikoa ambayo iko pembezoni, wana-*opt* zaidi kufanya biashara Kenya kuliko Tanzania. Badala yake watu wa mifugo wangejielekeza kuhakikisha kwamba *economies of scale* inaongezeka kwa maana ya ku-*encourage* wafanyabiashara wengi kwa Tanzania na ndiyo ingeweza kupunguza ule utitiri wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wenzetu wa Kenya unaweza ukatumia Shilingi bilioni 15 mpaka 16, wame-*cut down* zile *cost* nyingi kwa sababu kuna idadi kubwa ya wafanyabiashara. Kwa kufanya hivi, nchi yetu pia ingeweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sijaona *collection centers* za maziwa. Maziwa yetu mengi hayaingii katika mfumo rasmi wa biashara kwa sababu, hakuna *milk collection centers.* Pale

Serengeti tumejaribu kutaka kuweka kiwanda cha maziwa. Utafiti umeonesha, ni lazima mwekezaji atumie pesa nyingi sana kwa sababu bado Serikali haijawekeza kwenye *collection centers.* Kwa hiyo, tuiombe sana Wizara iende kuwekeza kwenye *milk collection centers* kwa sababu zitaongezea mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni miundombinu ya ufugaji. Sasa hivi kule kwetu wanyama wengi wanaingia kwenye mapori, wanaenda kwenye mapori ya akiba, wanaingia kwenye hifadhi kwa sababu hakuna maji ya kutosha, na hakuna malisho. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii tutengee fedha ya kutosha. Serengeti peke yake tuna zaidi ya ng'ombe 600,000, tunahitaji zaidi ya majosho 30, tunahitaji zaidi ya malambo 25, kwa sababu yaliyopo sasa hayatoshi. Tunakuomba kwa uwekezaji huu, tunaweza tukawa-*boost* wale wakulima ili waweze kufanya uzalishaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado *transformation* ya *income* ya mfugaji ni ndogo. Leo ukienda vijijini wanahitaji zaidi fedha ili waweze kuendesha maisha yao, tofauti na huko nyuma. Pamoja na kwamba pesa hii ya mkulima na mfugaji, bado ingeongeza *National income* pamoja na *individual income*. Sasa kazi ambayo wenzetu wa Wizara hii wanayo, ni kuhakikisha maziwa na mazao mengine yote ya mifugo wanaweza kuyabadilisha yakaleta fedha na waongeze ubora, lakini sasa unaona hakuna jitihada hizi zikiendelea. Kwa hiyo, tuombe sana Wizara, wenzetu vijijini nao wanahitaji maisha mazuri, wanahitaji kulipia bili za umeme, maji, wanahitaji kusafiri, wanahitaji vocha, wanahitaji simu na haya yanawezekana kama tuta-*transform* sekta hii ya maziwa na sekta ya mifugo kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika vituo vyetu vya uzalishaji wa ng'ombe, ukienda pale Mabuki unaona kazi inafanyika, lakini vifaa gani wanatumia? Teknolojia gani wanayoitumia? Bado ni *very old,* haiwezi kufanya watu hawa wakasonga mbele, haiwezi kufanya wazalishaji wa maziwa wakapiga hatua kwa sababu, uzalishaji huu ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona soko la nyama, bado soko letu la nyama limeendelea kuwa na wasiwasi mkubwa duniani kwa sababu hatu-*clear information.* Ukiangalia kuna baadhi ya magonjwa ambayo yaliwahi kuikumba nchi yetu na mpaka leo hatujawahi kutoa taarifa katika ulimwengu juu ya magonjwa haya kwamba tumepambana nayo. Kwa hiyo, nadhani ukiangalia kwa ujumla huioni *concept* ya biashara, huoni jinsi gani Wizara hii imejipanga vizuri ku-*trade,* huoni namna gani inatafuta *information* ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Muhammad Yunus anadai ukienda China peke yake, mtu mmoja anatumia zaidi ya kilo 60 za nyama kwa mwaka. Ukienda Marekani mtu mmoja anatumia zaidi ya kilo 55 za nyama kwa mwaka; haya yote ni masoko. Ukienda Bangladesh kuna masoko makubwa, ukienda India kuna masoko makubwa, ukienda *South Africa* kuna masoko makubwa. Lakini kwa nini hatuwezi ku-*trap* masoko haya, ni kwa sababu hatujakaa kibiashara zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana wenzetu wakae kibiashara. Tunaomba wawekeze uwekezaji mkubwa, matokeo makubwa ya kufanya vizuri…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amsabi, muda wako umekwisha.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi mchana huu nitoe mchango wangu kwenye mada iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoendelea kuuheshimisha Mkoa wa Lindi. Leo hii Mkoa wa Lindi tunataka kujengewa kituo kikubwa pale cha bandari ya uvuvi, lakini vilevile tuna kile kiwanda chetu cha *LNG,* kuna chuo kikubwa pale kinataka kujengwa na ndugu zetu wa Nishati. Kwa hiyo, kwa vyote hivi niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuutupia jicho Mkoa wetu wa Lindi ili na wenyewe uinuke kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu anasema usiposhukuru kwa kidogo basi huwezi kushukuru kwa kikubwa, na vilevile usipomshukuru mwanadamu mwenzio basi hata Mungu huwezi kumshukuru. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha mwaka uliopita 2022/2023 kujenga lambo pale kwenye Kata yetu ya Kimambi. Pamoja na kwamba lile lambo halijakidhi viwango kulingana na wingi wa mifugo waliopo kwenye Mkoa ule wa Lindi, nishukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu turejee kwenye historia kwa nini ng'ombe wako Mkoa wa Lindi leo. Miaka ya 2012

kwenda 2014 baada ya kule Ihefu kuonekana kwamba wale wafugaji wanaharibu ekolojia, wakaja viongozi kutoka Serikalini kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara wakiomba nafasi lakini Mkoa wa Mtwara wakakataa, sisi Mkoa wa Lindi tukakubali, na Mkoa wa Lindi Wilaya ya Liwale ndiyo ilikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Liwale tulitenga maeneo matatu kwenye Kata za Kimambi, Lilombe na Mlembwe kwenye Kijiji cha Ndapata. Lakini masharti yalikuwa kwamba kabla hao ng'ombe hawajaja miundombinu itangulie. Mpaka leo naongea hapa ndiyo lambo la kwanza limejengwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuliambiwa kwamba tutaletewa malambo na majosho kabla hawa ng'ombe hawajakanyaga kwenye ardhi ya Mkoa wa Lindi. Lakini leo tunazungumzia 2023 tuna lambo moja tu kwenye Kata ya Kimambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ukianzia Nangurukuru mpaka Liwale kote kumejaa wafugaji. Kwa mfano kama Wilaya ya Kilwa kuna Vijiji vya Zinga, Nangurukuru, Njinjo, Kipindimbi mpaka unafika Kimambi, kote kumejaa wafugaji. Lakini uone urefu wa kutoka Nangurukuru mpaka Liwale, kilometa 230, kuna lambo moja tu kwenye Kata ya Kimambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongea na wataalam wa ufugaji kule wanakwambia mahitaji yetu kwenye Wilaya ile ya Liwale tunahitaji kuwa na malambo matatu kwenye Kata ya Kimambi, lambo moja kwenye Kata ya Lilombe na lambo moja kwenye kata ya Ndapata. Kwa ujumla wake tunahitaji malambo saba ili tuweze kunufaika na watu wale wa Liwale nao wajione kama walikubali mifugo na wananufaika na mifugo hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa majosho hatuna josho hata moja. Ukiwauliza wataalamu wanakwambia tunahitaji majosho matatu, angalau kwenye kila kata tupate josho moja moja, kwenye zile kata ambazo zimekuwa zikipokea wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu angalia umbali uliopo kutoka Kimambi kwenda Ndapata, ni zaidi ya kilometa 222. Kutoka Lilombe kwenda Kimambi ni kilometa 111, hawa wafugaji wanatembeaje kufuata hili bwawa lililopo kule Kimambi? Uone umuhimu wa kuhitaji malambo kwenye ile wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa tumepokea mifugo tuna jambo lingine la minada. Tunao mnada mmoja lakini mpaka sasa hivi bado una kizungumzkuti cha bei. Tayari wafugaji wameanza kulalamika kwamba ng'ombe mmoja pale gharama yake sasa hivi imefikia 14,000. Kwa taarifa nilizozipata wanasema kodi ya pato pale ni 2,000; kuna kodi ya muuzaji ambayo ni 5,500; kodi ya mnunuzi ni 7,500. Ukipiga hesabu hapo unapata shilingi 14,500, bado wafugaji wanaendelea kulalamika na wananchi wanaendelea kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye hili; huo mwongozo wa bei kama uko *uniform* kwa minada yote nchi nzima basi tuuone, uwe wazi na wananchi wale waweze kuupata nao waendelee kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea mara nyingi sana mgongano kati ya wafugaji na wakulima. Mgongano ambao unatokana na kugombea maji kwa sababu mkulima anahitaji maji na mfugaji anahitaji maji. Lakini naomba kupata ufafanuzi mahusiano yaliyopo kati ya wafugaji na wanyamapori?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo ni kwamba maeneo yale ambayo tembo walikuwa wanaishi ndiko sasa hivi ng'ombe wanaishi huko. Matokeo yake sasa sisi wakulima tunaendelea kuhangaika na hawa wanaoitwa wanyamapori. Lakini hivi juzi baada ya neema kubwa kutangazwa *TANAPA,* Pori letu la Akiba la Selous likagawiwa likapatiwa eneo la *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nikwambie kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji kwenye Vijiji vya Ndapata na Kimambi, leo yamechukuliwa na *TANAPA*. Matokeo yake wale wafugaji wamehama kutoka *TANAPA* wameachia lile eneo *TANAPA* wanakuja maeneo ya wakulima. Kwa hiyo, mgogoro wa wakulima na wafugaji unaendelea kushamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana palitokea mauaji, mwaka huu pametokea kujeruhiana…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka, muda umekwisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tusimamie jambo hili tuone kwamba wakulima na wafugaji wanakaa kwa salama na amani. Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa *Eng.* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo. Kwanza nitangulize pongezi kwao Wizara

nzima akiwemo Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Makatibu wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ambalo ninapenda kusema ni kwamba kwa Tanzania tumekuwa na *figures* za mifugo kila mwaka tunaongeza. Lakini ukijaribu kuangalia takwimu zetu sijui kama tunazo takwimu ambazo ni sahihi. Tunasema leo tuna ng'ombe milioni 36.6, mbuzi milioni 26.6 na kondoo milioni 9.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukijaribu kuangalia kwa idadi ya mifugo tulionao na mchango kwenye Pato la Taifa kidogo inafikirisha. Ni lazima tujiulize kama Taifa kwamba tunajali mifugo kama kitega uchumi au tunaona mifugo kama tatizo kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo hii tukijaribu kuangalia Nchi kama Ethiopia ina mifugo zaidi ya milioni 70, lakini hatusikii Serikali yao ikisema kwamba mifugo wamekuwa ni tatizo. Lakini sisi Tanzania tumewatangulizia wafugaji tunawaona kama tatizo kwenye nchi hii. Ukishamtangulizia mtu ukamuona kama tatizo, huwezi ukamsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tu-*change mentality* kama Serikali ili wafugaji tuwaone kama ni watu ambao nao kwenye nchi hii tunaweza kuwasaidia wakaongeza uchumi wetu na maisha yao yakaimarika. Lakini tukiwaona kama tatizo tutaendelea kuwalaumu kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la hereni, kaka yangu, Mheshimiwa Musukuma pale, alizungumza, lakini binafsi pia wananchi wangu kila siku wamekuwa wakilalamika kuhusiana na suala la hereni. Binafsi sioni kwamba ni kitu ambacho kitatusaidia kujua idadi ya mifugo Tanzania. Kinachotakiwa, kama tunataka kujua idadi ya mifugo tulionao

tuendeshe sensa kwa kila wilaya; tuna wakuu wa wilaya, tuna ma-*DAS,* tuna wakurugenzi, tuna watendaji wa vijiji, tuna watendaji wa kata, wafanye hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo tunakwenda tena kuwatoza Watanzania wenzetu, wafugaji, fedha kwa ajili ya kuhesabu mifugo yao. Sisi kama Serikali tuwekeze ili tupate kujua idadi ya mifugo na ili tuweze ku-*accrue economic bases* kutoka kwa wafugaji. Siyo tunawaona wafugaji kama tatizo. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Edward Kisau.

**TAARIFA**

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa kwamba idadi ya mifugo tayari inajulikana. Tumeambiwa hapa ni milioni 30. Kwa hiyo sasa sijui wanakwenda kufanya nini tena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa inapokelewa kwa mikono yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wafugaji ambao tumekuwa kwenye ufugaji kuanzia utotoni mpaka sasa hivi tunajua mifugo ni mali, ni dawa na ni kitanda kwetu. Kwa sababu mfugaji nalalia ngozi, nakula nyama, nakunywa maziwa. Nikiugua nachinja mifugo kwa ajili ya kuleta afya yangu ijirudie katika hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wengine Tanzania tumewaona wafugaji kama ni watu ambao hawafai. Hata kwenye vyombo vya habari tunawaona wafugaji kama ni watu ambao ni wa kutoka hapa kwenda pale kila siku, kuzunguka. Kwa nini wafugaji wanazunguka Tanzania nzima; ni kwa sababu tumewanyang'anya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia kwa Wilaya yangu ya Ngorongoro kabla ya eneo lile la Pori Tengefu kutengwa hatujawahi kuhamahama lakini mwaka huu itakuwa mara ya kwanza kwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kuhama kwenda kutafuta malisho kwa sababu tumewanyang'anya ardhi yao. Na ili tuone ni tatizo baada ya lile eneo la pori tengefu kutengwa, mifugo zaidi, ng'ombe 5,780 wamekamatwa kwenye lile eneo, na Serikali kuwatoza zaidi ya shilingi milioni 578. Kwa sababu hawana malisho itabidi waende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima kama Wizara, sijui kama ndugu yangu, Mheshimiwa Ulega, wafugaji Tanzania hii – ukimuona Waziri wa Maliasili ana wivu na tembo wake, sasa sijui wewe utakuwa na wivu na mifugo? Kwa sababu Watanzania wafugaji wanaumia kwenye hii nchi. Hatujawahi kumsikia Waziri wa Mifugo akizungumza hadharani na kukemea tabia ya wafugaji kukamatwa na kutozwa shilingi 100,000; hatujawahi kumsikia. Kwa nini tusisikie, na wewe umepewa na Rais Wizara hii usimamia uweze kuwatendea haki wafugaji wa nchi hii. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Sasa sijui kama kuna Wizara…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cherehani.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kweli Waziri wa Mifugo anatakiwa awaonee wivu wafugaji wake; wanakamatwa, wanatozwa faini, na wengine, mfano Yohana Mahona aliuziwa ng'ombe wake 1,221 na alishinda kesi Waziri hajatoa tamko. Lakini kuna Shabani Roya wa Ngorongoro, ng'ombe 170, alishinda kesi lakini Waziri hajatoa tamko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emmanuel, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa inayopokelewa kwa mikono yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe taarifa kwamba Desemba mwaka jana familia 27 walitaifishiwa ng'ombe 1,922 Ngorongoro. Mpaka leo familia hizo zimekuwa maskini. Kwa hiyo, niombe pamoja na masuala mengine tuwatafutie wafugaji wetu maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hawezi kukunyima fedha ukiwa na *big vision* lakini ukiwa Waziri unayekaa kila siku, kama walivyosema wengine, ni lazima ufikirie namna ya kuwakamua hawa wafugaji wa nchi hii. Tumechoka kuonewa kwenye nchi hii. Tunahitaji na sisi tuthaminike na tuweze kuchangia uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la chanjo; nashukuru umetuletea dozi 1,200 za *PPR*. Lakini toka mwezi Septemba mwaka jana mpaka sasa hivi hawajachanja mifugo kwa

sababu kwenye wilaya zetu wewe unapeleka chanjo lakini huna fedha za operesheni kwa ajili ya kufanikisha. Sasa sijui chanjo zitakwenda kwa mifugo yenyewe? Tunahitaji gari na fedha kwa ajili ya wataalamu kwenda kuchanja mifugo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wamechukua muda wangu kwa taarifa, naomba uniongezee.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa, taarifa ni sehemu ya mjadala.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunashukuru. Mheshimiwa *Eng.* Samweli Xaday Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng.* Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie sekta hii muhimu ya mifugo na nianze kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano ambao walikuwa wametupa kwenye Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa sababu ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kusema kwamba sekta ya mifugo na uvuvi ni sekta muhimu ya uzalishaji kwenye nchi yetu. Na wenzangu pia

wamesema Waziri anapaswa kuonesha wivu na suala la mifugo kama Mawaziri wengine wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili, mifugo imekuwa ikikamatwa hovyo na wafugaji kutozwa gharama kubwa ambayo wakati mwingine wengine wamefilisiwa. Wengi wamekuwa wakizunguka kwenye *corridors* za Wizara kwa sababu mifugo wao wametaifishwa, lakini hali ya wafugaji nchi hii ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wamelazimika kuhama sehemu moja kwenda nyingine sababu kubwa ni uhaba wa malisho na maji. Na wanapohama tunawashangaa kwa nini wanahama, lakini nikwambie tu Mheshimiwa Waziri, kwa sisi wafugaji unaporudi nyumbani jioni ng'ombe hawajashiba ni sawasawa na mama ambaye watoto wake wana njaa, wewe hupati usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo lazima lichukuliwe kwa uzito mpana kwamba suala la malisho kwa mifugo nchi hii ni suala kubwa na lazima tufanye kazi ya ziada. Nimekusikia ukisema kwamba utahakikisha ranchi zote zitatumika kutengeneza malisho kwa mifugo yetu. Lakini sioni kama kuna muujiza utakaotokea Mheshimiwa Waziri, fedha zilizoongezwa kwenye bajeti hii tunayokwenda kuipitisha ni fedha kidogo mno. Hata utekelezaji wa bajeti ya 2023/2024 fedha zilizotolewa ni kidogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiangalia sekta ya Kilimo, Fungu 99, iko kwenye asilimia kama 49 tu. Na ninaomba nitaje vitu vichache ambavyo vimetekelezwa. Vitu hivi hata kama vikitekelezwa kwenye Jimbo la Hanang pekee hakutaleta mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilivyotekelezwa; ujenzi wa Bwawa la Kimambi lita milioni 95; ujenzi wa Bwawa la Matekwe, lita milioni 102 – na bahati nzuri hili bwawa mimi nimelitembelea na Kamati. Ni bwawa dogo ambalo hata kuhudumia kijiji kimoja cha wafugaji hakitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekarabati Bwawa pale Mwanga, Itigi lita milioni 54; kisima kirefu kimoja na mabwawa mengine 11. Kwa mwendo huu wa kibajeti na fedha hazitoki zote, kwa hakika kazi inayofanyika ni ndogo sana, haitawasaidia wafugaji wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye Wilaya yangu ya Hanang, kwanza nishukuru tumepata mbegu 8,000 za kuhimirisha mifugo yetu ili tuweze kuiboresha; mpaka sasa tumeweza kuchukua tu mbegu 300. Changamoto kubwa ni sehemu ya kutunzia mbegu hizo ili ziwafikie wafugaji, haipo. Vifaa vilivyopo ni vidogo havitoshelezi hata kidogo; lakini kwa sababu hizi zinaenda kwa wafugaji ambao hiyo taaluma hawajaelimishwa vya kutosha, wanachajiwa shilingi 25,000. Elfu ishirini na tano ni sawa sawa na bei ya mbuzi, kwamba hii ni kumpandisha ng'ombe uuze mbuzi. Kwa wafugaji hii ni gharama kubwa na haiwezekani, kwa sababu hawana elimu hiyo. La muhimu kwanza Serikali iwezeshe mifugo yao ihimirishwe bure ili wengine wakajifunze kule, wakijifunza baadae watakuwa tayari kugharamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande wa watumishi, tunao watumishi wachache. Wilaya ya Hanang' yenye kata 33, vijiji 96 tuna watumishi 17 tu na tuna pikipiki mbili tu. Sasa ni namna gani utawafikia wafugaji? Mheshimiwa Waziri lazima achukue hatua ya ziada kuwakaribia wafugaji. Wafugaji wanahangaika sana. Wafugaji wetu wanapaswa kuelimishwa, watu wanaacha ufugaji sasa hivi wengi wanakimbilia kwenye upande wa kilimo, kwa sababu ukienda kwenye kilimo unajua

kabisa kwenye hekari moja ukilima unapata magunia mangapi utafaidika kiasi gani, kwenye mifugo hamuwaelezi mambo hayo. Wafugaji wangu wa Gehandu, Mureru na Mulbadaw, wanataka elimu hiyo iwasogelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuwa Naibu Waziri muda mrefu kwenye Wizara hiyo hajatembelea Jimbo la Hanang. Hakuna Waziri aliyekuja jimbo la Hanang' akaongea na wale wafugaji wakapata ile elimu inayotakiwa. Ninaomba eneo hilo muwakaribie wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nigusie kidogo eneo la uvuvi. Sisi tunategemea ziwa Bassotu kwa ajili ya Uvuvi. Ziwa lile limeanza kujaa mchanga, sasa waangalie namna ya kulikarabati. Zaidi ya hapo kuna mwalo pale Mulbadaw tumeomba muda mrefu lile mwalo lifunguliwe wananchi waweze kufanya shughuri za uvuvi. Ninaomba wakati anasimama hapa awaelekeze watu wake ndani ya Wilaya kwa sababu nimeona wakiyumba yumba bila kufanya kazi hiyo. Wananchi wanasubiri wakafanye kazi maandalizi ya awali yameshafanyika, ule mwalo ukafunguliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna bwawa la Gidahababieg, tathmini imefanyika mara nyingi. Ungana na watu wa idara ya maji, watu wa kilimo pale tujenge bwawa ambalo litawasaidia watu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji lakini litasaidia kwa ajili ya kunyweshea mifugo; na pia pale tunaweza kupata mboga ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama muda wangu unaanza kukimbia. Sekta ya mifugo; Jimbo la Hanang ni jimbo la wafugaji, Hanang wanahitaji kusogelewa. Tunaomba tuone miguu yenu ndani ya Jimbo la Hanang'; hakuna chochote cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi inafanyika kwenye Jimbo la Hanang'

ili wafugaji wangu wale waone Serikali iko nao na inafanya kazi ya kuwahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hhayuma. Mheshimiwa Chilewesa atafuatiwa na Mheshimiwa Kasinge.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi pia na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kushuika nafasi hii. Naamini nyie ni vijana, Mheshimiwa Rais anaelewa kazi ya ufugaji iko vijijini na sio vijijini tu, maporini na ndiyo maana amewateua nyie vijana ili mweze kufika huko kuonana na wafugaji. Baada ya kuyasema haya; mimi ni Mjumbe wa Kamati kwa hiyo kuna mambo ambayo tuliyaona hasa kwenye ziara na nilikuwa natamani kuishauri Wizara na ikiwezekana Bunge tuweze kusaidia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea miradi, hasa ule mradi wa mabwawa ya kunyweshea mifugo. Tulitembelea Bwawa la Matekwe Nachingwea. Mmpaka ufike Nachingwea kwanza ni safari ndefu sana ambayo kwa kweli unafika umechoka, lakini kutoka Nachingwea penyewe mjini kwenda huko Matekwe kwenye hilo bwawa ni kilometa 154. Kwa hiyo unaweza uka *imagine* ni kiasi gani Kamati iliingia ndani na iliingia ndani kweli kweli maporini. Kwa nini nayasema haya, jana wakati nawasilisha taarifa ya Kamati, nadhani mtakua mlisikia nyote, kwamba thamani ya bwawa tuliyoikuta kule ilikuwa haiendani na uwekezaji ambao tuliambiwa. Sababu

kubwa ambayo tuliiona kama Kamati; *engineers* wapo wawili, sijui watatu nchi hii, wazunguke wao kushughulikia miradi yote hii ni, ngumu kufanya hicho kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni mashahidi, tunao ma-*engineers* kwenye majimbo yetu au Wilayani lakini bado hawajaweza kufika sehemu zote hizo, sasa *Engineer* mmoja kuweza ku *manage* miradi ambayo inapitishwa na Wizara hapa ni ngumu, na ndiyo maana tukaja na pendekezo kama Kamati jana. Kwamba, tunaomba iwekwe taasisi maalumu inayo-*deal* na mifugo, na pia iwekwe taasisi maalumu inayo-*deal* na uvuvi, sawa na ambavyo tumeanzisha Wakala wa Umeme Vijijini, tumeanzisha wakala wa barabara na vitu vingine kama hivyo; tuanzishe wakala atakay-*deal* na mifugo na atakaye-*deal* na uvuvi, itatusaidia miradi ile ambayo tunaipeleka huko vijijini tuweze kuwa na *monitoring*. Ni aibu kupeleka mradi wa milioni 405 mna uweka porini baada ya hapo mmeaga na salama ndio mmeondoka na mradi ukishazinduliwa umekabidhiwa kwa wananchi umepotea. Kesho hata kama kuna tatizo linalotokea hakuna mtaalam kule. Kwa hiyo mradi mnauweka baada ya muda *value for money* haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unajenga mradi wa maji hata wa milioni 20, milioni 30 kuna watu wanaufanyia *monitoring* na ma *engineer* wapo. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba taasisi maalumu ya ku-*deal* na mifugo na uvuvi iundwe ndani ya Bunge hili iweze kusaidia fedha hizi zinazopelekwa huko. Ni mabilioni ya shilingi yanapelekwa lakini hayaonekani thamani yake kwa sababu hakuna anayefatilia. Mwaka mwingine unaofuata Waziri anakuja na kitu kipya, tukishapitisha unaofuata anakuja na kitu kingine, hivyo hivyo. Kwa hiyo fedha hii inaenda lakini hakuna anayeonekana kuisemea. Nilikuwa nataka niliweka hilo.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra kuna taarifa naomba…

**TAARIFA**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwamba maeneo haya sio yapo mbali tuna mjini kama alivyotolea mfano wa Jimbo la Nachingwea ambako mimi ni Mbunge bali hata *monitoring* yake kama halmashauri hatuelewi chochote kwa sababu Mkandarasi anatoka moja kwa moja Wizarani na kama halmashauri hatuna namna ya kwenda kumsimamia na kukagua huo mradi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra, taarifa hiyo unaipokea.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, ni nyama tosha kabisa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niachane na huko; cha kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Alhamisi alitoa hotuba hapa yenye mwelekeo mzuri; lakini kama Wabunge wengine walivyosema. Wizara ya Mifugo nimesema ninyi ni vijana tunaomba mtusaidie. Kuna kipindi tunagombana na watu wa maliasili hapa ninyi mkiwa mmekaa kimya; *we want you to speak out.* Kwa sababu Waziri wa Maliasili amekuwa na wivu mkubwa hapa. Unamuuliza kati ya tembo na binadamu anayeuawa mwenye thamani ni nani anawaambia wanamfuata tembo, unaweza ukaona; lakini nyie wafugaji wetu wananyanyasika kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nina ushahidi hapa kwenye simu ninaweza nikatoa. Juzi Alhamisi Mheshimiwa Waziri Mkuu

alisimama, hapa ameelezea *reconciliation* ambayo inabidi ifanyike na akasema hata haya mambo sasa ya watu kukaa karibu na hifadhi wanachukua wananyama na wakati mwingine wanawaingiza ndani wanasema wamekamatwa, Jumamosi mwenyekiti wangu wa halmashauri, na *message* ninazo hapa, huyu si mtu mdogo ndiye anayesimamia halmashauri yetu, na haina hati chafu. Kwenye kata yake akanitumia ujumbe wafugaji wawili, mmoja katozwa milioni tano mwingine katozwa milioni 11 hawajapelekwa sehemu, pesa imetolewa *cash* hakuna risiti hakuna; wafugaji wananyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili baada ya Waziri Mkuu kuhutubia Bunge mambo yanafanyika kule sisi tukiwa hapa. Kwa hiyo tunaomba Wizara ya Mifugo mchukue hatua vinginevyo sasa utakuja kuanza ugomvi kule wale wahifadhi na wakulima na sisi sasa tutaingilia kati. Lakini tumechoka, hatuwezi kuja hapa kila siku wafugaji wetu wananyanyaswa kila ng’ombe shilingi laki moja Wizara iko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tunaomba mtusaidie, wafugaji ni Watanzania. Ni lazima, kama mnasema Pato la Tanzania linaingia kwa asilimia 7.8 hawa watu hii nchi ni yao, lazima ifikie hatua na wao waone thamani ya kuwa hapa, wasinyanyaswe tuna watu. Kwa hiyo tunaomba hilo mlione mje na *strategy* nzuri ya kutusaidia ili wafugaji ambao wanafuga ng’ombe kule na wao wajione kama Watanzania. Nimelisema mara nyingi hili suala sasa inafikia *stage* tunachoka, tunaomba hilo mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nishukuru pia na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, nadhani tumeona wote video na hotuba jana kipindi anapita kwenye mabanda. Ameelekeza suala la utambuzi wa wanyama lianze upya, hususan suala la herein, ameelezea jana pale. Kwa hiyo kama Waziri Mkuu tumepokea lakini tunachoomba tunaomba Wizara

tuwashauri. Wafugaji hawa mlikuja na habari ya chapa ng'ombe wakachapishwa ng'ombe wakaumia ngozi matokeo yake hatukuona kilichoendelea, na baada ya miaka mitatu mnahamisha mnapeleka kwenye heleni sasa mimi nilikuwa na ushauri…

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra kuna taarifa

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mngeniacha nichangie, muda umeisha.

**MWENYEKITI: …**kutoka kwa Nusrat Shaaban Hanje.

**TAARIFA**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kuhusiana na suala la *identification* ya mifugo, kwamba si suala la utashi wa viongozi kwa sababu ni sheria ambayo ilitungwa na Bunge hili, Sheria ya Usajili, ufatiliaji na utambuzi wa mifugo mwaka 2010, ambapo kifungu cha saba, cha nane mpaka cha tisa vina elezea *devices*. Kwa hiyo ni jambo la kisheria si jambo la utashi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa unaipokea?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea ila sasa naomba unilindie muda wangu maana na mimi hapa nahesabu. Taarifa nazipokea jamani tungevumiliana tumalize maana muda unaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoomba, cha kwanza tuna ranchi zetu za taifa, kwenye zile *ranch* kuna watu wanapewa nafasi ambao si wafugaji. Kwa hiyo tunachoomba,

kwa kuanzia, mifugo yote ambayo iko kwenye *ranch* za taifa, achana na hawa wafugaji ambao wanafuga wao kama wao. Wewe umekodisha mtu anakwambia ana mifugo kwenye eneo lako; mifugo ni mingapi hatujui anamifugo mingapi. Kwa hiyo tunachoomba *process* ya kuweka heleni ianze na ng'ombe wote walioko kwenye Ranchi ya Taifa, tuwajue. Tukishaanza na ng'ombe walioko kwenye Ranchi ya Taifa hapa ndipo tutakapoujua ukweli kwa sababu kuna watu wameshikiria maeneo kwenye *ranch* na hawana ng'ombe pale wanatukodisha sisi; hilo ni la kwanza ambalo watakuwa wametusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kwa wafugaji wale ambao dawa ni yake, malisho ni yake kila kitu ni chake hamjawatengea chochote wanapouza ng'ombe si wanatozwa kwenye minada, hawa watu wananunua madawa tunapata, hebu tufumbeni macho basi wafugaji hao muwasaidie kwa kwenda kuvalisha heleni. *First process* mfanye nyie *the second one* itakapotokea itakuwa sasa kila ng'ombe anayezaliwa anazaliwa mfugaji anaruhusiwa kulipia heleni; hiyo itaweza kutusaidia. Lakini leo ukimwambia mtu mwenye ng'ombe 200, 300 hadi 400 akalipe hereni kwa mkupuo itawaumiza sana wafugaji. Kwa hiyo tuombe, walio kwenye *ranch* kwa sababu ni wakodishaji wenu cha kwanza mtakijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, Wizara walituahidi habari ya malisho. Kwamba kuna majani maalum wanataka kuja kuotesha nchi nzima na yale majani yatatusaidia hasa upande wa kiangazi kuzuia ng'ombe wasitoke sehemu moja kwenda sehemu nyingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra ahsante sana.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie muda wangu umeliwa sana dakika moja, nimalizie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sekundee moja.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay,* sekunde haitatosha. Sasa Mheshimiwa Waziri tunakuomba fanya *identification* ya maeneo na hasa uanzie kwangu kwa sababu kuna mifugo mingi ili tutengewe maeneo na yale majani yaoteshwe, wananchi wa Biharamulo waweze kupata majani wakati wa kiangazi wasihangaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge kuwa mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote nianze kwa kuwapongeza sana mawaziri wote wawili, kwa maana ya Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde, ndugu zangu hawa, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza sekta mbili hizi za Mifugo na Uvuvi. Mimi kwa upande wangu, kama mimi, binafsi sina shaka kabisa na Waheshimiwa Mawaziri hawa lakini pili niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza kile ambacho sisi Wabunge tulipitisha katika Bunge lako kama mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha ujenzi wa bandari ya uvuvi pale Kilwa Masoko, nitoe tu taarifa kwamba ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambayo mkataba wake ulisainiwa mwaka

jana mwezi wa sita unaendelea kwa kazi kubwa sana pale Kilwa Masoko; pongezi sana kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Wanakilwa kwa ujumla wao, lakini wana. Kilwa Masoko kwa upekee wanaomba sana itakapofikia hatua yoyote ile ama ya kuweka jiwe la msingi au kuzindua bandari hii Mheshimiwa Waziri tunaomba ushauri mamlaka husika, Mheshimiwa Rais aje afanye kazi hiyo pale wananchi waje wampe pongezi wakiwa live pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi pale Kilwa Masoko kulikuwa na changamoto ya wapiga kura wangu 54 kutolipwa fidia. Niliwahi kuzungumza katika Mkutano wa Nane wa Bunge hili, lakini pia niliwahi kuzungumza katika Kikao cha Pili cha Mkutano huu wa Kumi na Moja katika Bunge hili. Vilevile tarehe nne mwezi wanne nilizungumza na Mheshimiwa Waziri Ulega ofisini kwake kuhusiana na wananchi 54 ambao bado hawajalipwa fidia; tuliweka sawa mambo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa shukrani sana kwa Serikali lakini kupitia Wizara ya Uvuvi na kupitia kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana husika, Mheshimiwa Ulega. Ninayo furaha kumjulisha kwamba wananchi wangu 54 wakiwemo Fatma Musa Mjaka, Bibi Mwanawetu Zarafi, Mwanafadhila Sudi pamoja na Bwana Said Bungara a.k. a Bwege tayari wameshalipwa fidia ya bilioni 8.5. Sasa mambo ni mazuri hakuna tena mgogoro kati ya wananchi wangu na Serikali ya Awamu ya Sita. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili katika mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano, lakini kwa upekee wake katika bajeti ya Wizara hii mwaka jana tulipitisha kwamba tutajenga masoko ya samaki Kilwa Kivinje pamoja na Kilwa Somanga. Nielezee kwa masikitiko tu kwamba mpaka

tunaelekea mwishoni mwa mwaka huu, sasa hivi tuko robo ya nne tumeianza hii hatujapata fedha yoyote kwa ajili ya ujenzi wa masoko ya samaki, Kilwa Kivinje na pale Kilwa Samanga. Nitumie fursa hii kuikumbusha Wizara sisi wana-Kilwa Kivinje na wana-Kilwa Somanga bado tunahitaji masoko haya kutokana na uzalishaji mkubwa wa samaki katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nielezee mambo ambayo nimeyazungumza kupitia Wizara hii na kupitia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu mara kadhaa hapa Bungeni kuhusiana na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 20202 ambazo zimekuwa kikwazo kwa wavuvi wetu. Niliwahi kuuliza swali la msingi hapa ili kufahamu ni lini Wizara ya Mifugo na Uvuvi itabadilisha kanuni hizi; Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana sasa hivi Mheshimiwa Ulega wakati huo akiwa Naibu Waziri alijibu swali hili kwamba muda si mrefu kanuni hizi zinakwenda kubadilishwa. Kwa masikitiko niseme kwamba kilichofanywa na Wizara ni kubadilisha kanuni za tozo peke yake lakini kanuni za usimamizi wa masuala ya Bahari ambazo ni kikwazo kwa wavuvi wetu bado hazijabadilishwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba wakati anajibu vile Mheshimiwa Ulega alikuwa ni Naibu Waziri, sasa ni Waziri kamili; nenda kabadilishe kanuni hizi kwa maslahi ya wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili bajeti ya mwaka jana ya Wizara hii tulipitisha hapa kwamba Wizara hii itakwenda kununua boti 320 kwa ajili ya kukopesha wavuvi wetu, lakini taarifa ya hotuba ya Waziri hapa leo anatuambia mpaka sasa hivi boti zilizogawiwa ni 150 tu. Hizi zingine zaidi ya 150 zinasubiri nini kupelekwa kwa wavuvi wetu katika maeneo mbalimbali katika ukanda wetu wa Bahari lakini pia katika ukanda wa maziwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kuona wavuvi wetu wasotee kule Mkuranga kwa Mheshimiwa Ulega wanapata boti hizi. Tunapenda kuona wavuvi wetu wa Mafya kule Bwajuu kwa Mheshimiwa Kipanga wanapata boti hizi, tunapenda kuona wavuvi wetu wa Msanga Mkuu kule Mtwara kwa Mheshimiwa Mtenga wanapata bodi hizi. Tunapenda kuona wavuvi wetu wa maeneo ya Pwani, Kibiti, Tanga, Dar es Salaam na kwenye maziwa yetu wanapata boti hizi; ndio utakaokuwa ukombozi pekee kwa wavuvi wetu kuinua uchumi katika sekta hii ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie suala la migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Migogoro ya ardhi ya wakulima na wafugaji hili lipo ndani ya Wizara hii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiratibu vema na Wizara zingine ikiwemo *TAMISEMI,* migogoro hii wanaimaliza. Nieleze tu kwamba juhudi kadhaa zimefanyika na Serikali lakini migogoro hii bado ipo. Nitoe tu mfano hapa, mimi katika jimbo langu la Kilwa Kusini bado migogoro hii bado ipo, ukienda Kikole migogoro ipo, ukienda Nanjirinji migogoro ipo, ukienda Kilanjelanje migogoro bado ipo; lakini hata jimbo jirani kwa jirani yangu pale kwa Mheshimiwa Ndulane kule Kilwa Kaskazini ukienda Nginjo, Mitole, Miguruwe, Kandalale bado migogoro ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tatizo ni nini? Wakati utaratibu wa kupeleka mifugo unafanyika katika maeneo yote mikoa ya kusini; utaratibu na makubaliano ulikuwa kwamba Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ikaweke maandalizi ya kupokea hawa wafugaji, lakini mandalizi hayo hayajafanyika, kulikoni? Nitumie fursa hii kuikumbusha Serikali hebu wakaweke utaratibu wa kupokea hii mifugo ili wafugaji waishi vizuri, malambo yawepo, majosho yawepo na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ikomeshwe na imalizwe kabisa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya hapo naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasinge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa ratiba yetu ya mchana wa leo. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia na tuna amini wenzetu upande wa Serikali wamesikia michango, maono, mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge na watayafanyia kazi. Baada ya kusema hayo machache nasitisha shughuri za Bunge hadi saa kumi na moja kamili alasiri.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza

mchana huu. Kwanza kabisa niipongeze na kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais wetu na Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi unaendelea vizuri, wananchi hasa wa Jimbo langu la Mwanga wanafurahia kazi za maendeleo zinazoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu kwa dhamana kubwa hii waliyopewa, hotuba ya Mheshimiwa Waziri toka jana asubuhi ilileta hamasa kubwa sana na hatuna sababu kwa nini tusipitishe bajeti yake. Naunga mkono hoja kwa sababu nataka kuona hiyo hamasa aliyotupa ikiingia kwenye vitendo.

Mheshimiwa Spika, niliangalia kwa haraka tu jukumu la Wizara hii. Pamoja na mambo mengine, lakini kuna *statement* pale kwamba ni kusimamia na kuendeleza Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa ujumla, kukuza uchumi na kupunguza umaskini na kuyafikia malengo ya *millennium.* Katika upana huo ni kwamba Wizara hii inagusa maisha ya kila mtu ya kila siku. Naamini kabisa zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania aidha wanakula nyama au samaki, mayai au maziwa na ikibidi sana basi hata wanatumia mbolea kulima mchicha na kula mazao ambayo yanatokana na mbolea za mifugo hii. Kwa hiyo ni sekta ambayo imegusa maisha ya kila siku ya watu. Kwa hiyo usimamizi wake ni jambo ambalo ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mwanga tuna ufugaji wa aina mbili ukizungumzia habari ya ng'ombe na mbuzi. Maeneo ya milimani wanafugia ndani *zero grazing,* tunazalisha zaidi maziwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alipokuwa Naibu niliwahi kumvuta koti siku moja, nikamwambia kwamba kule kwetu tunahitaji sana masuala ya kukusanya maziwa pamoja na uhamilishaji. Sasa amekuwa *full* Waziri

tunaomba atukumbuke hasa kwenye Miradi yake ya *Heifer* ili tuendelee kuzalisha maziwa kule milimani.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya tambarare karibu kata kumi, zote zina ufugaji huu wa huria wa kuchunga. Ni jamii za Wamasai pamoja na makabila mengine, lakini kwa kweli tumesahaulika sana kwenye upande wa miundombinu ya ufugaji kama majosho, malambo na hata madawa ya mifugo. Kama sio Shirika la *WWF* kutukumbuka mara kwa mara nadhani wale wafugaji wangu Mwanga wangekuwa wameshakimbia. Kwa hiyo, tunaomba Wizara itukumbuke katika huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, pia tuna mnada wa kimataifa pale wa mifugo kwenye Kata ya Mgagao. Katika mnada ule wanakuja watu kutoka Mombasa na Comoro kuja kuchukua mifugo pale, lakini miundombinu ya mnada ule bado sio rafiki. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwekeze katika mnada ule wa Kimataifa wa Mgagao. Pia eneo hili la Mgagao linafaa sana kwa Kiwanda cha Kusindika Nyama, kwa sababu tuko katikati tunapokea mifugo kutoka Mwanga yenyewe, Simanjiro na hata kutoka maeneo ya Mkoa wa Tanga na *airport* ya *KIA* haiko mbali, Bandari ya Tanga iko karibu pia, pamoja na mpaka wa Kenya pale kwa ajili ya biashara. Kwa hiyo, ni eneo la kimkakati, tunaomba pia tukumbukwe.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye Sekta ya Uvuvi, Jimbo la Mwanga lina rasilimali kubwa mbili za uvuvi. Kwanza ni Ziwa Jipe ambalo liko mpaka mwa Kenya. Ziwa hili kwa muda mrefu sana uvuvi sasa unakaribia kufa kwa sababu ya suala la magugu maji. Serikali karibu miaka 20 sasa imekuwa ikitoa ahadi ya kuondoa magugu maji pale. Mara ya mwisho mwaka 2021 alikuja Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira akatuahidi pale kwamba fedha zipo na kwamba magugu maji yataondolewa, lakini mpaka leo hakuna kitu na

nimeendelea kufuatilia kila siku lakini inaonekana ahadi hii haitimii wakati ilitolewa mbele ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ni upande wa mifugo lakini ukiangalia jukumu la Wizara yake ni pamoja na kusimamia hivi vyanzo. Kwa hiyo, tunaomba kauli ya Serikali kwamba wanaliachaachaje Ziwa lile la Jipe life wakati ambapo lina uvuvi mzuri wa samaki aina ya *tilapia* na liko mpakani mwa Kenya? Tunaomba Ziwa lile liangaliwe kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, ukija chanzo kingine ni Bwawa la Nyumba ya Mungu. Bwawa hili asilimia 61 iko upande wa Mwanga na asilimia zinazobakia ni Simanjiro na Moshi Vijijini. Watu wa pale wanategemea uvuvi peke yake kama njia yao ya Maisha, kwa sababu lile eneo halina hata mvua ya kutosha, hivyo, hakuna kilimo pale. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa uvuvi wa pale hauendi vizuri, samaki wale hawakui na kwa sababu samaki hawakui kila Mvuvi sasa anaonekana ni mvuvi haramu. Serikali imepambana sana na uvuvi haramu lakini bado mambo pale ni magumu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna taarifa kwamba Wakuu wetu wa Wilaya hizi tatu wameandika barua Wizarani kuomba kufunga lile bwawa. Sasa kufunga bwawa tafsiri yake ni kwamba uvuvi haramu ndio pekee unaosababisha kutokukua kwa wale samaki. Sasa nilizungumza na mtaalam mmoja ambaye hata Wizara inamtambua kwa umahiri wake akaniambia wale samaki aina ya *tilapia* wameumbiwa namna ya kujilinda wasipotee.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, panapokuwa na tishio fulani hivi la kimazingira kama ni mabomu ya uvuvi haramu au ni maji kupungua au ni maji kuchafuka huwa wana *mature* ghafla ili wasipotee wanaishia hapo hapo walipo. Kwa hiyo, ndio maana

wote wanakuwa wadogo. Nilipokwenda jimboni mara ya mwisho kwenye *weekend* hii ya Mei Mosi, watu wananinonesha wanasema Mheshimiwa angalia hawa samaki ni wadogo lakini wana mayai, tena wana watoto na wajukuu tayari lakini ndio wamefikia hapo. Ndio maana kila mvuvi pale anaonekana kuwa ni mvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema kwa vile hatujaona kama wenzetu wa *Lake* Tanganyika, hatujapata taarifa kwamba kwa nini Serikali inaona ni uvuvi haramu tu na sio sababu zingine za kimazingira zinazofanya wale samaki wengine wasikue? Basi kama ni hivyo ina maana huu ufungaji ni ufungaji wa majaribio *(experimental closure)*. Sasa kama ni *experimental closure,* tunaomba basi wale wananchi wapatiwe mbadala.

Mheshimiwa Spika, tumesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna fedha nyingi kwa ajili ya ufugaji wa samaki. Naomba wakati tunafikiria kufunga Bwawa la Nyumba ya Mungu, basi wale wananchi wapatiwe hii miradi ya ufugaji wa samaki. Halmashauri ya Mwanga imewekeza ikajenga Soko la Samaki lenye mpaka jengo la chakula barafu. Sasa hatuwezi kuacha ile *facility* ikakaa hivi hivi, tufuge samaki ili tuendelee kutumia.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kujenga lile Soko la Samaki na jengo la chakula barafu ni kwamba samaki wauziwe mahali pamoja ili tuweze ku-*control* vizuri masuala ya afya, masuala ya ushuru wa Serikali na yule mtu atakayekuja sokoni na samaki wake wasiuzike aweze kuwaweka kwenye chakula barafu wawe *fresh* kesho asubuhi. Pia yule anayetaka kusafirisha basi tunamtengenezea wanakaa kwenye *temperature* inayofaa ili aweze kusafirisha. Kwa hiyo hatutarajii kabisa na wala hatutamani tuone kabisa lile bwawa linafungwa na wale watu

wakose chakula, wakose ajira halafu na hii *facility* kubwa ambayo tumeweka isipate matumizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya Bajeti hii twende akaangalie eneo lile la Lang'ata jinsi ambavyo halmashauri imewekeza kujenga hizi *facility* na jinsi ambavyo watu wote wanategemea maisha yao pale kwenye bwawa, halafu ndio atuambie kwamba tunalifunga kwa utaratibu gani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad na Mheshimiwa Luhaga Jonhson Mpina ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji kwenye hotuba ya Waziri. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jitihada kubwa sana ambayo anaifanya pamoja na Naibu wake na Wasaidizi wake kwenye Ofisi, wanafanya kazi nzuri lakini yapo ambayo tunahitaji kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze kwenye eneo la mifugo. Kwenye eneo la mifugo, Serikali ina wajibu wa kuimarisha *Ranch* ambazo zitasaidia wakulima au wafugaji wadogo wadogo waweze kupeleka mifugo kwenye hizo *Ranch* na *Ranch* hizo zitumike kwa ajili ya kuwa kama soko ambalo litakusanya mifugo ya wafugaji wadogo wadogo ili mifugo ikinenepeshwa wao wanaiuza kwenye masoko ya nje. Hili litasaidia sana kukuza sekta hii ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufugaji wetu asilimia kubwa wamekuwa wachungaji kwa sababu ya kukosa huduma zile za

msingi. Hawana malisho ya kutosha, hawana malambo na majosho. Kwa hiyo, wafugaji wanalazimika kutafuta malisho na kutafuta huduma zile ambazo zinaweza zikasaidia mifugo iweze kuishi. Kwa hiyo, niombe Serikali iimarishe eneo hili ili kuwasaidia hawa wafugaji wetu ambao maisha yao kweli ni ya kuhamahama kwa sababu wanahitaji kupeleka mifugo ili iweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nizungumzie suala la uvuvi. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia sana hoja au mapendekezo ya Serikali juu ya kufunga Ziwa Tanganyika. Mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao wapigakura wetu wapo kwenye eneo hilo la Ziwa Tanganyika. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, endapo kama zoezi hili litakuwa limekubalika na likatekelezwa, ukanda mzima wa Ziwa Tanganyika kuanzia Kasanga hadi Kigoma tutatengeneza wezi wengi na majambazi wengi, kwa sababu maisha yote ya wananchi wa ukanda wa mwambao wa Ziwa Tanganyika, yanategemea suala zima la uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwaeleze tu ule ukweli, Serikali haijafanya utafiti mzuri. Ziwa Tanganyika ni Ziwa ambalo linajifunga lenyewe kulingana na jiografia ilivyo. Ziwa Tanganyika, muda mchache sana wanatumia wavuvi kufanya shughuli za uvuvi kwenye Ziwa hilo. Tunayo miezi ambayo Ziwa Tanganyika haliwezi kutoa hata samaki wa mboga, kwa sababu Ziwa lile lina kina kirefu na ndio Ziwa kubwa ambalo lina kina kirefu karibu mita 1500 ambazo kina chake kinaenda chini. Kwa hiyo, kuna kipindi samaki wanakwenda chini wanakimbia ubaridi wa huku juu. Kipindi hicho wavuvi huwa hawapati kitu chochote. Sasa sioni sababu Serikali inapokuja na mawazo ya kulifunga hili Ziwa kwa sababu jiografia na uhalisia ulivyo Ziwa huwa linajifunga lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie jambo lingine la pili kwenye eneo hili la uvuvi wa Ziwa Tanganyika. Uvuvi haramu ndio chanzo cha mawazo ya kufikiria kwamba Ziwa lifungwe, lakini kuna mambo ambayo yanafanywa Serikali wanashindwa kusimamia wao wenyewe. Uvuvi haramu chanzo chake ni kuleta nyavu zile ambazo zimekatazwa na Serikali. Pia inanisikitisha sana kama nchi ya Zambia, Congo na Burundi waliafikiana kulifunga hili Ziwa wakati wao wanaruhusu nyavu hizo haramu zinauzwa bila kuwa na shida yoyote. Mfano halisi, nenda pale mpakani Tunduma, ukivuka tu upande wa pili unakuta zile nyavu zipo zinauzwa wala hazina shida ya aina yoyote, marufuku iko huku huku nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wavuvi wanaovua na nyavu hizo haramu wanatoka Nchi za *DRC* Congo, Burundi na Zambia. Mvuvi wa Tanzania hawezi kwenda kuvua kwenye eneo la Ziwa linalomilikiwa na Zambia wala Congo wala Burundi. Asilimia kubwa ya wavuvi wanaoendesha shughuli za uvuvi haramu ni wenzetu wa kutoka nchi za jirani. Kwa hiyo, naomba hili Mheshimiwa Waziri alielewe. Mbaya zaidi Maafisa wetu wa Serikali ambao ndio wenye jukumu la kulinda rasilimali za kwetu, wao ndio wamekuwa wahusika wakubwa wa kuwalinda na kuwahifadhi hao wanaovua kwa njia ya haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutamsaidia Mheshimiwa Waziri, akituhitaji na bahati nzuri tumeona kuna mwaliko ambao amewaalika Wabunge wote wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Tutamweleza uhalisia jinsi ulivyo. Maafisa wao wanatumika. Mfano, tunapopakana Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma, kuna eneo ambalo wavuvi wa nchi zote hizo nilizokutajia hasa DRC Congo na Burundi wapo pale katikati na Maafisa wao wanakwenda kuchukua michango ambayo inawaruhusu waweze kuendeleza shughuli za uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo zile nyavu haramu ambazo ni hatarishi kwa maisha ya viumbe hai kwenye maeneo ya Ziwa. Hizo nyavu zinatumika na Maafisa wa Wizara wanazikuta na hawachukui hatua ya aina yoyote. Kwa hiyo, sioni sababu ya Mheshimiwa Waziri kuungana na tamko ambalo wamekubaliana kwamba tulifunge hili Ziwa, kwa sababu uzembe upo Serikalini. Kwa hiyo, naomba hili Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hawezi kufunga Ziwa hajaweka vitendea kazi. Uvuvi ule wa kisasa ambao ungepelekwa kwenye eneo la Ziwa Tanganyika hajawapelekea, dhana zote wamepeleka Ziwa Victoria. Kwa sababu, kule kama ni tamko la kufunga Ziwa wangepeleka kule kwa sababu walishaandaa utaratibu. Kwa Ziwa Tanganyika hawajapeleka kitu chochote kile. Kwa hiyo, naomba hili wasiende wakafanya maamuzi ambayo yatawaumiza wananchi na baadaye wakaumiza Serikali na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla. Niombe hili walifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo ambayo tutaishauri Serikali, kama dhana ni kulinda rasilimali, kitu cha kwanza ambacho tunahitaji kukifanyia kazi waende wakaisimamie sheria ambayo itaondoa tatizo la uvuvi haramu. Wakaimarishe doria, wakatafute watu ambao watawasaidia ili waweze kulinda rasilimali.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kulinda baadhi ya maeneo ambayo yatatenga mazalia ya samaki ambayo yatakuwa yamehifadhiwa na walianzisha vizuri na kuna dalili ambayo walianza, wakaweka mpaka maboya kwenye maeneo ambayo wanaonesha kwamba maeneo haya yatakuwa ya matunzo na mazalia ya samaki. Ile ndio njia sahihi ambayo wanaweza wakasaidia hawa wavuvi. Wawapelekee sasa uvuvi

na ufugaji wa samaki wa kisasa ambao wamepeleka Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika wawapelekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, wapeleke zana za kisasa ambazo zinaweza zikavuna kwenye eneo la Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika ndilo Ziwa pekee ambalo wapo samaki ambao kumwona mpaka aweze kufa yeye mwenyewe ndio anapanda huku juu, kwa sababu hakuna zana za kuweza kuwavuna. Naomba hili wakalifanyie kazi kuliko yale ambayo wanaweza tu wakifika wanakubaliana mikataba ambayo itakuja kuwaumiza Watanzania na mkataba huo asilimia kubwa watakaonufaika ni nchi jirani kuliko sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu asilimia kubwa ya wavuvi wanaokuja kuvua eneo letu ni Nchi ya Congo, Nchi ya Burundi na upande ule wa Kusini ni Zambia wanavua kwenye maeneo ya kwetu. Ukiangalia maeneo haya yote uvuvi wa kwao na maeneo wanayoyamiliki ni kidogo sana lakini ndiyo wanaovua kwa kiwango kikubwa kuzidi kwenye maeneo ya kwetu. Zambia wamewekeza, wamepeleka vifaa ambavyo vinaweza kuwasaidia wavuvi lakini kwenye maeneo mengine kama DRC Congo, Burundi wameruhusu nyavu hizo ambazo ni hatari kwetu na kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayazungumza haya ili kuepusha tafrani ambayo inaweza ikajitokeza endapo Serikali itaenda kwa mawazo ambayo wakakubaliana kitu ambacho hakitakuwa na tija kwa wananchi wetu. Mimi naamini Serikali mkijipanga vizuri mkasikiliza mawazo ya Wabunge, mnaweza mkatatua tatizo ambalo kimsingi litaleta furaha kwa wananchi ambao tunawasimamia.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, kengele ya pili ilishagonga.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba Mheshimiwa Waziri ayafanyie kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, ajiandae.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yao hii ambayo moja kwa moja imeenda kutafsiri maono pamoja na mawazo ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan namna ambavyo anataka Taifa letu liendelee kiuchumi, kimaendeleo na mambo mengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama samia Suluhu Hassan kwa kweli Mama anafanya kazi kubwa mno, anajitahidi sana kufanya kila *means* kutengeneza diplomasia ndani ya nchi ili kuhakikisha Taifa linasonga mbele kwa maendeleo zaidi. Pia kupitia Wizara hii nitakuwa nina dhambi kubwa nisipompongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya hususan kwenye Wizara kama hii kwa kule Zanzibar tunaita Wizara ya Uchumi wa Bluu, kwa kweli

Mheshimiwa Rais ameonesha wazi namna ya kutaka kuifumua Zanzibar kwenye uchumi, hususani ambao utaenda kwenye masuala ya uvuvi kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na nimtie moyo aendelee kuchapa kazi na Watanzania tunaona kazi kubwa ambayo anaifanya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa hapa takribani zaidi ya miaka Kenda tunaposimama hapa kwenye Bunge tunakuwa tunashauri, hususani Wabunge ambao tunatokea upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namna ya kitoweo ambacho kinaitwa nyama. Nyama ya ng'ombe kwa upande wa Zanzibar ni *very expensive* ukilinganisha na huku Bara, ingawa nyama ya ng'ombe kwa asilimia 100 kwa upande wa Zanzibar tunategemea soko kubwa kutokea huku Bara, lakini kuna tozo lukuki ambazo bado Wizara haijataka kusema kwamba sasa kwa vile sisi ni nchi mbili, tunawaachia wenzetu kwenye suala la kodi hizi nyingine ndogondogo ambazo zinatuumiza kwa upande wa pili wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuamini sasa hivi bei ya nyama ukilinganisha Bara na Zanzibar ni tofauti sana. Upande wa Bara nyama inanunuliwa kwa kilo moja shilingi 6,000 hadi shilingi 7,000 lakini upande wa pili wa Zanzibar nyama kilo moja sasa hivi unanunua shilingi 13,000 na kuendelea, hii yote inasababishwa kwamba bado Wizara haijaamua kabisa kusamehe baadhi ya tozo.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nizitaje baadhi ta tozo ambazo zimekuwa kichefuchefu kwa uapande wa pili wa Zanzibar na inapekea bei ya nyama kuwa nzito kwa upande wa pili wa Zanzibar. Mfano mzuri bei ya nyama, ng'ombe anapotoka Bara kumpeleka Zanzibar kuna tozo ambazo zinachajiwa, ipo tozo ambayo Wizara ya Mifugo inatoza ng'ombe ambaye anaenda Zanzibar, ambayo hii tunaweza pia tukaisamehe kama Wizara ili Zanzibar aweze kununua kilo ya

nyama kwa bei nafuu, hii nayo iangaliwe Mheshimiwa Waziri ikiwezekana ifutwe kabisa na isamehewe, sote ni nchi moja, sote tunafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ipo tozo ya Halmashauri nayo pia inachajiwa, yule ng'ombe ambaye anapelekwa Zanzibar lazima achajiwe tozo ile ambayo inatoka huku Bara, Halmashauri ya Tanzania Bara. Pia ipo tozo ya Kijiji ambayo inachajiwa kwa ng'ombe yuleyule ambaye anaenda Zanzibar. Pia ipo tozo ambayo inachajiwa na wenzetu wa *TRA* yule ng'ombe mmoja ambaye anaenda Zanzibar. Tozo ya *TPA* watu wa bandari nao pia wanamchaji ng'ombe yule anayeenda Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia ipo tozo ambayo inaitwa *export levy* ambayo hii hata mtu wa Kenya akija kununua ng'ombe Tanzania anampeleka Kenya hii anachajiwa ambayo inaitwa *export levy,* na Mzanzibar hivyo akinunua ng'ombe huku Bara kumpeleka Zanzibar na wao pia inachajiwa. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, ili kulinusuru soko la Zanzibar pia kuwanusuru Watanzania wa Zanzibar tuziangalie hizi tozo na ikiwezekana mkae Wizara zote mbili ili kuweza kuzifuta hizi tozo na bei ya nyama ikawa rafiki kama ya Zanzibar na bei ya Bara zote zikawa sawa. Tukifanya hivi tutakuwa tayari tumewapunguzia wenzetu kule wa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naliomba sana hili jambo kupitia Wizara yako Waziri Mheshimiwa Abdallah Ulega, naamini ni kijana una uwezo mkubwa wa kuweza kufanya *lobbying* ya kuzungumza na baadhi ya taasisi nyingine hizi ambazo zinashirikiana na wewe kwa ajili ya kufuta kabisa hizi tozo.

Mheshimiwa Spika, niende upande wa pili wa uvuvi. Imekuwa kila mwaka kipindi cha bajeti nalizungumzia suala la zao la mwani, mara hii kwenye bajeti yako Mheshimiwa Waziri

umelizungumza zaidi ya mara tatu suala la mwani, lakini kuna taarifa imewasilishwa na Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira ambayo inashughulika na suala hili pia imezungumzia zaidi ya mara nne. Suala la mwani bado hatujaona mpango mkakati, bado mmezungumzia suala la elimu, kutoa vifaa, sijui kuwezesha wakulima wa mwani, lakini ninachotaka kuwaambia mwani hasa changamoto yake ni soko siyo *issue* ya kuzalisha. Wakulima wetu bado hawajakatishwa tamaa, zao hili takribani zaidi ya miaka 20, 30 linalimwa na wakulima bado hawajakata tamaa, bado hali zao ni duni bado najua hawakopesheki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali bado hamjaandaa mpango mkakati wa kulisaidia hili zao la mwani. Leo wakulima wengi wa mwani wanalalamika suala la bei, bado Serikali haijawa wazi kabisa, haijawa na mpango wa kuwasaidia wakulima kuweza kupata soko rafiki na ikapatikana bei nzuri ya mwani ili mkulima aweze kufurahia zao lake la mwani. Mfano mzuri, Mheshimiwa Waziri tunalo zao la korosho, kuna parachichi, kuna mazao mbalimbali yote tumeona Serikali imeweka mpango mkakati na mazao haya yote yanauzika huko nje na wakulima wanafurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini zao la mwani bado hatujaona kabisa Serikali kulizungumzia hili, hasa kuwatafutia soko la mwani? Kwa hiyo, nawaombeni sana, Mheshimiwa Waziri unaufahamu mwani, unawafahamu wajasiliamali wa mwani sasa hivi wanavyopata shida, lakini suala la soko bado. Tuliangalieni, karibisheni wawekezaji wakubwa waje kuwekeza hapa nchini kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naiomba sana Wizara kwa ushauri tengenezeni Bodi ambayo itakuwa inashughulika na masuala ya mwani tu kwenye suala la bei, kwenye suala la upandaji, kwenye suala la dawa na masuala mengine mbalimbali

itasaidia sana na naamini kwa kipindi kifupi zao la mwani litapata *value* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nakuona umeshabonyeza kengele yako, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wapo wageni ambao hawakupata fursa ya kutangazwa asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni Saba wa Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda ambao ni viongozi wa wavuvi kutoka Kigoma Mjini, karibuni sana. Wapo pia wageni Watano wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze ambao ni viongozi wa wavuvi kutoka Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa wakiongozwa na Ndugu Bakari Mfaume, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili na mimi niweze kuchangia hii Wizara muhimu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni-*declare interest* kwamba niliwahi kuwa Waziri wa Wizara hii tangu mwaka 2017 mpaka 2020, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Abdallah Hamis Ulega kwa uteuzi na kwamba mimi namwamini kwa sababu wakati ule alikuwa Msaidizi wangu, najua uwezo wake na najua kwamba atafanya kazi nzuri kwenye Wizara hii. Nakumbuka mambo mengi tuliyofanya pamoja lakini pia nawakumbuka Watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Upande wa sekta ya

mifugo namkumbuka Dkt. Asimwe, Dkt. Furaha Mramba, Dkt. Mwambene, Dkt. Mlawa, Dkt. Shirima, Ndugu Stephen Michael pamoja na Iman Sichalwe na Ndugu Noel.

Mheshimiwa Spika, upande wa uvuvi pia nawakumbuka vizuri sana Ndugu Chama Marwa, Ndugu Madaha, Ndugu Komakoma ambaye alipima samaki hapa Bungeni, ninamkumbuka Ndugu West Mbembati, Ndugu Romani Mkenda, Ndugu Ruhasile, Ndugu Judith Mgaya, Dkt. Sweke na Dkt. Mgalila, tulifanya kazi nzuri pamoja na watumishi wengine wote wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ambao tulifanya kazi nzuri, kuzunguka nchi hii karibu kila sehemu, pia tulifanya kazi hadi Saa Saba usiku wakati mwingine hata wakati mwingine tulikesha ofisini katika *slogan* ya masaa ni namba. Nawashukuru sana bado nakumbuka mchango wenu mkubwa katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana hatua za Wizara ambazo sasa hivi wanaendelea na ujenzi wa bandari, hili ni jambo ambalo nililitamani sana lakini uwekezaji unaoendelea NARCO sasa hivi, napongeza sana ni jambo zuri, tofauti na mawazo ambayo tuliletewa mwanzo kwamba sasa inabadilishwa tena inakuwa shamba la alizeti. Hii mipango ndiyo tunayoitaka na Waziri aendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri utakumbuka kwamba Wizara iliahidi ujenzi wa mnada wa Kimataifa Mwambea na eneo lilishapatikana wataalam walishalikagua, sasa tunachokitaka ni huu mnada ujengwe, tunataka utuambie utakapokuwa una-*wind up,* sasa mnada huu wa Kimataifa ulioahidiwa na Serikali toka mwaka 2020 wa Mwambea unaenda kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni wapangaji katika Ranchi ya Mabale, kuna wananchi waliopanga zaidi ya vitalu

23 na walishasaini mikataba yao muda mrefu, zaidi sasa ya mwaka mzima, lakini nakala ya mikataba hiyo hadi sasa kampuni la Ranchi za Taifa *(NARCO)* haijawarejeshea mikataba yao tatizo ni nini? Waziri kamilisha maliza hili tatizo la migogoro ya hawa wafugaji ili waweze kupata haki yao kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni ukamataji holela wa mifugo. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la ukamataji holela wa mifugo, sheria ziko wazi, Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 *(The Animal Disease Act No. 2003)* lakini pia na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 na Kanuni ya *The Animal Welfare Impounded Animal Regulation 2020*.

Mheshimiwa Spika, hizi kanuni ziko vizuri sana juu ya ukamataji wa mifugo lakini bahati mbaya sana watendaji wengi wa Serikali wamekuwa wakizivunja kanuni hizi, mambo haya yamekuwa yakijirudia. Kikubwa ni kwamba kuna maslahi makubwa juu ya ukamataji huo wa kiholela, tunasikitika kwamba kila tunapozungumza hapa Bungeni hakuna hatua zinazochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mfano ni ukamataji holela ambao unapelekea Wanyama wanayimwa malisho, wananyimwa maji, wanayimwa dawa, wananyimwa chanjo, matokeo yake mifugo imekuwa ikifa tu ikiwa imeshikiliwa na Serikali. Tunazungumza wafugaji wa mwisho wa mwaka 2020 waliokamatiwa mifugo yao ikafa zaidi ya 6,000 mpaka leo hii wanakuja kudai hapa mifugo, wafugaji zaidi ya 12 kutoka Jimbo la Kisesa wamekuja na fimbo zao kufuata ng'ombe zao hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ukamataji bila kushirikisha viongozi. Mifugo inakamatwa viongozi

hawashirikishwi, wafugaji hawaitwi kuhakikisha mifugo yao, matokeo yake mifugo inaibiwa, mifugo inapotezwa, mifugo inauzwa kiholela. Sasa hivi tunavyozungumza kule Kilombero, *DC* wa Kilombero amekamata mifugo zaidi ya siku 10 sasa. Mifugo hawakuwa kwenye hifadhi zaidi ya ng'ombe 2,082, hawakuwa kwenye hifadhi lakini wameshikiliwa tu, maelezo hayatolewi, ushirikishwaji haukutolewa, mifugo wanaendelea kufa na wengine wanazidi kupotea na wengine wanazidi kuibiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mifugo kuuzwa kiholela. Mifigo inakamatwa baadae inauzwa kuholela tu kwa sababu haijahesabiwa haijulikani inauzwa kuholela. Sheria zinasema mifugo hii lazima iuzwe kwenye minada kwa bei ya ushindani na kwa uwazi, matokeo yake mifugo hii imekuwa ikiuzwa porini na Serikali inaruhusu hilo jambo kuendelaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilituletea hapa kuishia Disemba Serikali iliuza mifugo ng'ombe 3,828, hawa ng'ombe baada ya hapo Serikali ikauza kwa milioni 685, kwa maana ya kwamba kila ng'ombe aliuzwa kwa shilingi 180,000 wakati *average* ya mifugo ng'ombe mmoja ni 750,000 maana yake zinaibiwa karibu 570,000 kwa kila ng'ombe. Katika *transaction* hiyo tayari wale watumishi walijinufaisha zaidi ya bilioni 2.18, haya yanafanyika na Wabunge tuko hapa na Serikali iko hapa *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile wafugaji wanatozwa faini ya Shilingi 100,000 ambayo haimo kwenye Sheria ya Wanyamapori, haimo kwenye Sheria ya Misitu lakini wanaendelea kutozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko hapa la kuzuia hayo mambo kutokea, lakini mambo hayo yamekuwa yakiendelea, mimi siamini kama wale watumishi

wana uwezo wa kuzuia maelekezo ya Waziri Mkuu, isipokuwa Waziri Mkuu mwenyewe anaruhusu haya mambo yafanyike na yanafanyika kwa ridhaa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la hereni Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko hapa la kuzuia suala …

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mpina kwamba hakuna uthibitisho huo kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa ridhaa, huko ni kutumia vibaya jina la Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo ambalo kauli ambayo siyo nzuri na siyo ya kiungwana. Jambo la pili nimpe taarifa pia kwamba….

**SPIKA:** Taarifa ni moja Mheshimiwa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Mpina unapokea taarifa hiyo?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, sipokei taarifa yake na ninaomba niendelee. Suala la ufungaji wa hereni mifugo, Mheshimiwa Waziri Mkuu..

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ananimalizia muda wangu naomba usipokee taarifa yoyote. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, kati ya watu mahiri sana wanaosaidia wafugaji katika kutatua matatizo yao ni Waziri Mkuu, kwa hiyo naomba hilo jambo asiliingize kwenye mchango. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na unilindie muda wangu, naweza nikaendelea pamoja na makofi haya yakiendelea.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naombeni mkae kimya.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, suala la ufungaji wa hereni linaloendelea hivi sasa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa taarifa hapa……

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kupiga makofi ambayo yalisababisha Mheshimiwa Luhaga J. Mpina kushindwa kuendelea kuchangia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge,…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Hizo ni fujo, Mbunge huwezi kufanya mambo hayo, hizo ni fujo, waniachie muda ambao..

*(Waheshimiwa Wabunge waliendelea kupiga makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mpina subiri kwanza, umepewa taarifa na Mheshimiwa Getere unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo yanayolalamikiwa katika Wizara hii, yapo mambo yanayolalamikiwa katika Wizara hii, wananchi na Wabunge lakini Wizara imekaa kimya. Mambo ambayo wakati mwingine yanaenda kupelekwa mpaka kwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, mambo ambayo yalitekelezwa kwa mujibu wa sheria, mambo hayo mfano uchomaji wa vifaranga…..

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kuna Kanuni inavunjwa inaonekana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Kanuni inayovunjwa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu Kanuni ya 71(1)(a) na Kanuni ya 75 kama nilivyoanza nayo, kinasema: "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli." Katika ku-*support* Kanuni hiyo, inanipasa mimi kuthibitisha ni kwa namna gani Mbunge huyo anatoa taarifa ndani ya Bunge ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpina anamtuhumu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ni chanzo cha kutotekelezwa kwa utendaji bora kwenye masuala hayo ya kutetea wafugaji na kusimamia haki za wafugaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba taarifa zinazotolewa na Mheshimiwa Mbunge hapa ndani hazina ukweli kwa sababu, ni juzi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa kauli hapa ndani mbele ya Bunge lako kuonesha ni kwa kiasi gani Serikali, na yeye akisimamia na kutoa maelekezo kwa Serikali, namna bora ambayo Serikali itafanya kushughulikia migogoro ya wafugaji, kushughulikia migogoro ya hifadhi na kuhakikisha pia malalamiko ya Wabunge, malalamiko ya Watanzania na Maazimio ya Bunge yanafanyiwa kazi ipasavyo, ili kulinda heshima ya Serikali na heshima ya Wabunge na vile vile kujali hali na malalamiko ya Watanzania katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu wako kama jambo hili analoendelea nalo Mheshimiwa Mbunge pamoja ya kupewa taarifa mbili amezikataa, kama ni jambo sahihi na linakubalika ndani ya Bunge lako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, akionesha kwamba kuna kanuni inavunjwa wakati Mheshimiwa Mpina akichangia na ametupeleka kwenye Kanuni ya 75 ambayo inampa fursa ya yeye kusimama na kueleza ni Kanuni gani inayovunjwa na ametupeleka kwenye Kanuni ya 71(1)(a), akieleza kwamba, kanuni hiyo inakataza Wabunge kutoa taarifa ambazo hazina ukweli. Pia ameeleza kuhusu mchango wa Mheshimiwa Mpina ambao kwa yeye Mheshimiwa Jenista ameona ametoa taarifa ambazo hazina ukweli.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nimemsikiliza Mheshimiwa Mpina, ameeleza maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu huko nyuma, na kwamba hayo maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu hayafuatwi katika hili eneo analochangia yeye. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo, ndiyo anasema, ikiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo na hayafuatwi na wale wanaopaswa kuyafuata, basi maana yake mtoa maelekezo, yeye mwenyewe pia anaona sawa. Ndiyo mchango wake ulipo. Kwa sababu mimi nimemsikiliza kwa maneno aliyoyasema. Sasa Mheshimiwa Jenista ameomba utaratibu kwamba taarifa alizozisema hazina ukweli.

Sana sana hapo mimi nitataka kujua katika yale maelekezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyasema, ni kweli aliyasema hayo maelekezo ama hayapo? Kama yapo, je, yamefanyiwa kazi au Hapana? Kama hayajafanyiwa kazi, hoja ya Mheshimiwa Mpina ni kwamba, kama hayafanyiwi kazi, na yapo maelekezo, maana yake mtoa maelekezo ameona kwamba yale maelekezo yake yanaweza yakafuatwa, ama yasifuatwe. Ndiyo hoja ilipo ya kisheria kabisa kuhusu utaratibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndivyo mimi nilivyomsikia Mheshimiwa Mpina. Sasa kama amesikika vinginevyo, Mheshimiwa Jenista mimi nitakupa nafasi nyingine. Hicho ndicho nilichokisikia ili niweze kutoa maamuzi kuhusu utaratibu huu ulioombwa. Kama maelezo yapo tofauti na hayo niliyotoa, Mheshimiwa Jenista nakupa tena fursa, na kama sio haya, basi nitaenda kufuatilia kwenye *Hansard* halafu nitakuja kutoa uamuzi hapa.

Mheshimiwa Jenista nakupa nafasi nyingine.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, nadhani wote tumemsikia Mheshimiwa Mpina maelezo aliyoyatoa Bungeni. Maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mpina anayazungumzia kwa muktadha wake yanahusu migogoro ambayo inawahusu wafugaji. Nimesimama kusema kwamba, Serikali haitekelezi ama hakuna hatua ambazo zimechukuliwa kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kulithibitishia Bunge lako ni kwamba, mfano halisi ambao Serikali tunao, huku ndani na hasa katika michango ya Bunge la Bajeti lililopita na michango mingine ya Wabunge ambayo ilikuwa inazungumzwa kuhusu migogoro hii, Bunge liliiomba Serikali iunde Timu za Uchunguzi, itafute njia za kufanya na kusuluhisha migogoro yote ambayo imekuwa ikijitokeza. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ujumla wa hayo yote, yakiwemo hayo ambayo anayazungumza Mheshimiwa Mpina, aliyajumisha utekelezaji wake katika taarifa aliyoitoa akionesha yaliyofanywa na Serikali na maelekezo ya ziada kwa Mawaziri na Serikali kuhakikisha mambo hayo yote yanafanyiwa kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaposema kwamba ama Waziri Mkuu hajasimamia, ama Serikali haijachukua hatua, ndiyo inawezekana yapo maeneo machache, lakini kwa ujumla wa maagizo ya Serikali na mwongozo ambao umekuwa ukitolewa na aliyeutoa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ndani, unadhihirisha kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe, Serikali kwa ujumla na sekta zinazohusika zimechukulia uzito suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwako, tayari tumeshaelekezwa na shughuli zimeshaanza na ratiba za kushughulikia masuala hayo zilishaanza na zinaendelea. Hata *weekend* hii zipo ratiba ambazo zitaendelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Mpina maeneo mahususi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyatolea maelekezo ili usiwe umeeleza kwa ujumla hayo mambo ili tushughulike na hayo, nitoe maamuzi juu ya jambo hili.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Ni maelekezo gani Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyatoa na hayajafanyiwa kazi?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nilifurahi sana uliposema kwamba tutaenda kwenye *Hansard* ili kwenda kuthibitisha kile nilichokizungumza mimi. Nilisema hapa, Wabunge hapa wamezungumza wengi, nami nina ushahidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, sasa hivi kamata kamata ya bila kushirikisha wananchi ni marufuku. Toka Agizo la Waziri Mkuu la kamata kamata ya mifugo bila kuzingatia sheria; na hii kanuni ninayoizungumza, mimi ndio nilikuwa Waziri, niliisaini mimi ya kuzuia ukamataji ovyo ovyo; watu wanakamatwa.

Mheshimiwa Spika, toka Waziri Mkuu alipotoa tamko, watu wameendelea kukamatwa, na ushahidi upo. Sasa Waheshimiwa Wabunge, Waziri Mkuu ni Mtendaji wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, na sisi ndio tunamthibitisha. Sasa unapotokea upungufu kama huu hatuwezi kuufumbia macho kuusema.

Mheshimiwa Spika, hata kama anavyotaka yeye kuleta, ushaidi wa matukio…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, tuelewane vizuri. Maelekezo ya Waziri Mkuu aliyoyatoa siku ya Alhamisi wiki iliyopita, ndiyo unayosema? Kati ya ile Alhamisi alipoyatoa mpaka sasa, kamata kamata imeendelea?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Hilo eneo ndilo ambalo wewe una ushahidi nalo?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Sawa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu, jambo hili limefika mahali ambapo linahitaji ushahidi. Sasa ili niweze kutoa huu mwongozo, kwamba yale aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu yanafanyiwa kazi, Mheshimiwa Mpina anasema yeye anao ushahidi kwamba yale aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu hayafanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mpina utaniletea huo ushahidi. Kwa hiyo, hiyo hoja unaiacha ili uendelee na nyingine mpaka nitakapopata ushahidi ili nitoe mwongozo kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mpina, malizia mchango wako.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, najua umenitunzia muda wangu. Sasa nilikuwa…

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, tuelewane vizuri. Muda wako uliotunzwa vizuri ni ule unaohusu Utaratibu, siyo unaohusu taarifa. Kwa hiyo, usije ukaanza kudai dakika zako za Mheshimiwa Getere na za Mheshimiwa Waziri hapa. Dakika pekee unazonidai ni zile za kuhusu utaratibu ambazo nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Jenista hapa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, utaniongeza kidogo tu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia suala la utekelezaji wa mambo yaliyotekelezwa kwa mujibu wa sheria, halafu mwisho wa siku anakuja kulaumiwa mpaka wanalaumiwa viongozi wetu wakuu. Analaumiwa Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu wa Tano wa Nchi hii, mambo ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyatekeleza kwa mujibu wa sheria, halafu Wizara iko kimya. Waziri yuko kimya, na watendaji wa Serikali wako kimya.

Mheshimiwa Spika, suala la uchomaji wa vifaranga. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilichoma vifaranga 6,550 kwa mujibu wa sheria. Tunalo zuio la kuingiza mazao yote ya ndege kutoka nchi yoyote ile kutokana na nchi yetu kuwa *suspected* na kuenea kwa magonjwa ya mafua makali ya ndege. Tuna zuio la toka mwaka 2006, hairuhusiwi. Kosa lingine, ni kwamba huyu aliyekuwa anaingiza, hakuwa na kibali chochote kinyume cha Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya Mwaka 2003. Hana kibali chochote na haijulikani hao vifaranga wametoka wapi?

Mheshimiwa Spika, la pili, hakukuwa na cheti cha afya. Ukaguzi wowote wa kujua hao mifugo walikuwa wamechanjwa wana magonjwa gani? Hakuna kibali chochote. Sasa katika mantinki hiyo, sheria inasema, ukikutana na bidhaa za namna hiyo uzichome. Serikali ingefanya nini? Utawapeleka wapi? Hawajulikani walipotoka, hakuna kibali cha afya, hawajachanjwa, yaani Waziri au Serikali ikubali kuridhia Watanzania waje kufa na magonjwa ya mafua ya ndege hapa! Serikali ikubali kuridhia wafugaji wa Tanzania zaidi ya kuku 76,000,000 wa Watanzania, Waziri uliyeapishwa kwa mujibu wa sheria, uje uruhusu wafugaji hawa wote kuku wao wafe kwa magonjwa ya ndege kwa kumbeba mfanyabiashara mmoja, ili mfanyabiashara tu huyo wa vifaranga 6,000 aingize vifaranga vyake hapa nchini! Hayo mambo kwa nini hayazungumzwi na Wizara?

Mheshimiwa Spika, la tatu, suala la kupima samaki kwa rula Bungeni. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini kinachomfanya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kutamka kwa sauti kwamba samaki anapimwa kwa urefu, na kwa urefu huo anapimwa kwa kutumia rula? Waziri wa Uvuvi anashindwa nini kusema nini kwa sauti kwamba ili uweze

kukidhi matakwa ya Kanuni Namba 58 ya Kanuni ya Uvuvi ya Mwaka 2009, ni lazima umpime kwa rula ili uthibitishe vipimo kama ni sangara au sato? Anashindwa nini kufanya hivyo? *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya wanazidi kutapakazwa viongozi, walipima kwa rula, walifanya hiki na kile!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, muda wako umekwisha, ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, dakika moja, dakika moja tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, dakika moja.

**SPIKA:** Hiyo dakika ilikuwa nikupe, lakini nachelea unatukumbusha mtu anapima na rula samaki ambaye ameshapikwa, yuko tayari kwa ajili ya kuliwa! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nusu sekunde. Nusu dakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nadhani sasa tutulie tupate mambo mengine tofauti kabisa na hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utazidi kusisitiza umuhimu wa ukujuaji wa uchumi wa Taifa hili. Baadaye mtaona nitasisitiza umuhimu wa Sekta ya Uvuvi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Jimbo langu la Musoma Vijijini, tuna kata 21, tuna vijiji 68, Kata 18 ziko pembezoni mwa Ziwa Victoria wanajishughulisha na uvuvi. Katika hizi kata, ni kata tatu. Kwa hiyo, hiki ni kithibitisho kwamba uvuvi lazima uchangie uchumi wetu kwa hali ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uvuvi tunavyouchukulia sisi watu wa Musoma na nadhani ndiyo Taifa zima, kwanza unatoa chakula. Kwa hiyo, kwa mambo ya kiuchumi, uvuvi ni kwenye *food security*, uvuvi unatoa ajira na uvuvi unachangia uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa Taifa. Uchumi wa Tanzania kwa muda wa kama miaka mitatu, minne unakua kati ya asilimia tano na sita. Saa hizi nadhani upo kwenye 5.6.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili Bunge la Bajeti kuna maeneo ambayo ninawasihi tutoe ushauri kwa Serikali kusudi uchumi wetu kama tunataka uondoe umasikini kama nilivyowaeleza juzi, uchumi ni lazima ukue kuanzia asilimia nane kwenda asilimia 10. Ni sekta tano tu ndizo zinaweza kufanya uchumi uende kwa haraka *(accelerated growth)*. Cha kwanza kabisa ni gesi asilia. Tutalijadili huko. Cha pili ni madini, cha tatu ni kilimo, inakuja mifugo na uvuvi na cha tano ni utalii. Hizi sekta tano, kila moja ningechangia asilimia mbili ya ukuaji wa uchumi, tungeweza kufika hizo nane mpaka kumi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa nini nasema uchumi. Wataalamu wa lishe wanasema kwamba, kama unataka *balanced diet* (chakula bora) unapaswa kutumia *grams* 280 mara mbili kwa wiki. Yaani *portion* ya kwanza gramu 140, na siku nyingine gramu 140, 280. Sasa tunavyosema uvuvi ni uchumi muhimu, tuangalie soko letu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, soko letu la kwanza, kama wananchi wote duniani wanataka kula namna hiyo, wako watu bilioni nane sasa hivi. Tanzania ikiuza huko Samaki, tutapata fedha nyingi. Kama soko letu ni ndani ya Bara la Afrika, sasa hivi Barani Afrika tuko watu bilioni 1.43. Kwa hiyo, hizo ni fedha nyingi sana ukipiga kwa *grams* 280. Kwa hiyo, Sekta ya Uvuvi tuichukulie kibiashara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022 samaki waliozalishwa duniani walikuwa ni tani milioni 184.6. Mzalishaji wa kwanza hapo alikuwa ni China aliyezalisha tani milioni 67.5, na katika hizo tani milioni 54.6 alizalisha kutumia vizimba, na huko baadaye ndiyo nitakuja kusisitiza suala la vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wa pili alikuwa ni India ambaye uzalishaji wake duniani ni asilimia 7.56. Sasa maoteo ya mwaka huu ya biashara ya samaki duniani, mapato yake yatafika bilioni 612. Hapo ndipo tunapaswa kushawishi na kuishauri Serikali iwekeze zaidi kwenye uvuvi. Samaki wa vizimba duniani wanaozalishwa ni tani milioni 180. Mzalishaji namba moja ni China, anazalisha theluthi moja; wa pili, ni India ambaye anachuana na Misri *(Egypt)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Afrika Egypt ndiyo inaongoza, sasa Egypt yenyewe kwa mfano mwaka juzi ilizalisha samaki tani milioni 2.2 kati ya hizo, tani milioni 1.7 walizalishwa kupitia vizimba hii ni zaidi ya 77%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja yangu hapa na mchango wangu kwenye hii Wizara nitabaki kwenye uvuvi na ninazidi kusisitiza umuhimu wa samaki wengi wamesema samaki wamekosekana Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria. Suluhisho lake ni samaki uvuvi wa vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuiangalie Tanzania ilivyo na ndugu zangu wa *Lake Tanganyika* walikuwa wanalalamika, wana haki ya kulalamika. Utafiti ambao nina muomba Mheshimiwa Ulega na maprofesa wake wafanye siyo ule alioripoti jana kwamba walifanya utafiti wakafikia *conclusion* kwamba lazima zana zipatikane. Nadhani hiyo unaweza ukafikia hiyo hata bila utafiti.

Mheshimiwa Spika, utafiti unaohitajika Mheshimiwa Ulega ni kijana mzuri, msomi mzuri wa *Bio-aquatic sciences*. Tunachukua *Lake Tanganyika*, *Lake Tanganyika* umri wake ni miaka milioni 10, maji ya Ziwa Tanganyika yaliyomo Ziwa Tanganyika ujazo wake ni *cubic meter* 18,880. Aina ya samaki waliopo ni zaidi ya 350. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara yetu tunataka wafanye utafiti hapa, Ziwa Tanganyika; nikiwa Kigoma nimekaa Kipiri, nimekaa sehemu nyingi huko nafanya utafiti lakini mbona samaki ni aina mbili tatu? Hizi 330 wengine wanaenda kwenye *extinction* wanapotea sisi bila kuwajua. Tunaenda Ziwa Nyasa, Ziwa Nyasa lina umri wa miaka milioni mbili. Ujazo wa maji kwenye Ziwa Nyasa ni *cubic kilometer* 8,400, Ziwa Nyasa hilo na lenyewe ndiyo lina samaki wa aina nyingi kuliko aina yoyote hapa duniani. Ni kati ya 800 na 1,000 *species of fish*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ripoti zetu hizi *species* zote 1,000 za Ziwa Nyasa ziko wapi? Tunakuja Ziwa Victoria lenyewe ndilo changa kuzidi yote. Umri wake ni miaka 400,000 lakini ujazo wake wa maji ni *cubic kilometer* 2,424. Aina ya samaki waliomo

Ziwa Victoria ni zaidi ya 500. Kwa hiyo, pendekezo langu la kwanza kwa Wizara yetu hii kwenye haya maziwa makuu matatu yana maji ya kutosha. Yana aina nyingi sana za samaki kama Ziwa Victoria 500. Je, hawa samaki wote wako wapi? Wanavuliwa na nani? Hao wengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muhongo kengele ya pili imeshagonga, dakika mbili malizia.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, dakika mbili afadhali. Sasa kwa kumalizia niseme hivi; Ziwa Victoria nimechukua ukubwa wake, Kenya wana 6% ya Ziwa Victoria, Uganda wana 45% na Tanzania tuna 49%. Kenya yenye 6% ina viwanda 18 vya samaki. Uganda yenye 45% wana viwanda 11. Tanzania ambao tuna 49% na ripoti hapa Mheshimiwa Ulega Musoma hatuna kiwanda hata kimoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pendekezo langu la mwisho ni kwamba tuwekeze kwenye uvuvi wa vizimba. Tutoe kama hii mikopo iliyokuja nashukuru Mheshimiwa Waziri ameniambia wiki ijayo watu watapewa ile mikopo yao tuvue kwa vizimba lakini vilevile kwa sababu samaki wa vizimba ni wengi tutoe mikopo kwa Watanzania waanzishe viwanda vya samaki kwa sababu samaki wa vizimba watakuwa wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo; kwanza Benki ya Kilimo iweke kipaumbele kukopesha wafugaji hasa wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Spika, Wizara na taasisi husika zilizo chini ya Wizara ziendelee kutenga maeneo ya kufugia na maeneo ya malisho, mifugo ni mingi kuliko rasilimali ardhi, malisho, maji, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupata vitalu vya kufugia katika Ranchi za Taifa usiwe mgumu kama ilivyo sasa. Wizara iweke utaratibu rafiki kwa wananchi wanaohitaji vitalu wasipate vikwazo na vikatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke ruzuku kujenga vituo vya maziwa na viwanda, kama inavyojenga masoko, stendi za mabasi, vituo vya afya, na kadhalika; kwa nini hawajengi vituo vya maziwa na viwanda?

Mheshimiwa Spika, wafugaji wa ng'ombe wa asili wako tayari kubadilika na wao kujaribu kufuga kisasa, shida ni upatikanaji wa ng'ombe bora wa maziwa ukitaka hata ng'ombe 100 utazunguka nchi nzima hupati, Serikali iwekeze zaidi kwenye uhimilishaji na kuagiza mitamba nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijenge masoko ya kuuzia maziwa au vituo vya kuuzia maziwa maana si salama kiafya, wauza maziwa wanapanga maziwa chini, pia Serikali inakosa mapato mengi kupitia utaratibu huu mbovu uliopo hivi sasa. Asilimia 90 ya maziwa yanayozalishwa nchini karibu lita bilioni nne kwa mwaka huuzwa katika mfumo usio rasmi na kuikosesha Serikali mapato. Tunaomba Serikali iwekeze kujenga mifumo na miundombinu ya kukusanya na kuuza maziwa mpaka vijijini kama ilivyo kwa sekta ya nyama kila kona kuna *butchery.*

Mheshimiwa Spika, Serikali iwekeze sana kwa vijana na wanawake ili sekta ikue na kuwa endelevu.

Pia Serikali itenge bajeti kubwa ya kuhamasisha kulima na kuhifadhi malisho na maji kwani bila kufanya hivyo wafugaji wataendelea kuhamahama kwa kufuata yalipo malisho na maji na kuendelea kuharibu mazingira. Tupeleke mashamba darasa kila kijiji kuhusu majani ya malisho ya ng'ombe kuepuka ufugaji wa kuhama hama.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa hotuba nzuri iliojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu za mifugo na uvuvi ya mwaka wa kilimo 2022/2023 inaonesha kuwa idadi ya

ng'ombe ilikuwa milioni 36.6 kutoka milioni 35.3 waliokuwepo 2021/2022. Kati ya hao, wakulima wadogo walikuwa na ng'ombe milioni 36.4 na mashamba makubwa yalikuwa na ng'ombe milioni 0.2. Aidha, wakulima wadogo walikuwa na mbuzi milioni 26.3 na mashamba makubwa mbuzi milioni 0.34.

Kwa upande wa kondoo, wakulima wadogo walikuwa na kondoo milioni 8.9 na mashamba makubwa kondoo milioni 0.24. Vilevile nguruwe waliofugwa na wakulima wadogo walikuwa milioni 3.7 na mashamba makubwa yalikuwa na nguruwe 5,123 na kulikuwa na jumla ya kuku milioni 98 ambapo wakulima wadogo walikuwa na kuku milioni 85.5 na mashamba makubwa yalikuwa na kuku milioni 12.5.

Mheshimiwa Spika, pamoja na idadi hiyo kubwa ya mifugo, mchango wa sekta ya mifugo na uvuvi wa asilimia saba bado ipo chini sana na tija ikiboreshwa kuna fursa kubwa ya sekta hii kuchangia sehemu kubwa ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mifugo na uvuvi ni utajiri mkubwa, lakini pamoja na ukuaji wa asilimia tano, na Tanzania kuwa nafasi ya tatu kwa nchi za Bara la Afrika, na kuchangia asilimia saba katika uchumi wa Taifa, sekta hii ya mifugo na uvuvi inazalishwa kwa tija ndogo sana. Katika hali hii, sekta ya mifugo haijamsaidia mfugaji na mvuvi kwa kiasi kikubwa kunajinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua zaidi ili kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi ikiwemo ujenzi wa mabwawa, kuwezesha mashamba ya kuzalisha lishe/chakula cha mifugo, kuwezesha sekta binafsi kuzalisha mitamba ya kisasa na vifaranga wa samaki. Napendekeza Serikali ianzishe vitalu vya mifugo katika Kata za Mjele na Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ikiwemo kuchimba mabwawa na visima.

Pia napendekeza kuwezesha kuanzisha mashamba makubwa ya kuzalisha lishe ya mifugo ikiwemo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali imalizie kujenga Kiwanda cha Nyama cha Utengule (Mji wa Mbalizi) ambacho kwa muda mrefu ujenzi umesimama pamoja na kuwepo vifaa vyote muhimu vilivyotolewa na wafadhili. Kutokana na kuwepo uwanja wa Kimataifa wa Songwe ambao ni wa kimkakati kusafirisha mazao ya kilimo na mifugo kwa masoko ya nje, napendekeza umaliziaji wa kiwanda hiki cha nyama na pia uwezeshaji wa vitalu vya kunenepesha mifugo katika Kata za Mjele na Mshewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze Maafisa Ugani; waliopo kwenye Halmashauri ya Mbeya ni wachache na wale waliopo hawaonekani kutoa huduma za ugani kwa wananchi. Wizara iweke msukumo wa kuhamasisha, kuanzisha na kutoa elimu kuhusu kilimo cha malisho ili kuwezesha malisho kutosheleza mifugo mwaka mzima na pia kwa soko la nje ili isaidie mapato ya fedha za kigeni.

Pia Serikali iongeze kasi ya uzalishaji wa mitamba kutokana na idadi ndogo ya ng'ombe wazazi kwenye mashamba ya Serikali na matumizi madogo ya teknolojia ya uhimilishaji kwa kutumia mbegu bora za mifugo. Kuwepo na mkakati wa kuongeza mazao ya uvuvi ikiwemo *deep sea fishing* ili kuwezesha samaki wapatikane kwa tija na kuwezesha ushindani kwa soko la nje. Vijana wenye nia thabiti na wanaopenda kujishughulisha na ujasiriamali wa ufugaji samaki kwenye mabwawa watambuliwe na uwekwe utaratibu maalum wa uwezeshaji kupitia Halmashauri zao kupata mitaji na utaalam wa kufuga samaki kwenye vizimba na mabwawa na hivyo kuweza kujiajiri wenyewe na kujipatia kipato. Serikali ishughulikie changamoto ya chakula cha samaki na uhaba wa

vifaranga hapa nchini. Vijengwe vitotoleshi vingi katika vituo vya ukuzaji viumbe maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri inayofanyika katika hii Wizara na kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyoendelea kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi kwa kuwaongezea bajeti, kuwawezesha vijana na uboreshaji wa huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, mifugo; katika Mkoa wa Kagera shughuli kuu za uzalishaji ni kilimo, ufugaji na uvuvi. Ng'ombe wengi zaidi wanafugwa na watu binafsi. Kwa kuwa asilimia 90 ya eneo la malisho tayari limetumika, hivyo napendekeza yafuatayo:-

Kwanza, wafugaji/wawekezaji waliopewa vitalu, watenge maeneo, walime majani malisho; pili, wapewe elimu ya namna ya kulima majani/malisho; wawezeshwe kupata mbegu bora na *NARCO* iwezeshwe kuwa na matrekta na mitambo ya kulimia mashamba, wapewe mitambo ya kuvuna na kufunga majani ya malisho, ili sasa *NARCO* iwe inawakodisha wawekezaji mitambo, walime na kuuza majani ya malisho kwa wafugaji wengine hasa katika kipindi cha ukame/kiangazi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera una Ranchi za Serikali tano, ya sita ambayo ni Mwisa II bado mchakato wake haujakamilika. Mwisa II ina ukubwa wa hekta 66,215.76. Vitalu tayari vilikwishakatwa, lakini wawekezaji hawajamilikishwa. Eneo hili likianza kufanya kazi litawezesha uwepo wa kiwanda cha

nyama na kiwanda cha maziwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mchakato wa Mwisa II?

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na migogoro mingi kati ya wananchi na wawekezaji waliopewa vitalu vya *NARCO*, kwa sasa migogoro mingi ilikwisha na imebaki katika eneo moja la Ranchi ya Kagoma; kati ya wakulima na wafugaji hakuna amani, wameanza na kuuana. Serikali ina mpango gani wa kuwagawia wananchi/wakulima maeneo na wawekezaji wakapatiwa ili kurejesha amani katika eneo hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi; mkoa una fursa nyingi za uvuvi na soko la samaki ni kubwa humu nchini na Congo, Zambia, Malawi na South Sudan. Pia kuna fursa za uwekezaji katika viwanda vya uchakataji samaki, viwanda vya chakula cha samaki, *cold rooms* na mitambo ya kukausha dagaa.

Mheshimiwa Spika, vilevile mkoa una maziwa madogo madogo yanayoweza kutumika, wakapandikizwa vifaranga vya sato au kambale na kuwakuza, kuwavuna na kuwauza katika soko kubwa la samaki lililopo nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mradi wa ufugaji wa vizimba katika Ziwa Victoria. Kuna maeneo mengi yanayofaa kwa ufugaji wa vizimba ambayo ni Kashenye - Missenyi, Rubafu - Bukoba Vijijini, Bumble, Ikondo, Kabasharo Kimwani, Kabunyora ya Runazi na Ikuza yakiwa katika Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuwezesha maeneo hayo kupimwa na kupatiwa vibali vyote vinavyotakiwa (Ardhi, *NEMC, TAFIRI*). Gharama zake ni kubwa, zingewashinda wananchi/vijana/wawekezaji wengi, lakini Serikali imezibeba.

Mheshimiwa Spika, napendekeza ugawaji wa maeneo ya kuweka vizimba uzingatie pia kuwapatia maeneo ya kufugia vijana wetu wanaoishi karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maeneo ya Rubafu (Bukoba Vijijini) tayari mwekezaji amepatikana. Je, ni lini mchakato utakamilishwa, watu wakapewa maeneo na wakaanza kufuga samaki kwenye vizimba ili kuinua kipato cha hao wananchi na Taifa?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba kujengewa majosho katika Kijiji cha Nyaburundu, Mekomariro, Nyansirori, Nyangere, Hunyari, Sanzate, Rakana, malambo mawili Nyaburundu na Rakana.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ilemela asilimia 87 ni maji, nchi kavu ni asilimia 13 tu, hivyo uchumi wa Ilemela kwa kiasi kikubwa wanategemea rasilimali za majini hususani Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, maombi; akina mama wengi wanaofanya bidhaa ya dagaa wanahitaji vifaa vya kukaushia dagaa tofauti na sasa wanakausha dagaa katika mazingira yasiyoridhisha.

Mheshimiwa Spika, vijana wanahitaji mashine za boti kwa ajili ya uvuvi katika maji yenye kina kirefu na vizimba kwa ajili ya ufugaji samaki wa vizimba.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu wake Mheshimiwa Ernest

Silinde, taasisi zilizopo chini ya Wizara na wataalam wa Wizara na wadau wa sekta hizi kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyochangia mwaka jana kwenye kipindi cha bajeti, Mkoa wa Kilimanjaro una fursa nyingi za kufuga aina mbalimbali za wanyama kama vile ng'ombe na mbuzi wa maziwa na nyama, kondoo, nguruwe, sungura, kuku, bata na samaki kwa kutumia rasilimali zilizopo. Tunaiomba Serikali ipeleke teknolojia bora za ufugaji wa wanyama hawa katika Jimbo la Moshi Vijijini, kwani kwa kufanya hivyo tutaongeza tija katika uzalishaji na kuwaongezea wafugaji kipato na kulisaidia Taifa kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya mlimani (Kilimanjaro) yanaweza kutumika kwa ufugaji wa ndani *(zero grazing)* kwa ng'ombe wachache na mbuzi wa maziwa, nguruwe, sungura, kuku na bata. Katika maeneo haya, tunaiomba Wizara ifikirie kupeleka mbegu bora za wanyama wanaofugwa na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, eneo la ukanda wa tambarare kwenye Kata za Arusha Chini na Mabogini lina wafugaji wa Kimasai na lina uwezekano wa kuzalisha kwa tija ng'ombe, mbuzi na kondoo wa nyama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za wafugaji wa Jimbo la Moshi Vijijini, aina za kienyeji za wanyama (ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kuku) wanaofugwa ni kikwazo kikubwa kwenye maendeleo ya sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi inaweza kuwapatia wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini kipato kikubwa iwapo itaendelezwa. Hili litawezekana ikiwa wananchi watapatiwa mafunzo ya kitaalamu ya jinsi ya kufuga na kukuza samaki kwa kutumia teknolojia ya mabwawa. Ufugaji endelevu wa samaki

unaweza kutatua changamoto za umaskini kwa kuwaongezea kipato na kuchangia kikamilifu kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Arusha Chini kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu, wavuvi wanaweza kusaidiwa na Maafisa Ugani wa Uvuvi mbinu bora za ufugaji wa samaki, ikiwepo matumizi ya vizimba. Uwekezaji wa vizimba unaweza kufanyiwa majaribio kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa na nyama, kondoo, nguruwe, sungura, kuku, bata na samaki katika Jimbo la Moshi Vijijini, ninaishauri Wizara itusaidie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naishauri Serikali iwe na programu maalumu ya kuzalisha mitamba wa maziwa wenye sifa zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na mifugo mingine kama mbuzi wa maziwa, ng'ombe wa nyama, nguruwe na kuku. Wafugaji wengi hawana mbegu bora za ng'ombe na mbuzi wa maziwa. Kwa ujumla, huwa wanabahatisha.

Mheshimiwa Spika, pili, naishauri Serikali ihamasishe kuanzishwa kwa vikundi vya ushirika wa wafugaji mifugo na samaki ambavyo itakuwa rahisi kuwapatia huduma za mitaji na utaalamu.

Mheshimiwa Spika, tatu, naishauri Wizara ianzishe mashamba darasa ya samaki Jimboni Moshi Vijijini kwani kuna rasilimali nyingi za maji katika maeneo yote jimboni. Hii ni pamoja na kuanzisha kituo cha kuzalisha vifaranga wa samaki ili wafugaji wavipate kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, nne, naishauri Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Moshi, wawezeshe kupandikiza vifaranga bora vya samaki katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, kwani

wavuvi waliniambia kwenye kampeni kuwa samaki wamehama, ikiwa na maana kuwa wamepungua.

Mheshimiwa Spika, tano, napendekeza Serikali ifanye majaribio ya kuweka vizimba kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuongeza tija kwenye ufugaji wa Samaki; na sita, naishauri Serikali iwekeze kwenye kujenga majosho ya kuogesha mifugo katika maeneo ya Kata za Arusha Chini na Mabogini zenye uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kiplomasia, kisiasa, amani na utulivu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi ilivyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Kamati yetu na watendaji wake wote kwenye Wizara hii kwa ujumla. Kwa kweli mambo mengi yaliyoshindikana muda mrefu yamefanyika sana katika jimbo langu, kwa mfano mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Tlawi Endayaya katika Halmashauri ya Mbulu Mjini ulifanyiwa usanifu toka mwaka 2003 lakini tunashukuru Serikali sasa unajengwa kwa shilingi bilioni saba.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja la Gunyoda ulikuwa kilio cha wananchi wa halmashauri ya Mbulu Mjini, Karatu na Mbulu Vijijini mwaka 1998 lakini sasa imejengwa kwa shilingi bilioni 1.4.

Kuhusu ujenzi wa barabara ya lami kutoka Karatu, Mbulu Mji, Haydom, Sibiti mpaka Lalago mradi huu unaounganisha majimbo matano ya Karatu, Mbulu Mjini, Mbulu Vijijini, Mkalama na Meatu unajengwa na Kampuni ya Kichina sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kila sekta kazi kubwa sana imefanyika kwa lengo la kutatua kero za wananchi na maombi ya muda mrefu, hakika tuliadi wakati wa uchaguzi kupitia ilani yetu ya CCM na tumetekeleza.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, Serikali iangalie utaratibu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kama zinavyoombwa ili tuweze kuona tija ya uzalishaji katika Wizara hii muhimu sana kwani takwimu ya mifugo tulionao ni wengi sana, lakini tija ya kiuchumi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie mpango kabambe wa mafunzo na mikopo kwa ajili ya vikundi vya wafugaji na wasindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi kwa lengo la kuleta mageuzi makubwa ili kuleta tija kubwa zaidi kiuchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie wawekezaji wadogo watakaoanzisha ranchi ndogo ndogo na mabwawa ya kufugia samaki katika ngazi za tarafa na kata, hali hii itawabadilisha wafugaji wengi kuona umuhimu wa kufuga mifugo wachache wenye tija badala ya kuthamini idadi kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie matumizi sahihi na muhimu kwenye vituo vya mafunzo na zana za kilimo zilizojengwa toka mwaka 2013 kwa kuwapeleka wataalam na kuanzisha kalenda ya mipango kazi zao kulingana na maoni ya wafugaji na wavuvi. Wizara iangalie usimamizi na uendeshaji wa majosho ya mifugo na maeneo ya minada ya mifugo uwe chini ya Maafisa Ugani wa Mifugo badala ya kuziachia Serikali za Vijiji na Mitaa kwani tunazidi kusababisha uharibifu na kupoteza ukubwa wa maeneo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Wizara itoe fedha za ujenzi wa majosho kumi katika Halmashauri ya Mbulu Mjini kwenye Kata za Tlawi, Gunyoda, Gehandu, Bargish na Marang ambayo niliomba kwenye barua yangu kwa Katibu Mkuu mwezi Februari, 2023 kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo kwangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiw Rais kwa kazi nzuri katika maboresho ya sekta zote.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri kwa kipindi kifupi katika nafasi hiyo; na tatu, kumekuwepo na jitihada ya kuboresha Chuo cha Uvuvi Mikindani, Mtwara ambapo Serikali ilipeleka fedha za kujenga maabara na madarasa, bado samani ili kozi za muda mrefu ziendeshwe. Kwa sasa kuna programu ya atamizi ambayo imekuwa na manufaa sana na wanafuika wamefurahia kujifunza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuharakisha mchakato wa kukamilisha kozi ndefu kwenye Chuo cha *FETA* Mikindani, Mtwara.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kukamilisha mchakato wa muundo wa watumishi wa Vyuo vya *FETA* ambapo mpaka sasa kwa mfano Meneja wa *campus* ya Mikindani, Mtwara amekaimu kwa miaka 13 sasa pamoja na vyuo vingine vya Gabimori, Rorya, Kibirizi, Nyegezi Mwanza lakini pia Wakurugenzi wanakaimu na hawajatambuliwa na utumishi jambo ambalo linaondoa ari na ni kinyume na taratibu za utumishi.

Mwisho narudia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha programu ya atamizi ya miezi mitatu kwa wahitimu mafunzo ya uvuvi ili waweze kujifunza kwa vitendo.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Ernest Silinde, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia fursa hii kuchangia Bungeni kwako Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia nianze kwa shukrani. Moja nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ametukabidhi kwa sasa. Vilevile nimshukuru sana Makamu wa Rais kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Miongozo ambayo amekuwa akitupatia muda wote kuhakikisha kazi za Serikali zinakwenda kama ambavyo Mheshimiwa Rais anakusudia na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu nikushukuru wewe binafsi umekuwa ukituongoza vizuri ndani ya Bunge lako Tukufu. Umekuwa ni Spika wa mfano na tumekuwa tukijivunia wewe kwa kazi njema ambayo unaifanya katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho na kwa umuhimu wa kipekee nimshukuru Waziri Ulega ni mtu rahimu, mtu mwema, Waziri anayesikiliza. Nimefanya naye kazi kama wakati akiwa Naibu Waziri na katika kipindi kifupi nimefanya naye kama Waziri. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kama tuna Waziri ambaye anaweza kusikiliza, nikishirikiana na Mheshimiwa Ulega tunaamini Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi tutaibadilisha kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira yetu kupitia Wizara hii ni kuhakikisha tunamsaidia Mheshimiwa Rais, moja katika kuongeza wigo wa ajira nchini kupita Sekta ya Mifugo pamoja na Uvuvi. Hayo ndiyo moja ya lengo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaongezaje ajira kupitia Sekta ya Mifugo na Uvuvi? Mmeona katika Hotuba yetu tumeandika hapa na tumeanza utekelezaji katika Mwaka wa Fedha ambao huu tunaimalizia 2022/2023. Tumekuja na *program* za vituo atamizi vyenye lengo la kutoa ajira kwa vijana kwa kuwapa mafunzo ya ufugaji kwa vitendo na *program* hizo mmekuwa mkiona tukizizindua, mmekuwa mkiona viongozi wakubwa wakienda tukiwaonyesha dira ya wapi tunataka Sekta ya Mifugo ielekee.

Mheshimiwa Spika, katika awamu iliyopita tulianza na vituo vichache na katika Bunge lako Tukufu Wabunge wengi wakati wanajadili wamekuwa wakisema kwamba vituo ni vichache wanataka ongezeko la vituo ili mafunzo kwa vitendo kwenye Sekta ya Mifugo yaweze kuongezeka. Jambo hilo

tumelipokea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa hivi tuko katika mazungumzo na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba tunakuwa na vituo atamizi kila Mkoa ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu tunawaongezea wigo lakini vilevile watu wapate maeneo ya karibu ya kwenda kujifunza na kupata elimu ya vitendo ya ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ndiyo moja ya malengo yetu ambayo tunakwenda kuyatekeleza katika mwaka wa fedha unaokuja. Jambo jingine tutaongezaje wigo wa ajira? Ni kwa kuendelea kutoa mikopo ya masharti nafuu ambayo inatokana na mikopo ya *Extended Credit Facility* kwa maana ya *ECF* ambayo tunaipata kutoka *IMF* na mikopo hiyo tumeielekeza katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya ununuzi wa boti ambazo tutakwenda kuzitoa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu tumeonyesha hapa na tumeyaelezea hapa tutatoa boti 158 ambazo zipo katika hatua ya mwisho ya ujenzi wake. Kwa hiyo, kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu Wizara ya Mifugo na Uvuvi itafanya zoezi hilo na litatangazwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunatoa boti hizo kwenye maeneo ya wavuvi? Moja ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye aliagiza zinunuliwe boti hizo kwa lengo la kuongeza ajira kwa wavuvi lakini vilevile kuongeza uzalishaji wa mazao ya samaki na viumbe maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ni sehemu ya malengo ambayo sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Waziri wangu *Comrade* Ulega tumedhamiria kwenda kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tumesikia maoni mengi na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge wakati wanajadili hapa wakizungumzia mchango mdogo wa Sekta ya Uvuvi vilevile Sekta ya Mifugo katika uchumi katika Pato letu la Taifa. Moja ya nia yetu thabiti kabisa ni kutaka kuona mifugo ikichangia pato zaidi ya ambavyo inachangia sasa, vivyo hivyo katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika moja ya malengo ambayo tumejiwekea ni pamoja na lengo hili na ndiyo maana hata mchango wa mwisho wa Mheshimiwa *Professor* Muhongo wakati anaelezea hapa anasema sasa hivi tuje na mpango wa vizimba. Ninyi wote ni mashuhuda mpango huo sasa umeanza kutekelezwa katika baadhi ya maziwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini tunaleta huo mpango? Lengo ni kuongeza uzalishaji wa samaki lakini vile vile utasaidia maziwa yetu yaani kwa maana ya hizi *water bodies* ambazo zipo zitakuwa na fursa ya kupumua wakati ule ambapo yatakuwa yamefungwa. Kwa hiyo, hayo ndiyo malengo ambayo sisi tumekuwa tukijiwekea na tunaamini kwamba tutayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu Mheshimiwa Waziri wakati tunajadiliana amenielekeza niwaeleze Bunge lako Tukufu kwamba sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi; moja hatutachukulia ufugaji ama uvuvi kama kero kwa Taifa letu. Kwa hiyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haitakuwa *treated* kama Wizara ya Migogoro na ndiyo maana tunaruhusu Wabunge kuleta maoni wakati wowote siyo wakati wa Bunge peke yake ama wakati wa bajeti. Tunaruhusu maoni, tunaruhusu ushauri ili kuhakikisha kwamba tunajikwamua katika mawazo yale ambayo yalikuwepo hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ni sehemu ya malengo makubwa ambayo sisi tumejiwekea kuhakikisha kwamba baada ya mwaka mmoja tunaamini kuna jambo tutakuwa tumepiga hatua kubwa katika kuisaidia Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba moja ya jambo kubwa tutakalolitilia mkazo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni pamoja na kufanya tafiti nyingi zaidi za kitaalamu na ambazo zinatekelezeka ili tuweze kubadilisha mtazamo mkubwa ambao ulikuwepo hapo nyuma kwenye Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tuanaamini kwamba mifugo pamoja na uvuvi ni utajiri kinachohitajika ni nia thabiti ya kutekeleza na kubadilisha hii Wizara kutoka katika mitazamo ambayo ilikuwepo hapo awali. Sisi tunaamini hivyo na linawezekana. Hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi siyo Wizara ndogo kama watu wanavyokuwa wakiifikiria. Ni Wizara kubwa ina malengo makubwa na tuna uwezo wa kufanya mabadiliko makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwa Bunge lako tukufu kwamba tunawaomba mkubali kutupitishia Bajeti yetu siku hii ya leo halafu baada ya mwaka mmoja mje muone matokeo ya kazi nzuri ambayo sisi tunaamini tutaifanya kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ni sehemu tu ya mambo ambayo sisi tumekusudia kuyatekeleza katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema maneno hayo machache, nikushukuru sana ninaunga mkono hii hoja ipite kwa 100% ili tukafanye kazi kwa sababu kazi tumeaminiwa kuifanya

na tunaiweza na tunaamini kabisa kwa ushirikiano wa Bunge lako Tukufu jambo hili liko ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na Mwenyezi Mungu akubariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja niwaombe sana yale majadiliano tunayoendelea nayo ambayo ni ya muhimu sana kwenye Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi tupunguze sauti kidogo ili tumsikilize Mheshimiwa Waziri akijibu hoja zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega mtoa hoja uje uhitimishe hoja yako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na mwingi wa ukarimu kwa kupata fursa kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu na kutoa mchango wangu katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu ya kunipa nafasi kuhudumu kama Waziri wa Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa na pia naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaoonyesha katika kuliendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi *Comrade* Mheshimiwa David Ernest Silinde kwa kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii, bajeti ya *protein*, bajeti ambayo imepata wachangiaji wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa hoja zilizowasilishwa hapa na kuchangiwa kwa vyema sana na michango mizuri sana ya kina yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, mifugo na uvuvi ni utajiri. Kupitia michango mingi iliyotolewa na Wabunge, takribani Wabunge 54 waliochangia kwa maneno ya kuzungumza Bungeni na wachache waliochangia kwa kuandika inathibitisha juu ya ukubwa na umuhimu wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha katika michango hiyo imedhihirika wazi umuhimu wa kuimarisha Wizara kupitia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayoongoza Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sekta ya Uvuvi pia imepanga kutekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha uchumi wa buluu kwa kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinasimamiwa ipasavyo ili kuwa na uvuvi na ukuzaji viumbemaji endelevu, maendeleo ya viwanda, ukuaji wa kipato cha mtu mmoja mmoja na Pato la Taifa kwa ujumla kwenye maji baridi na maji chumvi na kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo ni dhahiri kuwa masuala ya kuendeleza malisho, ajira kwa vijana, mauzo nje ya nchi, utafiti wa mifugo ikiwa ni pamoja na kuendeleza kosafu bora za mifugo ni ya umuhimu katika kuongeza tija

katika uzalishaji wa maziwa na nyama, mayai na ngozi, kuendana na mnyororo wa thamani na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa hoja mbalimbali kuhusu Wizara ambapo jumla ya Wabunge 54 kama nilivyokwisha kusema wametoa michango yao. Kuna waliotoa maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni na wengine kwa maandishi. Naomba sasa wote hao niwatambue kama ambavyo watakavyokuwa wamesomwa katika risala yangu.

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge niliowataja katika risala ilikuwa ni mizuri sana na iliyosheheni busara, hekima na changamoto. Aidha siyo rahisii kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi nilionao hapa katika membari hii. Ninaahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo umezingatiwa. Hata hivyo ningependa nitumie muda mfupi nilionao kujaribu kutoa ufafanuzi katika baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ziko hoja mahususi kadhaa zilizozungumzwa hapa. Nikianza na upande wa mifugo. Katika upande wa mifugo iko hoja iliyozungumzwa juu ya hereni. Serikali ilianza kulitekeleza zoezi hili kupitia Wizara ya Mifugo na Uvivu na baada ya utekelezaji iligundulika kwamba yako makosa ambayo tuliyatekeleza kwa wakati ule. Na kwa hekima na busara za viongozi wetu wakaitaka wizara irejee, ifanye tathmini ijiridhishe kama ushirikishwaji umefanywa sawasawa; tuangalie juu ya bei, juu ya ubora wa bidhaa zile.

Mheshimiwa Spika, kazi hii sasa tumekwishakufika mwisho; kwa maana ya kwamba tumepata yale yote ambayo Serikali imeelekeza, kwa maana uongozi wetu umeelekeza maana maelekezo haya yalitolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge hili Tukufu. Baada ya kutoa maelekezo yale Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilichukua hatua sawa na maelekezo yale. Na hapa, ingawa kule mbele nitaendelea pia, nataka nieleweshe, maana yupo mmoja katika wachangiaji, Mheshimiwa Luaga Mpina, amezungumza kuwa maelekezo yanayotolewa na viongozi wetu, akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu, na amemtaja haswa yeye mahususi, kwamba hayafanyiwi kazi. Kufanyiwa kazi kwa jambo hili la hereni, kwa maana ya tathmini na kujiridhisha juu ya bei na juu ya uwezo wa zile hereni zenyewe ni moja ya ushahidi wa kwamba viongozi wanapoelekeza hufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nitakuja hapa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, ya kwamba katika mkakati wetu wa utekelezaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, la kwanza kwenye kwenda kuitekeleza sheria hii kwenye bajeti hii tuligundua kwamba tuna jukumu la kuwashirikisha ipasavyo Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine wote. Ninawaombeni kwa heshima kubwa na taathima tukubaliane ya kwamba leo tupitishe bajeti hii kisha tuanze *engagement* kati ya Wizara na ninyi viongozi. N mawazo yenu yote tutayachukua kwenda kuboresha zoezi hili. Nataka niwahakikishie litakwenda kuwa zoezi zuri sana litakalokwenda kuinua uchumi wa wafugaji, uchumi wa Taifa letu na mchango chanya wa hili Taifa. Msiwe na wasiwasi wowote, sisi ni watu wasikivu na ni watu ambao tuko tayari kushirikiana nanyi Wabunge wetu ipasavyo kabisa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine mahususi ambayo ningependa kuzungumza hapa ni hoja ya malisho. Nimesema katika bajeti ya kwamba tumetenga fedha za kuhakikisha mashamba yanayomilikiwa na Serikali ambayo yaliyojaa nchi

nzima na kwa kiasi kikubwa yamekuwa ni mapori, na Waheshimiwa Wabunge mmesema hapa. Nataka niwahakikishieni ya kwamba moja ya jukumu kubwa tutakalokwenda kufanya ni kuyafanya mashamba yale yawe ni mashamba ya uwekezaji na uzalishaji ili yaweze kuwa na tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tunazo njia mbili kubwa za kufanya, njia ya kwanza ni kwa kutumia fedha zetu wenyewe ambazo tumeziweka katika bajeti na njia ya pili tutafungua milango ya uwekezaji. Nilishasema katika Bunge ikiwa wewe Mbunge, ikiwa unaye mwekezaji yeyote mlete Wizarani atuambie andiko lake, alete *business plan* yake, alete mpango wake sisi tuko tayari kutoa ushirikiano tuzalishe.

Mheshimiwa Spika, mathalani kule Ruvuma tumechagua ni eneo la uzalishaji wa mahindi aina ya mahindi ya njano *(yellow corns)*. Kwa muda mrefu sasa mifugo kama vile wazalishaji wa kuku wamekuwa wakihangaika; inapofika kipindi cha kiangazi huwa wanapata tabu sana namna ya kupata mahindi. Mimi na wenzangu wizarani tumeshauriana na tumekubaliana mashamba ya upande wa kule tuliyonayo pale Hanga, Ngadinda na kwingineko, Songea kule tunakwenda kuzalisha *yellow corns. Yellow corns* hii itakwenda kwa ajili ya kutengeneza uhakika wa chakula cha kuku na mifugo mengine. Kwa hivyo niwahakikishieni jambo hili tunakwenda kulifanya; na kwa mara ya kwanza Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumetengeneza mpango wa kwamba sio kwa kutegemea mvua tena, tunakwenda kufanya *mechanization* tunakwenda kumwagilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunafikiria kwamba hata nyasi imwagiliwe, sio mahindi tu na mpunga hata nyasi tuzimwagilie, hayo ndio mawazo tuliyonayo. Mmoja katika ya Waheshimiwa Wabunge humu amesema kwamba kwanza tosheleza chakula

cha ng'ombe wako hapa nyumbani.; ni ukweli tutatosheleza chakula cha hapa nyumbani. Lakini niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sitaki kusema maneno mengi; angalia leo hii chakula cha mifugo inayolishwa kule Asia kwa kiasi kikubwa sana ilikuwa inatoka Sudan na jirani zetu wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, kama hatutaweza kutumia tena fursa hii sisi Watanzania leo haitatokea tena wakati mwingine. Kila mmoja hapa anajua matatizo yanayowapata majirani zetu, hii kwetu sisi ni fursa. Wamekuja, mimi nimempokea hapa Waziri wa Kilimo wa kutoka Saudia nimekaa naye, walikuwa wanachukua nyasi kutoka Sudan, moto unaowaka kule sitaki kusema kwa nguvu sana hapa Bungeni. Hiyo kwetu ni fursa tutapata *forex*, tutapata fedha za kigeni tutatumia hiyo kama ni ajira ya watu wetu. Kwa hivyo ni ukweli kwamba ng'ombe wetu hapa nyumbani huwa wanahainga. Nilisema, kwamba tunataka tuone gari zinatoka sehemu moja zinakwenda sehemu nyingine zikiwa zimebeba nyasi. Kama vile ambavyo tunatoa mahidni kutoka sehemu moja kupeleka kwa wahitaji na ndivyo hivyo tunataka tufike katika hatua ya kuchukua nyasi kupeleka Kiteto, Simanjiro ili ile mifugo ya kule Lungido iweze kuokolewa. Ndugu zangu inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikwenda Simanjiro na *Comrade* Ole-Sendeka, na nilikwenda Kiteto na rafiki yangu *Comrade* Olelekaita, niliwashuhudia ng'ombe wakati wa ukame mkali wakinyweshwa uji, *yes*, ndiyo, kwa ajili ya kutafuta *survival.* Na sisi binadamu tumekuwa tukijinusuru kwa kupelekeana mahindi ya nafuu. Nasema hivi tunakwenda sasa katika *mechanization* tutazalisha majani ya kutosha kama tunajihami tutawahami na mifugo yetu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa jambo la *vaccination* hapa, kwa maana ya chanjo. Chanjo ni muhimu sana. Ili tuuze

ng'ombe wetu vizuri chanjo na herein, kwa maana ya kuitambua mifugo yetu ni jambo la muhimu. Yuko ndugu yangu mmoja pale Mwanza anaitwa Chobo; alikuwa anauza nyama kule *UAE;* Chobo amekataliwa kuuza nyama Uarabuni hivi sasa, hauzi tena. Kiwanda kiko kizuri sana pale ni kwa sababu ya vitu hivi. Sisi tumedhamiria, kabla hatujakwenda huko nitakaa na Waheshimiwa Wabunge wote, kila mmoja anajua ana hoja yake, kwa nini anasema isiwe hereni, milango yangu iko wazi. Tutahakikisha tunakaa tunakubaliana, tutakwenda na *campaigns* za uhakika ambazo hazitatuletea taharuki ya namna yoyote.

Mheshimiwa Spika, nataka tutoke katika kuuza tani 12,000. Kwa nini sisi tuzalishe nyama tani 800,000 zinatutosheleza humu nyumbani, kwa nini hatuuzi tani 100,000 nje ya Taifa letu wakati uwezo wa kuuza na masoko yako makubwa sana? Ndugu zangu kupanga ni kuchagua, tunapata tupate *forex,* tupate ajira za watu wetu, tupate uchumi mkubwa. Yako mambo ni lazima tuyafanye ili kusudi tukubaliane hii mifugo yetu iweze kutunufaisha na inufaishe Taifa letu. Hii *GDP* inayochangiwa hivi sasa kwa asilimia nane ninawahakikishieni kama kuna nafasi nzuri na rahisi ya kuinua ni katika mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Mungu Mkubwa sana Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatutengenezea njia rahisi sana kwa diplomasia kubwa sana ya uchumi. Wanenepeshaji wa ng'ombe, wale wa mbuzi, wale wa kondoo na wengine tukae mkao wa utayari. Nataka niwahakikishieni hatutakwenda katika zoezi lolote baada ya bajeti hapa, tunatengeneza *engagement plan na implementation plan* ya uhakika. Waheshimiwa Wabunge wote msiwe na wasiwasi. Wale mliokuwa mnakusudia kuchukua shilingi yangu kwenye jambo hili naomba kabisa kwa uhakika wala msiwe na wasiwasi huo, manake tutakaa na mambo yatakuwa mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusiana na wakala, na hii inahusiana na miundombinu ya mifugo kila Mbunge anataka josho, kila Mheshimiwa Mbunge anataka rambo, kisima kirefu cha maji, kila Mbunge angependa awe na bwawa la mifugo na akitazama anaiona bajeti ya Waziri wa Mifugo imetengeza marambo manane tu kwa mwaka. *Way forward* mmeitoa ninyi wenyewe, mmesema hapa, na nimewasikieni, kuanzia kwenye kamati ya Bunge iliyowasilisha hapa na kuja kwa Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja mmesema hapa. Kwamba Wizara inasimamia miradi kutokea Dodoma. Bwawa linajengwa Kiteto kwa Mheshimiwa Olelekaita, bwawa linajengwa kule Simanjiro, bwawa linajengwa kule Longido, bwawa linajengwa kule Mkuranga ndani Mkurugenzi yuko pale Dodoma peke yake na *engineer* wayasimamie yale.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamesema, kwamba, hapa tunalo jambo la kufanya, na katika jambo la kufanya mnadhani ya kwamba tutengeneze wakala. Waheshimiwa Wabunge, wafugaji wenzangu nataka niwakumbusheleo hapa, kwa ufupi sana. Watu wa kilimo kupitia Tume ya Umwagiliaji wamepata fedha nyingi sana ninyi, nyote ni mashahidi na mmepitisha nyie wenyewe hapa. Zile *schemes* za umwagiliaji wakulima watakaokuwa wanatumia watakuwa wanachangia nadhani tunaelewana hapo. Sisi binadamu, nimetoa mifano ya *RUWASA,* yale maji tunayoyatumia sisi tunachangia. Ninafahamu, ndiyo maana mkasema tupate wakala. Ninawajua wafugaji, nimekaa nao miaka kadhaa sasa, wako tayari kuchangia lakini katika mambo ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, hoja hii inatosheleza kuwaambieni ya kwamba tunalichukua jambo hili ndani ya Serikali tunakwenda kulianzishia harakati zake. Tutali-*fast track* tukipata baraka *Inshallah Ta'ala* jambo litakuja litapita lita-*solve* matatizo ya watu wote hapa. Ninyi leo kazi yenu ni nyepesi sana tu,

nakuombeni kwa heshima kubwa na taathima tena kwa mara nyingine nipitishieni muone mchakamchaka utakaopigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende katika uvuvi; limesemwa jambo kwa mapana na marefu sana hapa juu *Lake Tanganyika*. Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma, Rukwa; narudia tena; limesemwa jambo la *Lake Tanganyika* kufungwa. Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma, Katavi na Rukwa wamesema kwa mapana sana na wananchi wamewasikia, na mimi na wenzangu Serikalini tumewasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba itifaki hii ilisainiwa ipo ndani ya Serikali, ilikuwa na lengo jema; lakini itifaki hii haikutulazimisha sisi nchi wanachama ya kwamba namna ya utekelezaji wa ile itifaki ufanane, haikuwa hivyo. sisi hapa katika Ziwa Tanganyika tuna kitu kinaitwa kilimia; mmoja miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge amesema hapa. Kilimia, najua Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Bindyaguze, na Waheshimiwa Wabunge wengine wanafahamu vizuri. Kilimia lile ziwa huwa linajifunga lenyewe *automatically,* hasa kipindi hiki cha baridi. Nimefurahi kwamba Waheshimiwa Wabunge kutoka mikoa hii mmewaleta wapiga kura, wavuvi wenyewe. Ndugu zangu hakuna sababu yoyote ya kupata taharuki.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge nataka niwahakikishieni, kama ambavyo tumewaandalia mkutano kesho; ninafahamu tuna mkutano na wakuu wa mikoa hiyo yote, Waheshimiwa Wabunge wote, wakuu wa wilaya zote, wakurugenzi wote, kwa kuwa hoja ni ushirikishwaji. Wabunge neno hili la ushirikishwaji tunakwenda kulikamilisha kesho pale *St, Gasper,* tunakaa tunajadili. Kwa hiyo hakuna hofu, wala hakuna mtu yoyote apate wasiwasi ya kwamba labda kuna jambo linalohusu kufungwa kwa ziwa. Niwahakikishieni, narudia

tena, *issue* si ni kushirikisha? basi nataka niwaambie mimi kwa heshima kubwa na taadhima na wenzangu kule Serikalini, hakuna jambo tunaloliheshimu kama kuwaheshimu watu ninyi mliopigiwa kura na wananchi. Wanasema sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kilumbe na Waheshimiwa wote, Mheshimiwa Bidyanguze, Mheshimiwa Aida, Mheshimiwa Kavejuru, Mheshimiwa Sylivia, Mheshimiwa Ndalichako, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Kakoso na Waheshimiwa Wabunge wote niwaondoe hofu. Waambieni wana-Tanganyika wavuvi wa Ziwa Tanganyika waendelee na shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Daktari Samia Suluhu Hassan kama mnaona jambo kubwa Mheshimiwa Rais wakati wote amekuwa akilisisitiza kwetu sisi wasaidizi wake ni kutokuleta taharuki. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Amejenga msingi imara wa zile "R" nne, kila mmoja anazijua hapa. Ikiwa yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefungua milango anakaa na kila mtu, anazungumza naye, anapata kufanya *reconciliation* hata; yale watu tuliodhani kuwa ni magumu kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan yamekuwa ni mepesi. Sasa mimi Abdallah Ulega ni nani nisijifunze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika nataka niwaondoeni hofu juu ya jambo hili ndugu zangu. Tunazo njia nzuri sana za kuendea mambo, msiwe na wasiwasi na wavuvi msiwe na wasiwasi, wakati wa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni wakati wa uzalishaji, ni wakati wa kukuza uchumi wetu na hakuna sababu nyingine ya kubabaika. Mifugo na uvuvi ni utajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya mamlaka ya uvuvi ninawaelewa, na Kamati ya Bunge imetuelekeza juu ya jambo hili. Niwakumbushe; katika Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2016 jambo hili limetamkwa, na sisi Serikalini tumelichukua. Tumelichukua kwa sababu tumekuwa tukifanya kila mara *operations.* Ninyi wote hapa mmesema, kila Waziri anayeingia katika Wizara hii anafanya *operation.* Tunachoma nyavu, tunafanya vile lakini inaonekana inakosekana ile *sustainability,* uendelevu unakosekana.

Mheshimiwa Spika, sayansi ya uvuvi inataka tulinde maeneo ya mazalia na makulia ya samaki na ndiyo maana Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 43(f) ikatuelekeza Serikali wazi wazi, kwamba tuhakikishe tunalinda maeneo ya mazalia na makulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mamlaka Mwenyezi Mungu akitujalia *insha Allah* litakwenda kuwa ni mwarobaini mzuri sana. Kwa hivyo kusudio hili tumeanza kuchukua maoni ya Waheshimiwa Wabunge na tutaendelea sisi, tutapitisha katika vikao vyetu vyote vya kiwadau, tutaona linalowezekana kufanyika. Hili unajua *automatically* linakwenda kuondoa hizo hofu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishakuwa umelinda maeneo ya mazalia na makulia una uzalishaji mzuri, kuanzia baharini kule katika matumbawe kuja huku katika Maziwa na mpaka Nyumba ya Mungu, Hale mpaka Jipe, yote hayo yanaingia mle, hapa mambo mbona yatakuwa mazuri sana na uzalishaji utakuwa ni mzuri sana. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wasiwe na wasiwasi wavuvi wenzangu juu ya jambo hili, kwani tumelichukua na tutalipa uzito na tutaona kusudio hili linawezaje kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo mengi ya kusema, lakini haya ndiyo yaliyokuwa mazito. Mengine nitayajibu kwa maandishi. Nataka nimalizie nisichukue dakika zako nyingi. Kwa kuwa nimezungumza juu ya mundombinu ya mifugo na nia yetu kama Serikali, najua wako watu wangependa kuzungumzia minada, wengine wangependa kuzungumzia magomvi kati ya wakulima na wafugaji yaliyosababishwa na mambo ya maji ukosefu wa mabwawa, nafahamu. Najua pia wako watu wangependa kuzungumzia malisho, nimeyasema hapa naomba watuunge mkono ili tukapunguze kero hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua sayansi ya kuondoa hii migogoro ya wakulima na wafugaji, naiona ni nyepesi tushikamane, tutaiondoa, watu waishi kwa amani. Leo najua njia za mifugo huko Wilayani kote njia za mifugo zinajulikana. Kama zinajulikana kupita mle katika zile njia za mifugo kama tunafanikiwa kwenda kutengeneza chombo ambacho kitakuwa kikisimamia ile miundombinu ya mifugo na wafugaji ambao wako tayari tukaenda tukashirikiana nao vizuri, wakawa wanachangia vizuri, sasa ugomvi utatokea wapi? Kama mtu anatafuta maji? Maji si ndiyo haya hapa, kama mtu anatafuta malisho, malisho si ndiyo haya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba hata kaka yangu Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa Mstaafu wa zamani Mheshimiwa Innocent Kalogeris angetamani aishike tena leo shilingi kama alivyofanya mwaka jana, lakini asiwe na wasiwasi, mawazo hayo na fikra hizi zilizotolewa hapa zinatosheleza kabisa kujenga msimamo wa kwamba tunakwenda pazuri.

Mheshimiwa Spika, najua hata rafiki yangu Mgosi Wandima, Mheshimiwa Reuben, angetamani ashike shilingi kwa ajili ya mnada wake pale Handeni Mjini. Kaka suluhisho ni hili hapa, tushikamane hakuna hoja tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwisho, naomba nimalizie kwa maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapa mtani wangu Mheshimiwa Luhaga Mpina juu ya hoja mbili; unajua nilikuwa sitaki kusema, lakini sasa ametaja majina ya wakubwa, nataka nimfafanulie baadhi ya mambo. Hoja ya kwanza kwa sababu amemtaja mpaka Rais ya Awamu ya Tano ile ya kuchoma moto vifaranga. Unajua hizi sheria zinatekelezwa halafu katika utekelezaji wa sheria yako mambo ya busara na hekima, namna ya kufanya vile vitu. Sheria inasema tu–*destroy* kwamba mtu kama amekosea akaingiza vifaranga unatakiwa ku–*destroy,* namna ya ile *destruction,* sheria haikusema uchome moto, uwachimbie katika shimo, uwafanyaje sheria haikusema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugomvi wa pale ulikuwa ni nini? Ni kwa nini vifaranga vichomwe mbele ya macho ya watu? Namshukuru amezungumzia juu ya *animal welfare* (haki ya wanyama), angalia mgongano wa mambo hapo, aliyekosea ni nani? Aliyekosea ni mwingizaji wa vifaranga au vilivyokosea ni vile vifaranga? Sasa kwa nini uvichome moto mbele za watu? *Simple,* kwa hivyo hapa *issue* inawezekana vinachomwa moto kila siku huko, yawezekana kabisa, lakini kwa nini unavichoma moto mbele za watu? Hii ndiyo hoja.

Mheshimiwa Spika, binadamu wameumbwa siyo mnyama, siyo hayawani, binadamu siyo hayawani, viumbe vile vina haki yake na namshukuru amezungumza vizuri wakati alipokuwa akitetea ng'ombe ambao ni kweli Kanuni ile tumeisaini ya kuilinda haki za Wanyama. Sasa haki za wanyama ni pamoja na kutokuwachoma hadharani. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pilli la samaki. Anataka mimi niseme, unajua Mpina mimi nakuheshimu sasa siwezi kusema kila kitu wewe ulikuwa bosi wangu pale Wizarani. Sasa mimi niseme ukweli, mimi ni muungwana, msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo na yeye anajua tumekaa vizuri sana, mimi na yeye pale wakati niko katika *winding up* pale Wizarani kwa namna ambavyo namheshimu, kwanza jana nilimpigia simu Mheshimiwa Mashimba Ndaki, kumuuliza bwana, kesho tunakwenda katika hoja, nimeliona jina lako, vipi Mzee unataka kuchangia? Akaniambia Mheshimiwa Waziri, sina haja ya kuchangia bwana. Akaniambia kwamba yeye atachangia kwenye kilimo, nikamwambia bwana mimi nakutakia kila la kheri kwa sababu nilitaka nijue anataka kuchangia kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo nikiwa na watendaji pale Wizarani, Mheshimiwa Luhaga Mpina, nilimpigia simu niseme ukweli na msema ukweli mpenzi wa Mungu na namfurahia amewataja watendaji wengi wa Wizara ambao na mimi nilikuwa nao pale Wizarani. Sasa hivi kama saa moja tu iliyopita, nikamuuliza bwana mzee nimeona jina lako unataka kuchangia, una jambo lolote nikusaidie? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, akaniambia, hapana bwana. Mimi ni kweli naenda kuchangia, nikamuuliza kuna kheri shehe? Akaniambia ipo kheri kubwa sana wala usiwe na wasiwasi. Sasa simkatalii yeye kuchangia hapa Bungeni kwa kuwa ni haki yake, lakini nataka nimkumbushe ananiambia kwa nini sisemi juu ya rula ilivyotumika pale kantini? Sasa Mheshimiwa Mpina wakati mwingine tunakaa kimya, maana kukaa kimya nako ni busara. Samaki yule akishapikwa anapoteza shepu, anapoteza *size,* sayansi ya samaki haielekei huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, samaki yule aliyempima hapa Bosi wangu wa zamani Mheshimiwa Mpina, alikaangwa, kapita katika nyuzi joto nyingi sana. Kwa hivyo ameshapoteza ile hali yake, yaani ile *physical appearance* yake imepotea kabisa, huwezi kupata uhalisia. Sasa alitaka mimi wakati ule nikiwa Naibu nimwambie Mzee unakosea hapo. Katika hali ya kawaida na nadhani kwa kuwa sikumwambia hivyo wakati ule sikupishana naye, sikugombana naye, ndiyo maana mimi Abdallah Ulega hadi hii leo nipo katika *podium* hapa kama Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mantiki yake ni nini? Mantiki yake ni kwamba, kama ningeligombana nae wakati ule ningeliambiwa mimi ni mkosefu, sina adabu, ni mjeuri, unagombana na bosi wako, labda saa hizi nisingekuwa mahali hapa. Itoshe kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge kwa heshima kubwa na taadhima nawashukuruni sana, ameondoka mke wangu Mama Tulia hapa na furaha kubwa sana kwa sababu amesikia michango mizuri ya pongezi, matumaini, shukurani na kunitakia kheri katika kutekeleza jukumu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaahidi kwamba kazi imeanza. Mtafurahi yaani *show show* vijana wa mjini wanasema, naombeni uungaji mkono wenu hata wale kama nilivyokwishasema waliokuwa wanafikiria kushika shilingi vinginevyo iwe nje ya hoja hizi, lakini naomba waniamini, ninaye Naibu Waziri mzuri sana, *comrade* Silinde. Mheshimiwa Silinde alikuwa akiniheshimu sana toka tukiwa wote Manaibu Waziri hapa sana. Leo hata mimi najua nilipoteuliwa na yeye kuwa Naibu wangu nilijiuliza hee! Hii nchi kweli inaona. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimalizie hizi dakika zangu mbili niwaambie Waheshimiwa Wabunge kidogo; katika Naibu Mawaziri sisi wakati ule nikiwa Naibu Waziri, tuna utamaduni

wetu, kila mahali mnapokuwa wawili, watatu anapatikana kiongozi. Sasa tukakaa Manaibu Waziri tukaulizana nani anakuwa Mwenyekiti wetu? Mheshimiwa Silinde akanyoosha mkono wa kwanza, wote tukiwa Manaibu, akasema ahaa jamani hilo nalo la kuulizana, Mwenyekiti hapa si Abdallah Ulega bwana Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Hiyo nawaonyesha namna ambavyo toka huko nyuma tumekuwa tukishirikiana na kuheshimiana sana. Kwa hivyo, nawapa matumaini, ninaye Profesa Riziki Shemdoe, wote wanamfahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu jamaa Profesa Riziki Shemdoe, ni Mgosi Wandima, kule kwa Lushoto kuna kitu kinaitwa *Muku,* wanajua Wasambaa hapa. *Muku* wanakula watu wa kazi, akila hiyo hachoki kufanya kazi, ndiyo huyu jamaa. Kwa hiyo saa nane ya usiku nikimpigia simu anaitika simu yangu, nikimwandikia meseji yuko hewani. Nataka niwahakikishie, sasa kuna maneno hapa naogopa kuyasema, nikiyasema itakuwa hatari, lakini kwa mchanganyiko huu jinsi ulivyo mzuri ni kama ile timu iliyoingia nusu fainali juzi hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, basi, kwa kuwa naomba nisishikiwe shilingi, niseme tu kwamba ni kama zile timu mbili ambazo zimefanya vizuri sana hapa juzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tunaendelea na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Kamati yako ijielekeze katika Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida. Fungu 99 - Sekta ya Mifugo, ukurasa 619 na katika kishikwambi ni ukurasa 703.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 99 – Sekta ya Mifugo

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*…..............Sh. 4,023,190,570

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mmeshafika wote hapo kwenye vishikwambi vyenu? Mmeshaliona Fungu? Haya Mbunge aliyeona? Ama wote hamjaona bado? Naona wote mna vishikwambi, halafu wengine mnanitazama, sasa sielewi kama kinasomeka huku mbele ama vipi? *Volume II.*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni *Volume II* kama nilivyosema ni ukurasa 703 katika kishikwambi. Kwa hiyo uki–*search* ukurasa 703 utaliona Fungu 99.

**MWENYEKITI:** Haya ukurasa 703. Tayari? haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kilichosomwa kina kina mshahara wa Waziri na naona hapa na majina mengi sasa. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa na Wabunge wengi nikawa nawaona mnapiga makofi kuashiria kwamba mmemwelewa maombi yake, naamini haya majina pengine yalikuja kabla hamjamsikia akihitimisha hoja. Kwa hiyo nikikwita Mbunge na kama majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri umeridhika unaniambia kwa sababu mimi majina nililetewa kabla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jerry William Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi naomba kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu, *alumn* mwenzangu *UDSM* mtaalam wa uvuvi, kuna eneo lilikuwa linamilikiwa na Kabimita kwenye Kata ya Pugu Stesheni eneo la Banguro, eneo ambalo lilikuwa na mgogoro ambao mwaka 2018 ulifika mwisho. Wananchi wa maeneo yale wanaishi kwa taharuki na tarehe 22 Aprili, 2022, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo aliandikiwa barua na Kamishna wa Ardhi kumtaka sasa baada ya kwisha mgogoro ule awasilishe hati ile, namba 4873 ili wananchi waweze kurasimishiwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza maelezo ya Waziri ya mwisho aliyoyatoa kwa ufundi mkubwa ambayo kama angekuwa na maelezo yangu ningeweza kushawishika, lakini sijapata maelezo sasa, naomba Waziri anipe maelezo na nisiporidhika nitaondoka na shilingi ya mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jambo la Mheshimiwa Jerry ni la muhimu lakini ni la Jimboni kwake mahususi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera yetu ya Uvuvi pamoja na mambo mengine imetupelekea tukatunga Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu. Sheria hii Sura ya 383 ya Mwaka 2020 pamoja na Kanuni zake za 2021, ambazo imetuwezesha kutengeneza chombo cha *DSFA (Deep Sea Fishing Authority)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wetu wa Bahari Kuu kwa sasa usimamizi wake ni mgumu sana, meli zinazovua Bahari Kuu kwa sababu ya kukosa bandari ya uvuvi ndani ya nchi, zikishamaliza kuvua zinalazimika kwenda nchi ya Jirani, mathalani Visiwa vya Ushelisheli ambako ndiko kuna bandari huko ndiko wanapofanya *sorting*, kama kuna samaki waliowavua ambao hawakuwaombea leseni ndiyo wanajulikania huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naifahamu meli moja ambayo ikienda inawarudisha samaki wasiohitajika ambao hawakuombewa leseni, lakini sielewi meli nyingine ambazo zinakuwa hazijasajiliwa hapa na haziendi Ushelisheli kwamba zikivua zinamaliza na kuondoka, *control* ya hao samaki ambao wanakuwa wamevuliwa Serikali wanaifanyeje? Kwa maana hiyo pamoja na kuomba ufafanuzi huo ninaiomba Serikali pia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa, hapa huwa ni jambo moja tu kwenye mshahara wa Waziri ni jambo moja la kisera, nadhani kwa maelezo uliyotoa hapo mwanzo umeshakamlisha hoja yako moja.

Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimemsikia vema Mheshimiwa Reuben rafiki yangu, Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ya Bunge na ukereketwa wake katika kuona faida inapatikana kupitia uchumi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhesimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapungufu haya anayoyasema imedhamiria kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi pale Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapofanikisha hayo tumeweka pia na viwanda ikiwemo viwanda vile vya kuhifadhi samaki kwa sababu kinachowafanya watu na meli zao kubwa waondoke waende nchi za jirani ni kukosekana kwa miundombinu kwa maana ya *facilities.* Ninaomba Mheshimiwa Reuben kwa heshima kubwa na taadhima, aendelee kutuunga mkono na ukereketwa huu alionao wa kuhakikisha kwamba tunakamilisha jambo lile ili kusudi haya mapungufu yaishe na nchi yetu iweze kunufaika na kuwa na uhakika wa rasilimali zetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa ameketi kwa hivyo naamini amekubaliana na ufafanuzi wa huu. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nimeondoa kusudio langu la kushika Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nilikusudia kupata maelezo ya Waziri ya kina, lakini katika maelezo yake ya kufanya majumuisho na hasa pale aliposema kwamba wavuvi wa *Lake* Tanganyika waendelee na shughuli zao, hiyo ni *commitment* inatosha, kwa hivyo naondoa hoja yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami vilevile nilikusudia kushika Shilingi lakini baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nikubaliane tu kwamba naondoa hoja yangu, lakini ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri alete Muswada wa Dharura katika Bunge lijalo ili tuweze kutunga hicho chombo cha kusimamia Wakala.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Athman Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami baada ya maelezo ya Waziri, baada ya kusema na kutuhakikishia kabisa wavuvi wa Ziwa Tanganyika wataendelea kufanya shughuli zao bila kubugudhiwa, naondoa kabisa kusudio. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi siondoi kusudio la kushika shilingi ya Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri yanasababisha mpaka Wabunge wenzangu

wanaondoa nia ya kutoa Shilingi lakini nadhani anaelewa ninashika Shilingi kuhusiana na suala la herein. Naishika kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji tumelalamika sana katika michango yetu, tumejaribu kufanya *research* kwamba hereni hizi kununua mpaka kumuwekea ng'ombe masikioni haizidi Shilingi 300 lakini inatozwa Shilingi 1,700. Mtu atatumia Bilioni 15 azalishe Bilioni 52, hivi ni vitu ambavyo haviwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia amesema kuhusiana na chombo na amesema pia Mheshimiwa Rais hapendi taharuki, hii ni taharuki kubwa sana kwa wafugaji na umewaalika wako humu ndani. Sasa kama anataka niondoe Shilingi yangu, atoe maamuzi kama aliyoyatoa kwa *Lake* Tanganyika na mimi nitaondoa, asipotoa na nisiporidhika nitaomba kushika Shilingi ili Wabunge waniunge mkono. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kufafanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Kasheku Musukuma kwa uungwana wake wa kusema kwamba nimeeleza vizuri ila alitaka nitoe *statement* ya moja kwa moja. Katika maelezo yangu nimeeleza kwamba tutakachofanya mara baada ya kupita hapa ni kukutana, kujadiliana mimi na timu zote hizi za wadau. Waheshimiwa Wabunge, Chama cha Wafugaji Tanzania ambacho kiko hapa kikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mrida Mshota, tutakaa tujadiliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimsikiliza vizuri Mheshimiwa Musukuma bado tatizo lake lipo kwenye bei ndiyo hoja. Anazungumzia kwamba kwa nini mtu atumie kiasi kidogo kujipatia mahela mengi, sasa hii ni hoja inayowezekana kabisa. Ninaomba nimhakikishie ya kuwa hii hoja ya bei inawezekana, hana sababu ya kunishikia hii Shilingi na mshahara wangu, aniruhusu mimi hatua ya kwanza mara baada ya kumaliza hii ni kukaa na wadau kutafuta sasa suluhu ya jambo hili ya kudumu, tukatekeleze kinachowezekana kutekelezwa tusonge mbele. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo maelezo yangu ni hayo, kwamba hana sababu ya kunishikia Shilingi jambo lake ni bei, na jambo hilo liko vizuri, *under control,* tunaliweza, tunalimudu tutasonga mbele kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma naona umesimama.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama kweli haya maneno ndiyo usije ukatuzulia taharuki, nakubaliana na wewe kuondoa shilingi isipokuwa mifumo iwe shirikishi.

**MWENYEKITI:** Rudisha shilingi.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekurudishia shilingi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Koka, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nataka kumuomba Waziri anieleze katika bajeti iliyopita aliniahidi kwamba katika

ukarabati wa minada, aliahidi kukarabati minada mingi ikiwemo ya Jimbo la Arumeru Magharibi mnada wa Olokii, katika bajeti hii sikuona kabisa mnada huo. Naomba *commitment* yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hilo nalo ni la Jimbo la Arumeru. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. *(Kicheko)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi niseme nilikusudia kuondoka na Shilingi ya Mheshimiwa Waziri lakini baada ya maelezo yake na mengine yaliyobaki amesema tunaweza kuzungumza kesho, basi nimeamua kuondoa kusudio langu la kushika Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kupata maelezo ya kisera kutoka kwa Serikali, kuhusiana na Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 Sura ya Tatu ukurasa wa 25, inayoeleza umuhimu wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo lakini Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya 2010 kifungu cha (7), (8) na (9), lakini Kanuni ya Sheria hizi ya mwaka 2011, pia mwongozo wa mwaka 2021 wa utambuzi, usajili na ufatiliaji wa mifugo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunakubaliana umuhimu wa kufanya utambuzi, usajili na ufatiliaji wa mifugo, ukiangalia majadiliano kinachobishaniwa ni namna gani bora ambayo itanufaisha Serikali kwa maana ya jumla, lakini pia kwa wafugaji wenyewe. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo kwamba wameshafanya tathmini ninaamini katika kile kipindi ambacho tulisitisha zoezi kwa miezi mitatu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelezo, ninaamini ndipo kipindi walifanya tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kufahamu kama wote tutakubaliana umuhimu ni kwa nini Serikali isiingie yenyewe gharama ya kufanya sensa ya mifugo, kama walivyofanya kwenye sensa ya watu na makazi, kwa sababu mwanzo zoezi la kupiga chapa kwenye ngozi liligharamiwa na wafugaji, leo hili zoezi lingine ambalo lina gharama *barcode,* kwenye hiyo *electronic devices* bado mfugaji ndiyo anaingia gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini Serikali isione namna bora ambayo inaweza yenyewe ika-*incur* hizi *costs* ili sasa tufike kwenye namna ambayo tunaweza tukawasaidia wafugaji lakini pia tukasaidia lengo la kufanya utambuzi, usajili na ufatiliaji wa mifugo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Nusrat Hanje ni nzuri na nimemuelewa. Ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba haya yote tutakwenda katika *engagement,* kukaa kwa pamoja, tutashauriana njia iliyobora ya kutoka na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima ieleweke hili jambo katika utekelezaji wake ni lazima liwe na uendelevu wake *sustainability.* Kwa hiyo, tutakapokuwa tumekaa ni lazima tukae tujadiliane. Mheshimiwa Nusrat wala usiwe na hofu haya mawazo na fikra nzuri ulizonazo, tutakapokutana, tutashauriana, tutakwenda mbele kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Nimefurahi umeitaja sera, umeitaja sheria, ukataja na Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusratameridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, sasa nitawahoji kuhusu kifungu hiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............Sh. 997,695,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...............Sh. 1,928,039,000
Kifungu 1004 – *Research, Training and Extension Unit*...............................Sh. 15,978,325,800
Kifungu 1005 – *Information, Education and Communication*……………..………Sh. 411,538,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*…........................Sh. 398,375,400
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 462,116,400
Kifungu 1009 – *Legal Service Unit*…........................Sh. 336,650,000
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*…….........…………Sh. 377,990,000
Kifungu 1011 – *Environmental Management Unit*...Sh. 159,888,267
Kifungu 7001 – *Veterinary Service*........................Sh. 12,789,294,930
Kifungu 7003 – *Livestock Infrastructure Development Unit*……........…………..Sh. 335,280,000
Kifungu 7005 – *Veterinary Council of Tanzania*.......Sh. 375,464,000
Kifungu 8001 – *Livestock Production & Marketing*…..................................Sh.9,805,410,633
Kifungu 8002 – *Grazing Land Animal Feed Resources Development*……………………..Sh. 1,743,412,000
Kifungu 8003 – *Animal Breeders Rights Unit*……….......………….Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 – Sekta ya Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.....................Sh. 2,961,781,800
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit* .............Sh. 1,161,743,329
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……..Sh. 1,827,985,671
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……….......………….Sh. 406,682,000

Kifungu 1005 – *Legal Unit*……..................................Sh. 369,354,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 487,532,000
Kifungu 1007 – *ICT Unit*…………………..……………Sh. 362,018,000
Kifungu 1008 – *Fisheries Laboratory*……………….Sh. 1,322,060,000
Kifungu 1009 – *Environment Management Unit*…..Sh. 155,060,000
Kifungu 1010 – *Government Communication Unit*…..............................................Sh. 203,520,000
Kifungu 9001– *Fisheries Development Division*...Sh. 17,835,209,500
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development*…….Sh. 12,720,896,350
Kifungu 9003 – *Fisheries Aquaculture Research, Training Ext. Serv*……….…………..Sh. 9,189,165,350
Kifungu 9004 – *Fisheries & Aquaculture Infrastructure Development*………..………......Sh. 459,288,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 64 - Uvuvi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*........Sh. 1,986,000,000
Kifungu 1007 – *ICT Unit* ……….................................................Sh. 0
Kifungu 1009 – *Environment Management Unit*……..................Sh. 0
Kifungu 9001 – *Fisheries Development*…..……..Sh. 45,801,028,929
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development*........Sh. 27,502,831,071
Kifungu 9003 – *Fisheries Aquaculture Research, Training Ext. Serv*…..........................Sh. 800,000,000
Kifungu 9004– *Fisheries & Aquaculture Infrastructure Development*………..…………Sh. 58,322,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 99 - Mifugo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*........................Sh. 400,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...............Sh. 1,900,000,000
Kifungu 1004 – *Research, Training and Extension Unit*................................Sh. 15,600,492,750
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*……..………..Sh. 7,987,614,000
Kifungu 7003 – *Livestock Infrastructure Development Unit*..............................Sh. 550,000,000
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing*…................................Sh. 22,043,344,000
Kifungu 8002 – *Grazing Land & Animal Feed Resources Development*…Sh. 13,442,656,250

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati

ya Matumizi limekamilisha kazi yake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge limepitisha rasmi Makadilio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wote ambao wanamsaidia katika eneo la utendaji na tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa ahadi ambazo mmezitoa katika bajeti yenu pia ahadi nyingine ambazo mmewaahidi Waheshimiwa Wabunge hapa kutokana na michango yao. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ambayo inashughulika na Wizara hii, mmeisimamia

vizuri, mmetoa ushauri vizuri na tumeipitia wote taarifa ya Kamati hii, kwa kweli wamefanya kazi vizuri sana. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati hii na Wabunge wote ambao mmefanikiwa kuchangia wengine kwa maandishi wengine kwa kuzungumza, michango yenu haina shaka itaisaidia Wizara kuendelea kuboresha utendaji kazi wake katika kuhakikisha wanaondoa zile changamoto ambazo wananchi wanazipitia katika maeneo yetu, lakini pia wanashughulika na yale mambo tunatamani siyo tu kushughulika na changamoto za wananchi lakini kulifanya Taifa letu lisonge mbele, kwa hivyo mchango wa uvuvi, mchango wa mifugo kuongezeka katika Taifa letu. Kwa hiyo tunawashukuru sana wote.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kuna mambo machache ya kukumbushana naona ni kila wakati inabidi tuendelee kukumbushana, na hakuna jambo baya kwa sababu binadamu tumeumbiwa kusahau.

Waheshimiwa Wabunge, moja ya jambo la msingi sana, Siwa inapoingia Bungeni unaposimama unanyamaza, hata kama ulikuwa unaongea na jirani yako, ahirisha ulichokuwa unazungumza, kwa sababu Siwa ni alama ya Mamlaka. Kwa hiyo, usizungumze Siwa inapoingia Bungeni. Vivyo hivyo Siwa inapotoka Bungeni usizungumze kwa sababu ndiyo Mamlaka yako Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe hilo naona limeshika kasi sana sasa hivi na mimi kwa sababu huwa nakuwepo Bungeni nakaa kule nyuma, huwa natazama watu tunaendelea kuzungumza. Ukishasikia meza imepigwa pale tena huwa inapigwa *mic* ikiwa imewashwa, ile inaashiria kama ulikuwa unatembea elekea kwenye kiti chako ukakae kabla hujasikia Mheshimiwa Spika ya kwanza maana yake uwe umeshakaa kwenye kiti chako. Sasa ikiitwa ile ya kwanza ndiyo

watu wanakimbizana humu ndani kutafuta pa kukaa, halafu Siwa inaingia inafika mpaka pale, bado mtu anatafuta kiti chake.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba hapa siyo darasani lakini tumejiwekea utaratibu wa kuiheshimu Siwa inapoingia Bungeni na inapotoka, kwa hiyo ni muhimu sana kuzingatia hilo, hasa kwa sababu humu Bungeni wapo wageni wengi ambao huwa wanakuja kujifunza, tusipotoa heshima kwetu wenyewe tusitarajie heshima kutoka kwa watu wengine. Kwa hiyo tukumbushane hilo Waheshimiwa Wabunge.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo ni la msingi sana kipindi hiki cha Bajeti ni Kanuni zile zinazotuongoza kwenye michango, kwa kweli tunaendelea vizuri sana, lakini nadhani tuna changamoto kidogo kwenye Kamati ya Matumizi na namna ya kushughulika na Mafungu ya Bajeti. Tumeshakuwa na mazoea fulani kwamba kushika Shilingi ni mshahara wa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, nilishawakumbusha hapo awali shilingi hushikwa kwenye Fungu lolote linalohusu jambo lako, tofauti ni kwamba kwenye mshahara wa Waziri unapaswa kuzungumza suala mahsusi linalohusu sera. Mambo yale maalum ya Jimbo lako, kuna jambo hujafurahi sijui halijafanywa vizuri, halijatekelezwa, tafuta Kifungu kingine ambacho hakina uhusiano na mshahara wa Waziri, kule utaweza kuzungumza kuhusu soko halikujengwa, mnada haujaja kwenye Jimbo lako, tafuta Kifungu mahsusi. Kanuni zetu huwa nawakumbusha kila siku, Kanuni ya mshahara wa Waziri ni Kanuni ya 120 inasema suala mahsusi na la kisera tena moja siyo zaidi ya hapo.

Waheshimiwa Wabunge, Kifungu kinachofuata kinahusu kubadilisha, hapo nadhani huwa hatuendi sana kwa sababu hatutaki wenyewe kuanza kupendekeza mambo mengine.

Kifungu cha 122 inaongelea kuhusu kuondoa Shilingi kwenye Mafungu mengine yasiyohusu mshahara wa Waziri. Tafuta Kifungu mahsusi katolee Shilingi huko, ukija hapa una eneo mahsusi kwenye eneo lako hujasoma Kanuni mimi nitakurudisha hapa, kwa sababu ndiyo kazi yangu kusimamia utaratibu humu ndani ili Kanuni tulizojiwekea zifuatwe.

Waheshimiwa Wabunge, huwa nawaambia hiki Kifungu nikiwakumbusha kumbusha lazima naona hapo Mawaziri na Naibu Mawaziri wananiangalia wanawaza Mheshimiwa Spika hivi anatutaka nini? Lakini ndiyo Kanuni zetu tulizojiwekea. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo watakuwa wanaona sasa mimi hoja nilikuwa nayo kwenye Wizara hii nilitaka niliseme hili, tafuta Kifungu cha kuisemea kwa kutumia Kanuni inayohusika, na kwa kweli kusoma Kanuni na kuzishika ni kazi yako, hasa kama ukitaka mimi nikikaa hapa mbele ndiyo nikutafutie Kifungu cha wewe kushika Shilingi, hiyo itakuwa kidogo mtihani.

Waheshimiwa Wabunge, nimeona niwakumbushe hilo kwa sababu inaonekana bado hatujaielewa vizuri Kanuni yetu ya 122. Kwa hivyo, niwaombe tukasome sote Kanuni kuanzia Kanuni ya 120, Kanuni ya 121, Kanuni ya 122 na Kanuni ya 123 zinatuongoza kipindi hiki cha Bunge hili la Bajeti ili tuwatendee haki wananchi wetu. Mheshimiwa Waziri tunakutakia kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo umeyasema na mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyachangia hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu kwenye hoja ya Mheshimiwa Mpina nilikuwa nimemuagiza alete Ushahidi, nadhani ni muhimu nimpangie muda wa kuleta huo ushahidi ili jambo hili tuweze kufika mwisho siku ya Jumanne wiki ujayo,

niupate huo ushahidi halafu tutaweza kulifanyia kazi lile jambo ambalo Mheshimiwa Waziri wa Nchi aliliombea hapa Kuhusu Utaratibu na nitatoa Mwongozo wakati huo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Kamili Asubuhi.

*(Saa 1.28 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*